Nipashe

Jumanne Novemba 8, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581123

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US


Nipashe TESA
Jumanne Novemba 8, 2022
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI
Monica, mwalimu wa ufundi ujenzi anayevuta wasichana kuwa wajenzi
NDIVYO ULIVYO UMUHIMU BIMA YA AFYA KWA WOTE
SAYANSI
NA DK. FELICIAN B. KILAHAMA
NGORONGORO NI ZAIDI YA WANYAMA, WATU (2)
Kumesheheni maajabu viumbe adhimu na adimu, nyayo mtu wa mwanzo, mchanga unaotembea

UKURASA 13

SUPA JACKPOT

TZS.1,048,875,802

KWA TZS. 1000 TU!

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SportPesa.CO.TZ

PIGA *150*87#



**Mbunge** mwingine kuhojiwa kortini kesi ya CHADEMA

UKURASA 7



# NI SHUJAA

• **Kijana** mvuvi aliyeokoa abiria 24 apewa mamilioni, Samia aagiza aajiriwe jeshini, mwenyewe asimulia rubani alivyopoteza maisha • **CHADEMA**, ACT: Serikali iwajibike... *Endelea ukurasa 2*



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akiongoza kuaga miili ya watu 19 waliofariki dunia kwa ajali ya ndege ya Shirika la Precision Air, Uwanja wa Kaitaba, Bukoba jana. **PICHA: OWM**

## Rais Samia kuongoza mjadala wa COP27 leo

UKURASA 3



## Bunge laagiza CAG afanye ukaguzi maalumu HESLB

UKURASA 3

MICHEZO SIMBA QUEENS KUMENOGA CAF UK.32

KATUNI UK.6

# Simulizi ya kijana shujaa aliyeokoa abiria

**Na Restituta Damian,** BUKOBA



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akimpongeza na kumfariji kijana Jackson Majaliwa kwa ushujaa wake wa kuwahi katika eneo ilipotokea ajali ya ndege na kuwaokoa abiria wakati wa kuaga miili ya watu waliofariki kwa ajali hiyo, katika Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba jana. **PICHA: OWM**

"ILIKUWA ndoto yangu ya muda mrefu kufanya jambo kubwa kwa ajili ya taifa langu, imekuja wakati wa majonzi lakini ninajiona shujaa kwa nchi yangu baada ya kuwaokoa abiria 24 kwenye ndege iliyopata ajali Ziwa Victoria mjini Bukoba," kijana Majaliwa Jackson (20) anasema.

Akizungumza na Nipashe jana baada ya serikali kumtangaza kama shujaa na kumpa zawadi ya Sh. milioni moja mbele ya umma na baadaye Rais Samia Suluhu Hassan kupiga simu na kuahidi kumpa Sh. milioni tatu, Jackson alisema alitamani kuwaokoa watu wote, lakini alipoteza fahamu wakati akiendelea na uokoaji.

Jackson anasema akiwa kwenye shughuli zake za kuanika dagaa ambazo anazifanya kila siku kwenye Mwalo wa Kisiwa cha Msila, aliona ndege ikitokea upande ambao haujazoeleka kwa ndege zinazokwenda kutua Uwanja wa Ndege wa Bukoba, ndipo akaanza kufuatilia kwa karibu kujua undani wa utofauti aliokuwa ameubaini.

"Nilivyoona hivyo, nikajua hii si kawaida. Baada ya muda mfupi, nikaona imeanguka ziwani, nikawaambia wenzangu ajali ile pale, tukachukua mtumbwi tukiwa wanne ili tukawaokoe waliomo ndani," alisema.

Aliongeza kuwa walipokuwa wanakaribia eneo la tukio, wenzake walishindwa kuendelea kuogelea lakini aliendelea hadi akafikia ndege.

Alisema kuwa baada ya kuifikia ndege hiyo, alikwenda moja kwa moja mbele ya ndege na rubani alimwonyesha ishara kuwa avunje kioo cha mbele kwa kuwa maji yalikuwa yanaingia kidogokidogo.

Kijana huyo alisimulia kuwa baada ya kupewa maelekezo hayo, alirejea juu ya maji kutafuta kitu cha kuvunja kioo husika lakini alikuta maelekezo ya serikali kuwa wasivunje ndege hiyo ili maji yasiingie ndani.

Kwa mujibu wa kijana huyo, alirudi kwa rubani akamjulisha kilichoamuliwa, rubani naye akimwelekeza mlango wa dharura ili aufungue ndipo alikwenda akafanikiwa kufungua kwa kupiga mlango ukafunguka, akaanza kuwatoa watu mmoja baada ya mwingine.

Shujaa huyo anasema kuwa iwapo angevunja kioo cha mbele, angeingia ndani ya ndege na kuokoa watu wengi zaidi.

"Kwa bahati mbaya, ile kasia ilinigonga nikapoteza fahamu. Sikujua kilichoendelea kuanzia hapo hadi nikajikuta nimelazwa hospitalini na nimeletwa hapa uwanjani baada ya kupata nafuu," alisema.

### RAIS AMWAJIRI

Jana Ofisi ya Waziri Mkuu ilitoa taarifa kuwa Rais Samia ameagiza kijana Jackson aliyeona ndege ikianguka na kuamua kwenda kuokoa watu, akabidhiwe kwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na aingizwe katika Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ili apate mafunzo zaidi ya uokoaji.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alitanga hayo wakati akiongoza wananchi kuaga miili ya watu 19 waliofariki dunia katika ajali hiyo ya ndege ya Shirika la Precision Air katika Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba.

Ajali ya ndege hiyo aina ya ATR 42-500 yenye namba za usajili 5H-PWF ilitokea juzi (Novemba 6, mwaka huu) majira ya saa mbili asubuhi baada ya kushindwa kutua uwanjani humo ikiwa na abiria 39, marubani wawili na watoa huduma wawili.

Vilevile, kati ya waliokolewa, abiria ni 22, watoa huduma wa ndege wawili huku waliofariki ni abiria 17 na marubani wawili.

### GHARAMA MAZISHI

Majaliwa alisema Rais Samia ameagiza kuwa mazishi ya waliofariki dunia kwenye ajali hiyo yatagharamiwa na serikali na kuelekeza wakuu wa mikoa ambako miili hiyo itapelekwa, kusimamia shughuli hiyo.

### PRECISION AIR

Mkurugenzi wa Shirika la Precision Air, Patrick Mwanri, alisema jana tayari ndege imeshatolewa kwenye maji na itafanyiwa matengenezo ili irejee katika safari zake kwa wakati.

Awali akitoa salamu za rambirambi, Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Albert Chalamila aliiomba serikali kuweka mafunzo maalum yatakayowahusisha wavuvi katika kupatiwa mbinu za uokozi na dharura katika maji.

Chalamila pia aliwapongeza wavuvi wa eneo hilo kwa kushirikiana na wananchi katika shughuli za uokoaji zilizofanikisha kuwapata watu 26 wakiwa hai.

Kiongozi huyo wa mkoa pia alizipongeza kampuni mbalimbali kwa kushiriki katika kutoa vifaa vilivyosaidia katika shughuli za uokoaji.

Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Innocent Bashungwa, aliahidi kupitia vyombo vya ulinzi na usalama kuwa watahakikisha wanaweka mpango mkakati wa kuimarisha mfumo wa uokoaji katika maeneo mbalimbali ya dharura.

Vilevile, Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, alisema wamepokea maoni ya watu mbalimbali kutokana na tukio hilo, akiahidi watayatumia kuboresha huduma za usafirishaji nchini.

Alisema tayari wamesharuhusu ndege ndogo za abiria wasiozidi 40 kutua kwenye Uwanja wa Ndege Bukoba wakati taratibu za kuondoa ndege hiyo kwa ajili ya matengenezo na muda si mrefu utaendelea na shughuli zake za usafirishaji.

### MAOMBOLEZO

Mji wa Bukoba jana ulitawaliwa na majonzi baada ya miili ya watu 19 kuwasili katika Uwanja wa Kaitaba huku mamia ya watu waliokuwapo wakiangua vilio.

Majeneza yenye miili yalibebwa na askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) na kuingizwa uwanjani kisha kupangwa katika eneo maalum huku baadhi yakiwa na picha za marehemu.

Baada ya viongozi wa kiserikali kutoa salamu, walipita mbele ya majeneza kwa ajili ya kutoa heshima za mwisho wakiongozwa na Waziri Mkuu, wakifuatiwa na wanafamilia na waombolezaji wengine.

### WATAKA UWAJIBIKAJI

Wakati huo wanasheria na wanasiasa wameitaka serikali kukiwajibisha kitengo cha maafa kilichoko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushindwa kutimiza wajibu wa kuokoa watu na mali zao kwenye ajali hiyo ya ndege.

Wamesema ni aibu kwa kazi hiyo kufanywa na wananchi ilhali wapo wenye utaalamu ambao wanalipwa mishahara na posho mbalimbali.

Kwa mujibu wa taarifa kwa vyombo vya habari iliyotolewa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa Timu ya Wanasheria Watetezi wa Mazingira kwa Vitendo (LEAT), Dk. Nshala Rugemeleza, vyombo vya uokoaji vya serikali vimeonyesha udhaifu mkubwa kwa kushindwa kuokoa watu katika ajali hiyo.

Alisema timu hiyo ilitarajia kuwa uwezo wa vyombo vya uokozi umeimarika kutokana na makosa ya miaka 26 iliyopita ilipotokea ajali ya MV Bukoba na kuua mamia ya watu.

"Kupitia ajali hiyo imeonyesha namna gani LEAT inataka kuwajibishwa kwao mara moja na si kutumia njia za geresha za kuunda tume na kamati za uchunguzi na kusema tuendelee kusubiri matokeo ya uchunguzi," alisema Dk. Nshala ambaye ni Rais mstaafu wa Chama cha Wanasheria wa Tanganyika (TLS).

Alisema imesikitisha kuona wavuvi ndiyo waliokoa watu huku vyombo vya umma vya uokoaji havina uwezo wa kufanya kazi hiyo.

Vilevile, alidai serikali inatambua matatizo ya uwanja huo, kama vile kukosa taa na kuwa na njia fupi za ndege, hali inayowalazimu marubani kutumia uzoefu wao kutua ikiwamo kukanyaga breki kwa nguvu ili ndege kutopitiliza nje ya njia lakini inashindwa kuzifanyia maboresho.

"Si mara moja au mbili mwonekano dhaifu wa uwanja huo wakati wa mvua umelazimisha ndege kuzunguka juu ya Ziwa Victoria na anga ya Bukoba kusubiri hali ya hewa kuboreka. Marubani mara nyingi hulazimika kutumia uzoefu wao na kutua katika hali hiyo mbaya ya hewa," alisema.

### ACT-WAZALENDO

Chama cha ACT-Wazalendo nacho kimewataka viongozi wenye wajibu wa kusimamia uokoaji kujiuzulu nafasi zao kwa kuwa wamekuwa chanzo cha tatizo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Idara ya Mawasiliano ya chama hicho jana, kimewataka Waziri wa Uchukuzi na Mambo ya Ndani kuwajibika kutokana na kinachokiita uzembe uliofanywa na watumishi walio chini yao huku kikimtaka Waziri Mkuu Majaliwa ajiuzulu kwa udhaifu ulioonyeshwa na kitengo cha uokoaji kilichoko kwenye ofisi yake.

### CCM NA WAVUVI

Katibu wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Shaka Hamdu Shaka, aliwapongeza wananchi wa Kagera kwa moyo walionyesha kusaidia uokoaji katika ajali hiyo kwa kuwa kitendo hicho kimethibitisha umoja, upendo na mshikamano wa Watanzania.

Shaka alisema chama hicho kinatoa shukrani kwa wavuvi na wananchi waliokuwapo eneo la tukio kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama kuokoa uhai wa baadhi ya watu.

"Ndugu zangu tumeishangaza dunia, umoja tuliouonyesha, mshikamano tuliouonyesha katika jambo hili tusishangae yatazungumzwa mengi, yatasemwa mengi, lakini huo ndiyo utamaduni wetu wa Afrika na huo ndiyo utamaduni wetu Watanzania, tumekuwa kielelezo kizuri kwenye kuonyesha umoja na mshikamano kwenye mambo magumu," alisema Shaka.

### CHADEMA NA UTAYARI

Katika taarifa ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) iliyotolewa na John Mrema, Mkurugenzi wa Mawasiliano na Itifaki wa Mambo ya Nje, chama hicho kinaeleza kuwa ajali hiyo inaonyesha Tanzania haina uwezo wa kukabiliana na majanga kwa wakati yanapotokea.

"Laiti kama tungekuwa tumejiandaa, madhara ya ajali hiyo yasingekuwa makubwa kama ambavyo tumeshuhudia. Tunawapongeza wananchi hasa wavuvi ambao waliwahi mapema eneo la ajali na kutoa huduma ya kuokoa abiria pamoja na ukweli kuwa hawakuwa na vifaa," alisema Mrema kupitia taarifa yake hiyo.

Alisema chama chao kwa hatua ya sasa, kinashauri mamlaka kwenye maeneo yaliyo na viwanja vya ndege zitoe elimu namna ya kuokoa watu kwenye ajali za ndege ili wawe na utayari wa kutoa huduma ya kwanza pindi maafa yanapojitokeza.

***Taarifa za ziada na Jenifer Gilla (DAR).***

## HABARI KITAIFA



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi akimsikiliza Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BOT), Prof. Florens Luoga, alipofika Ikulu Zanzibar na wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa BOT kwa mazungumzo jana. **PICHA: IKULU**

# Bunge laagiza CAG afanye ukaguzi maalumu HESLB

**Na Richard Makore,** DODOMA

BUNGE limesema limejiridhisha hakukuwa na upinzani mkali kwa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) kutoa ushirikiano kwa kamati iliyoundwa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, kuchunguza mifumo ya utoaji mikopo kwa wanafunzi hao.

Vilevile, chombo hicho kimeazimia Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kufanya ukaguzi maalum HESLB ili kuchunguza uwajibikaji wao kifedha.

Uamuzi huo ulifikiwa jana baada ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuwasilisha taaarifa yake mbele ya Bunge ya kujadiliwa na wabunge huku wakivutana kiasi cha kuwa na maombi ya taarifa kwa Spika mara kwa mara lakini baadaye walitoa maazimio.

Wiki iliyopita Waziri wa Elimu, Prof. Mkenda aliliambia Bunge jijini Dodoma kwamba aliunda tume kuchunguza mifumo ya utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu, lakini alikumbana na upinzani kutoka kwa bodi hiyo.

Kutokana na kauli hiyo, Spika Dk. Tulia Akson aliagiza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuiita bodi hiyo jijini Dodoma kuihoji kwanini inakuwa na kiburi kwa waziri.

Wiki iliyopita bodi hiyo ikiongozwa na Mwenyekiti wake, Prof. Khamis Dihenga ilihojiwa na kuwasilisha vielelezo vyake vya namna ilivyotoa ushirikiano.



Kaimu Mwenyekiti wa kamati hiyo, Musa Sima, akiwasilisha taarifa ya kamati yake baada ya kukutana na bodi hiyo, alisema baada ya kuhoji pande zote walibaini hakukuwa na ushahidi wowote wa kumkwamisha waziri.

Hata hivyo, alisema kamati ilibaini kuwapo mawasiliano duni baina ya wizara na bodi, wizara ikishindwa kutoa taarifa rasmi ya maandishi kwenda kwa bodi kuhusu kupokea kamati iliyoundwa na waziri ili ianze kazi.

Sima alisema bodi hiyo isingeweza kufanya chochote ikiwamo kuipokea kamati na kuipa ushirikiano bila kuwapo maelekezo ya maandishi kutoka wizarani.

Spika alimpa nafasi Waziri Mkenda kuzungumza, naye akisema bodi inampa ushirikiano wote na kamati aliyounda imeanza kazi yake kuhakikisha utoaji wa mikopo unawajali watoto wote wa Kitanzania.

### BAJETI FINYU

Mbunge wa Ubungo (CCM), Prof. Kitila Mkumbo akichangia hoja hiyo jana bungeni, alisema bajeti ya HESLB inatosha kukopesha wanafunzi 42,000 pekee, huku wengine takribani 40,000 hawawezi kupata mikopo kwa mwaka 2022/23.

Alisema kila mwaka wanafunzi wanaodahiliwa katika vyuo vya juu wanaongezeka hatua inayosababisha bodi kushindwa kuwakopesha wote.

Aliongeza kuwa bodi haina tatizo lolote isipokuwa inashindwa kutoa mikopo kwa wanafunzi wenye sifa kutokana na ufinyu wa bajeti inayopewa kila mwaka.

Alikumbusha kuwa kwa mwaka 2022/23 bodi hiyo imetengewa Sh. bilioni 570, kiasi ambacho haktoshi na hivyo kuzua malalamiko wanafunzi kukosa mikopo.

Akichangia hoja ya kamati, Mbunge wa Nzega Vijijini (CCM), Dk. Khamis Kigwangalla alimtaka Prof. Mkenda kujitathmini kama anatosha katika nafasi aliyonayo.

Hata hivyo, hoja hiyo ilimlazimu Spika Dk. Tulia kusimama na kuweka bayana kwamba wawili hao (Dk. Kigwangalla na Waziri Mkenda) hawana uhusiano mzuri kwa muda mrefu, hivyo akamtaka Dk. Kigwangalla kuchangia suala hilo kulingana na hoja ya kamati na siyo uhusiano baini yao.

Mbunge wa Bunda Vijijini (CCM), Mwita Getere pia alisimama na kumpa taarifa Dk. Kigwangalla kwamba wakati anachangia, aseme wazi kwamba ana ugomvi binfasi na Prof. Mkenda.

Licha ya kupewa taarifa hiyo, Dk. Kigwangalla aliendelea kuchangia huku akitaka Waziri Prof. Mkenda kujitathmini, akidai alilidanganya Bunge, jambo ambalo lilimlazimu Spika Dk. Tulia kuingilia kati na kumtaka asiendelee kuchangia kwa kuwa hata muda wake ulikuwa umeisha.

Spika pia alimwambia Dk. Kigwangala kwamba kauli yake hiyo alikuwa ameishaitoa katika mitandao ya kijami hata kabla ya kuchangia bungeni jana, hivyo alikuwa tayari ameshamhukumu Prof. Mkenda.

Baada ya wabunge kujadili taarifa ya kamati hiyo, Bunge liliazimia Tume ya Prof. Mkenda iendelee kufanya kazi huku likiagiza CAG, kufanya ukaguzi maalum kwa bodi hiyo kuhusu mikopo inayotolewa kwa wanafunzi wa elimu ya juu.

# Samia kuongoza mjadala COP27

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Samia Suluhu Hassan leo ataongoza mjadala wa wakuu wa nchi 12, kuhusu nishati mbadala, kwenye mkutano wa 27 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Kimataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP27), ulioanza juzi jijini Sharmel El Sheik, nchini Misri.

Mkutano huo utawashirikisha wakuu wa nchi zaidi ya 100 na utakuwa na washirika wengine kutoka serikali, mashirika yasiyo ya kiserikali na sekta binafsi 35,000.

Mdahalo huo utazungumzia namna ya kuziwezesha Nchi za Kusini mwa Afrika kutumia vyema nishati mbadala ambayo ni safi kwa mazingira na kuachana na ile chafu ambayo ni tishio kwa usalama wa watu na mazingira.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa Wizara ya Nishati jana, mdahalo huo ni muhimu kutokana na nia ya ulazima wa kupunguza uzalishwaji wa kaboni kwa nchi za Afrika kwa gharama nafuu, ikiwamo kuwapelekea vifaa wanavyoweza kuvimudu ili kuleta maendeleo ya Afrika na matarajio ya hali ya hewa.

Mkutano huo ulioanza Novemba 6, unatarajiwa kumalizika Novemba 18 na unafanyika Afrika kwa mara ya kwanza huku Mwenyekiti wa ujumbe kutoka Afrika ni Ephrahim Shitima wa Zambia.

Afrika inakwenda na ajenda sita muhimu katika kukabili mabadiliko ya tabianchi ambayo ni utekelezaji wa ahadi ya Dola bilioni 100 za Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi iliyotolewa mwaka 2009 na nchi zinazoongoza kwenye uzalishaji wa hewa ukaa duniani.

Nyingine ni jitihada za kupunguza joto duniani na kuzuia lisifike nyuzijoto 1.5, fidia kwa nchi zilizopata majanga yaliyosababishwa na mabadiliko ya tabianchi kama ukame, mafuriko, uharibifu wa miundombinu, vifo, majeruhi na watu kukosa makazi.

Ajenda nyingine ni kuzitaka nchi zilizoendelea kupitia Taasisi ya Umoja wa Mataifa kuhusu Mkataba wa Kudhibiti Mabadiliko ya Tabianchi (UNFCCC) na makubaliano ya Paris kusaidia nchi zinazoendelea kumudu gharama za kukabili mabadiliko ya tabianchi.

Kwa mujibu wa mwenyekiti huyo, kuhimili mabadiliko hayo ni njia nzuri kwa uchumi kwa kuwa uwekezaji wa Dola za Marekani trilioni 1.8 kati ya mwaka 2020-2030 utazalisha Dola za Marekani trilioni 7.1.

Katika mkutano wa COP26 nchi zilizoendelea ziliahidi kuongeza mara mbili msaada wa kifedha wa Dola za Marekani bilioni 40 kwa mwaka, lakini bado hazijatekeleza.

Pia namna nchi zinavyoweza kuhama kutoka matumizi ya nishati chafu kwenda kutumia nishati safi ambayo ni gesi, joto ardhi, jua na upepo, huku nchi nyingi zikiwa na vyanzo vya nishati vya mkaa wa kuni, makaa ya mawe na umeme unaozalishwa kwa maji.

Wiki iliyopita, Rais Samia alifungua kongamano lililojadili mada za upatikanaji, upataji na unafuu wa nishati mbadala wa tungamotaka (kuni na mkaa), mtungi wa gesi ya kupikia kila nyumba, athari za kiafya zitokanazo na nishati ya kupikia, nishati ya kupikia na ustawi wa wanawake na ugharamiaji wa nishati safi ya kupikia.

Kwa mujibu wa taarifa za Umoja wa Mataifa, nchi za Afrika zinazalisha hewa ukaa kwa asilimia 0.04, huku mtu mmoja kwa Tanzania akizalisha asilimia 0.22 na Marekani na China wakizalisha asilimia 26.


**LEGENDS AUCTION MART AND GENERAL BROKER LIMITED**

**LEGENDS AUCTION MART & GENERAL BROKERS** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya **ALLIANCE FINANCE CORPORATION LIMITED** tunatoa notisi ya kulipa deni kwa wadaiwa wafuatao ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili,Vinginevyo, tutafanya mnada wa hadhara wa kuuza dhamana zao za magari yaliyopo Vingunguti Dar es salaam na Sinai Mabatini SIKU YA TAREHE 22/11/2022 kuanzia saa tano kamili asubuhi na kuendelea

| S/N | JINA LA MTEJA | MODEL | USAJILI | MAHALI LILIPO |
|---|---|---|---|---|
| 1. | TAI DIVE LIMITED | LPK2518Tipper | T590DSM | DAR ES SALAAM |
| 2. | MERKIOR FABIAN NDEMERA | LPO10.2t/52 | T659DPS | DAR ES SALAAM |
| 3. | SAMWEL KISAKA MZAVA | LPK 2519 | T598DMK | MWANZA |
| 4 | SASN AUTO GARAGE COMPANY LIMITED | NOVUS 340HP | T275DVM | DAR ES SALAAM |
| 5 | ISAYA LWIDIKO SANGA | LP909Bus | T424DNM | DAR ES SALAAM |
| 6 | YAMIN MOHAMED SULEIMAN | UTRA BUS | T728DVN | DAR ES SALAAM |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo
2. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14 na ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali, hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwishailipa
3. Gharama ya kukagua na kuona magari ni ya mnunuzi pamoja na kuhamisha umiliki ni ya mnunuzi.
4. Hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa yeyote akatayejaribu kuharibu mnada huu.

POSTAL HOUSE | 5TH FLOOR, OFFICE NO. 1507 | PLOT NO. 6/7
OHIO STREET / GHANA AVENUE | P.O.BOX 80310 - DAR ES SALAAM
MOBILE: 0714939933 | 0788411524 | 0763243900
Email:legendsab20@gmail.com

117136102

RIPOTI MAALUM -2

# Kutoka kuwa wazalishaji wa chakula hadi kulia njaa

• Profesa aipa mbinu serikali kunusuru wananchi



Saida Salehe, mkazi wa Kijiji cha Sindeni akiingiza maji jikoni kwake. **PICHA ZOTE: JENIFER GILLA**

**Na Jenifer Gilla,** aliyekuwa

HANDENI

***SEHEMU** ya kwanza ya ripoti hii jana ilikuwa ufafanuzi wa wakulima na maofisa wa serikali wilayani Handeni kuhusu ukame uliolikumba eneo hilo na madhara yake. Endelea kufuatilia sehemu ya mwisho kujua mustakabali wake.*

Mratibu Mradi wa Usalama wa Chakula wa Shirika la Kimataifa la Save the Children Mkoa wa Tanga, Anania Josia, anasema wamekuwa wakigawa vyakula kwa shule za msingi 53 kwa wilaya za Mkinga na Handeni, ambacho wanahakikisha kila wanapokitoa kinawasaidia kwa kipindi cha miezi mitatu hadi sita ili kukabiliana na uhaba wa chakula kwa wanafunzi.

"Pia tumetoa miongozo kwa walimu ya namna ya kuwapa wanafunzi hao chakula kwa kuwa walikuwa wanawalisha bila mpangilio maalum, matokeo yake chakula cha kutosha miezi mitatu hadi minne kinatumika kwa mwezi mmoja," anasema.

Vilevile, Josia anabainisha kuwa wanawajengea uwezo wa namna ya kufuga kuku, sungura na kulima mboga za majani kupitia viongozi wao na kutoa mbegu na vifaranga vya kuku 1,000 kwa kata tisa na chakula cha mifugo cha kuanzia kinachotosheleza mahitaji ya mwezi mmoja pamoja na chanjo na dawa za mifugo hiyo.

**KIINI CHA TATIZO**

Prof. Pius Yanda kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, aliyebobea katika masuala ya mabadiliko ya tabianchi, anasema kinachoshuhudia Handeni na maeneo mengine nchini, ni matokeo ya mabadiliko ya tabianchi yaliyosababisha mvua kutotabirika, kunyesha kwa kiwango cha chini au cha juu tofauti na kinachohitajika, hivyo kuziathiri shughuli za kilimo.

> **"Jamii inahitaji kuwezeshwa kielimu na kiteknolojia ili kuachana na kilimo cha kutegemea mvua na kuhamia kwenye kilimo cha kisasa, kikiwamo cha umwagiliaji, kutumia makopo na kilimo cha muda mfupi.**



Mkulima wa Kijiji cha Sindeni, Selemeni Hamza, akionesha mashamba yalivyoathiriwa na ukame.

Anasema mabadiliko hayo pia yanasababisha kuwapo joto kali linaloathiri ukuaji wa mazao, kuwa na ukame na kukauka kwa vyanzo vya maji.

Ripoti ya Jopo la Kiserikali la Kimataifa linaloshughulika na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi (IPCC) iliyotolewa Agosti mwaka jana, inatahadharisha kuwa kama joto hilo lisipodhibitiwa na kufikia ongezeko la nyuzi joto 1.5 kutoka usawa wa bahari, hali itakuwa mbaya zaidi.

**NINI KIFANYIKE?**

Prof. Yanda anasema ili kukabiliana na shida hiyo, jamii inahitaji kuwezeshwa kielimu na kiteknolojia ili kuachana na kilimo cha kutegemea mvua na kuhamia kwenye kilimo cha kisasa, kikiwamo cha umwagiliaji, kutumia makopo na kilimo cha muda mfupi.

"Vilevile, wakulima wawezeshwe kiuchumi ili kumudu gharama za kilimo hicho. Pia wapewe misaada ya chakula cha dharura hasa kipindi hiki ambacho shughuli za kilimo zimesimama kutokana na uhaba wa mvua na ukame," mtaalamu huyo anashauri.

Prof. Yanda ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa IPCC, anasema ili kutimiza hayo, Tanzania inahitaji kufikiwa na fedha za mfuko wa kusaidia nchi maskini kujikimu pale zinapopata majanga yatokanayo na mabadiliko ya tabia nchi (Loss and Damage), yakiwamo mafuriko na njaa.

"Ninafikiri hiki ni moja kati ya vitu vitakavyojadiliwa kwenye Mkutano wa 27 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Kimataifa Mabadiliko ya Tabianchi (COP27). Hii itaisaidia serikali katika utekelezaji wake pale ambapo jamii itapitia changamoto hizo," anafafanua.

Prof. Yanda pia anashauri kuendelea kufanyika uhamasishaji wa kutosha wa kutunza mazingira ikiwamo kuhifadhi misitu anayoitaja ina mchango mkubwa katika kunyonya hewa ukaa, kuleta mvua na kuzuia madhara yatokanayo na mafuriko, ukiwamo mmomonyoko wa udongo.

Kwa mujibu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Maendeleo (UNDP), Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazoendelea kuathiriwa na mabadiliko ya tabianchi kama vile mafuriko na ukame ambayo yameathiri kwa kiasi kikubwa utendaji wa kiuchumi na kuzorotesha juhudi za kupunguza umaskini.

Athari zinarudisha nyuma jitihada mbalimbali zinazofanywa na serikali kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Juni 1999-2025 yenye dhima kuu ya kupunguza walau nusu ya watu wanaoishi katika umaskini na kuwafanya waishi kwenye uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

UNDP inabainisha katika ripoti yake hiyo kuwa karibu asilimia 80 ya Watanzania wanategemea kilimo kuendesha maisha yao, kipato na ajira.

**MIKAKATI KITAIFA**

Tanzania kupitia Mpango Kabambe wa Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi (NDC) imeahidi kupunguza athari hizo, ikiwamo ukame na mafuriko.

Baadhi ya mambo ambayo nchi imeahidi kuyafanyia kazi ni kuongeza kiwango cha uboreshaji wa ardhi ya kilimo na usimamizi wa rasilimali za maji, pia kuongeza tija kwenye kilimo kupitia afua za kilimo kwa kuzingatia hali ya hewa.

Mikakati mingine inajumuisha kuwasaidia wakulima wadogo wanapopata majanga yanayohusiana na mabadiliko ya tabianchi, ikiwamo kuwapatia bima za mazao.

Ili kutekeleza mpango huo, zinahitaji dola za Marekani bilioni 19.23 kutoka Mfuko wa Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi (Adaptation Fund).

## HABARI KITAIFA

# Tril. 43.2/- bajeti 2023/24

**Na Richard Makore,** DODOMA

SERIKALI inatarajia kukusanya na kutumia jumla ya Sh. trilioni 43.2 kwa mwaka wa fedha 2023/24 ikilinganishwa na makadirio ya Sh. trilioni 41.4 kwa mwaka 2022/23 sawa na ongezeko la asilimia 4.4.

Akiwasilisha Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2023/24 na Mwongozo wa Bajeti kwa mwaka 2023/24, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema ongezeko hilo limezingatia mwenendo halisi wa ukusanyaji wa mapato ya ndani na jitahada zinazoendelea kuchukuliwa na serikali za kuongeza mapato.

Alisema ongezeko hilo limezingatia mahitaji yasiyoepukika kama mikataba ya kugharamia miradi mbalimbali, deni la serikali na mishahara ya watumishi wa umma.

Alisema mwaka 2023/2024, mapato ya ndani yanakadiriwa kuwa Sh. trilioni 31 sawa na asilimia 71.7 ya bajeti yote.

Aidha, alisema washirika wa maendeleo wanatarajiwa kuchangia Sh. trilioni 4.5 sawa na asilimia 10.9 ya bajeti na kwamba serikali inatarajia kukopa Sh. trilioni 5.6 kutoka soko la ndani ambazo zinajumuisha Sh. trilioni 3.5 kwa ajili ya kulipia hatifungani na dhamana za serikali zinazoiva na Shilingi trilioni mbili, kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo.

Kadhalika, mikopo ya masharti ya kibiashara kutoka nje inatarajiwa kuwa Sh. trilioni 2.1 baadhi ya mikakati itakayotumika katika kufikia lengo la makusanyo ya mapato ya ndani ni pamoja na kuendelea kuwatengea wafanyabiashara na watoa huduma wadogo maeneo maalum kwa lengo la kukuza biashara zao.

Dk. Nchemba aliliambia Bunge kuwa matumizi ya serikali yanakadiriwa kuwa Sh. trilioni 43.2 kati ya hizo, Sh. trilioni 28.2 ni matumizi ya kawaida na Sh. trilioni 15 ni matumizi ya maendeleo, sawa na asilimia 34.7 ya bajeti.

Aidha, alisema kutokana na matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, ni dhahiri kuwa gharama za utoaji huduma za jamii zitaongezeka kutokana na ongezeko la idadi ya watu nchini kutoka watu 44,928,923 mwaka 2012 hadi 61,741,120 mwaka huu.

Aliwataka maofisa masuuli kuzingatia kikamilifu maelekezo yote yaliyopo kwenye mwongozo wakati wa uandaaji, utekelezaji na ufuatiliaji na tathmini ya mpango na bajeti.

Miongoni mwa maelekezo hayo na kuandaa bajeti ya miradi ya maendeleo kwa kuzingatia vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2023/2024 na kipaumbele cha bajeti kiwe ni ukamilishaji wa miradi ya maendeleo inayoendelea kabla ya kuanzisha miradi mipya.

Maelekezo mengine ni kutenga bajeti ya kuandaa miradi inayoweza kutekelezwa kwa utaratibu wa ubia baina ya Sekta ya Umma na Binafsi (PPP).

Alitaka miradi ya PPP kupewa msisitizo ili kupunguza utegemezi wa bajeti ya serikali katika kutekeleza miradi ya maendeleo.Alisema serikali inaendelea kukamilisha taratibu za mapitio ya sheria ya PPP ili kuifanya wezeshi katika utekelezaji.

Maelekezo mengine ni pamoja na kuzingatia waraka wa mkuu wa utumishi wa umma namba mbili wa mwaka 2021 kuhusu utaratibu wa kutumia magari, aina na stahili za magari kwa viongozi katika utumishi wa umma.




## NOTISI YA SIKU 14/ TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**AMA'Z AUCTION MART & GENERAL BROKES LIMITED, STEAM GENERATION RECOVERIES LTD na MBUZAX AUCTION MART AND COMPANY LIMITED** Kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na **MWANGA HAKIKA BANK LIMITED**, tutauza kwa njia ya Mnada wa hadhara mali/dhamana za wadaiwa wake kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali hapo chini. Mnada utafanyika mahali dhamana zilipo baada ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya Notisi /Tangazo hili endapo hawatalipa madeni yao.

| NA | JINA LA MDAIWA | JINA LA MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE NA SAA YA MNADA | KAMPUNI/DALALI HUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | SIKITU ABDALLAH MOHAMED | SIKITU ABDALLAH MOHAMED | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI Na.TMK003190, ARDHI Na.TMK/MKW/MAK11/176 | MAKANGARAWE, WILAYA YA TEMEKE, DAR ES SALAAM | 03-12-2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | AMA'Z AUCTION MART & GENERAL BROKES LIMITED |
| 2 | SAIDI ALLY MSANGAWINA | SAIDI ALLY MSANGAWINA | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI Na.TMK030175, ARDHI Na.TMK/MBGL/KBG19/288 | MBAGALA, KIBURUGWA, WILAYA YA TEMEKE, DAR ES SALAAM | 03-12-2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | AMA'Z AUCTION MART & GENERAL BROKES LIMITED |
| 3 | DANIEL .J. MAGIGE | DANIEL JOSEPH MAGIGE | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | MZINGA, KITUNDA, WILAYA YA ILALA, DAR ES SALAAM | 26/11/2022 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | STEAM GENERATION RECOVERIES LTD |
| 4 | MARIAM DALUWESHI IDDI | MARIAM DALUWESHI IDDI | GARI Na.T 723 DQD TOYOTA IST. | MBEZI BEACH, WILAYA YAKINONDONI, DAR ES SALAAM | 25/11/2022 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | STEAM GENERATION RECOVERIES LTD |
| 5 | CAPEVIEW COMPANY LIMITED | MUSSA SIMBA KALIMANZILA | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI Na.TMK042322, ARDHI Na.TMK/MBGK/KJC7/129, | MTONI KIJICHI, MBAGALA KUU WILAYA YA TEMEKE, DAR ES SALAAM | 23/11/2022 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | STEAM GENERATION RECOVERIES LTD |
| 6 | TITUS D NYIKA | PETER DANIEL NYIKA | NYUMBA YENYE LESENI MAKAZI Na.TMK011077, ARDHI Na.TMK/MBGL/KGG34/217 | KINGUGI, MBAGALA WILAYA YA TEMEKE, DAR ES SALAAM | 24/11/2022 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | STEAM GENERATION RECOVERIES LTD |
| 7 | DOTO PETER MADUKWA | LEYLA KHALIDY AHMED SHEBE | NYUMBA YENYE HATI Na. C.T.NO.161600, KIWANJA NA. 209, KITALU "A" | MBANDE, WILAYA YA TEMEKE, DAR ES SALAAM | 29/11/2022 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | STEAM GENERATION RECOVERIES LTD |
| 8 | CHARLES YUSUPH PUKA | GASPAR WILLIAM MWAKANYAMALE | NYUMBA YENYE HATI Na. C.T.NO.90710, KIWANJA NA. 635, KITALU "N", | PUGU, MWAKANGA, WILAYA YA ILALA, DAR ES SALAAM | 25/11/2022 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | STEAM GENERATION RECOVERIES LTD |
| 9 | ENEA G. BASAYA | GODFREY DAUDI BASAYA | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI Na.TMK035990, ARDHI Na.TMK/MBGL/KNY28/81 | KWA NYOKA, MBAGALA WILAYA YA TEMEKE, DAR ES SALAAM | 30/11/2022 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | STEAM GENERATION RECOVERIES LTD |
| 10 | MEGA ATTORNEYS | PAULO KARLO KALOMO | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI Na.KND007753, ARDHI Na.KND/MBB/MBO18/80 | MABIBO, MABIBO, WILAYA YA KINONDONI, DAR ES SALAAM | 24/11/2022 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | MBUZAX AUCTION MART AND COMPANY LIMITED |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi wa dhamana unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Mali/dhamana itauzwa katika hali ilivyo na mahali ilipo.
3. Mshindii wa mnada atalazimika kulipa malipo yasiyopungua 25% ya bei iliyofikiwa siku yamnada, na 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne (14) toka tarehe ya mnada.
4. Gharama zozote ikiwemo kubadilisha hati miliki (transfer of ownership), na kumtoa mtu kwenye nyumba/eneo lililouzwa na bank (eviction) ni za mnunuzi.
5. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti moja wapo hapo juu malipo ya awali hayatarejeshwa na mnada utarudiwa.

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na:**

| | | | |
|---|---|---|---|
| **AMA'Z AUCTION MART & GENERAL BROKES LIMITED**<br>P. O. Box 62163<br>Dar es Salaam<br>Tel: 0658100737, 0757276263<br>Email: amazauctionma@gmail.com | **STEAM GENERATION RECOVERIES LTD**<br>P. O. Box 80607<br>Dar es Salaam<br>Tel: : +255 715 91 74 51<br>Email: steam@steamtz.com | **MBUZAX AUCTION MART AND COMPANY LIMITED** P.O. Box 15694,<br>Dar Es Salaam,<br>Tel: : +255 714 200025, 0755 506 970<br>Email: mbuzaxauctionmarttz@gmail.com | **MANAGING DIRECTOR MWANGA HAKIKA BANK LIMITED**<br>P.O.BOX 11735<br>Dar es Salaam<br>Tel: 0747666511 |

117136702

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Wavuvi wastahili pongezi uokozi ajali ya ndege*

**MASHUJAA**, ndio sifa wanayostahili kupewa wavuvi waliofanya kazi kubwa ya kuwaokoa abiria waliokuwa kwenye ndege ya Precision Air, iliyoangukia ziwani baada ya hali ya hewa kuwa mbaya wakati ikitaka kutua katika Uwanja wa Ndege wa Bukoba mkoani Kagera.

Licha ya kutokuwa na vifaa vya uokozi, lakini kwa uzoefu wao wa kufanya shughuli zao kwenye maji, waliweza kuwaokoa watu wengi wasiendelee kupoteza maisha kwenye ajali hiyo.

Ajali hiyo iliua watu 19 na waliokolewa walikuwa 26 huku idadi ya abiria waliokuwa kwenye ndege hiyo ikielezwa kuwa ni 43.

Kuokoa watu 26 waliokuwa ndani ya ndege iliyozama kwenye maji si jambo la mchezo hasa ikizingatiwa kuwa waliofanya kazi hiyo walikuwa wavuvi waliokuwa wakiendelea na shughuli zao za uvuvi.

Mpaka vikosi vya jeshi ambavyo vinahusika na kazi hiyo ya uokozi vilipofika eneo la tukio, tayari wavuvi hao walikuwa wameshafanya kazi kubwa, vinginevyo watu zaidi wangeendelea kupoteza maisha.

Kiukweli wavuvi hao wanastahili pongezi kubwa kwa kuokoa idadi hiyo kubwa na kama wangekuwa na uwezo zaidi wa vifaa bila shaka, wangeweza kuokoa idadi kubwa zaidi na pengine kusingekuwa na vifo.

Kadhalika, juhudi zilizofanywa na wavuvi kujaribu kuivuta ndege hiyo kutoka kwenye maji kwa kutumia kamba za kawaida tu, kunaonesha jinsi walivyokuwa na moyo wa kizalendo wa kuokoa roho za wenzao.

Kwa Watanzania ni pigo kubwa kupoteza idadi hiyo kubwa ya watu wakiwamo marubani, ambao licha ya kuwa kwenye hatari ya kupoteza maisha, walielekeza abiria jinsi ya kujiokoa.

Inasikitisha na kuhuzunisha kupoteza nguvu kazi kubwa ya taifa, kwa sababu wengine walikuwa wakisafiri kikazi kwenda kuwahudumia Watanzania wenzao na wengine waliokuwa wanakwenda kusalimia familia zao, lakini safari yao ilikatishwa na ajali hiyo.

Mara nyingi zinapotokea ajali kama hizo kuna la kujifunza. Ajali hiyo inafundisha umuhimu wa watu kujifunza masuala ya uokoaji kwa sababu ni jambo la ghafla na linatokea mahali popote.

Ajali inaweza kutokea baharini, angani, barabarani kwenye reli hivyo ni muhimu kuwapo kwa elimu ya uokozi hasa kwa watu wanaofanya shughuli kwenye maeneo hayo.

Kwenye ajali ya juzi umuhimu wa watu kujifunza kuogelea, kuzamia na vile vile maelekezo yanayotolewa kwenye vyombo vya usafiri kabla ya safari kuzingatiwa.

Unapokuwa kwenye usafiri wa ndege, kabla ya kuanza safari, abiria huelekezwa jinsi ya kujiokoa kama itatokea dhoruba ya aina yoyote.

Lakini, wengi wetu hatutilii maanani na kuona kama wanaoelekeza wanatoa kiburudisho kwa abiria.

Hata kwenye usafiri wa majini, maelekezo hayo hutolewa, lakini baadhi ya abiria badala ya kufuatilia wanakuwa wanafanya mambo yao.

Kwenye baadhi ya mabasi wahudumu huwasisitiza sana abiria kufunga mikanda, lakini hilo baadhi yao hawalizingatii na matokeo yake inapotokea ajali, athari yake huwa kubwa kuliko kama angejifunga mkanda.

Katika ajali hiyo ya ndege, shukrani na pongezi nyingi ziende kwa wavuvi kwa ushujaa mkubwa walioonesha katika kuokoa maisha ya watu. Mungu aendelee kuwabariki katika kazi zenu na atawalipa kwa mlichokifanya.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253 676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.ippmedia.com






Na Golden Kisapile, TUDARCO

## Muungwana Lazima Nilonge

# *Nishati safi ina manufaa 'milioni'*

**WIZARA** ya Nishati 'imeupiga mwingi' kwa kuja na suluhisho kuhusu nishati safi ya kupikia ambayo upatikanaji wake utaleta suluhu kwenye mambo mbalimbali kuanzia kupunguza maradhi hadi kupatikana afya kwa kinamama.

Serikali imetangaza kuja na mpango wa nishati salama jikoni, ambayo si tu kwamba umewaponya kinamama na wasichana mizigo ya kuhangaika bali pia utawanusuru na ukatili wa kijinsia.

Wanawake na watoto hasa mabinti wengi wamekuwa wakifanyiwa ukatili wa kijinsia kama vile ubakaji, ulawiti na kupigwa bila sababu wakati wa kutafuta nishati hasa kuni, mkaa, makumbi na makuti ya nazi, kuokota vipande vya mbao kwenye nyumba zilizoezekwa mijini na vijijini.

Ni wazi kuwa ujio wa nishati salama jikoni unaelekea kuwa mwarobaini wa kupunguza msongo wa mawazo kwa wale waliokutwa na matatizo mbalimbali yanayotishiwa na ukosefu wa kuni.

Ukosefu huo waweza kuwa ni kwenye biashara, mgahawa, nyumbani na popote ambako nishati hiyo inahitajika, yote hayo yametishia afya ya akili.

Nishati chafu ni kiini cha magonjwa mbali mbali kwa vile moshi wa kuni unatajwa kuwa hauna tofauti na kutumia tumbaku inaleta saratani, vichomi, moyo, mapafu na saratani na macho.

Aidha, kama nishati safi ya kupikia itapatikana itawapa wanawake na watoto tumaini jipya la kuwa na afya njema ya akili na mwili hasa kwa kinamama ambao shida ya kuni imewaathiri.

Nishati safi jikoni ni kupatikana kwa fursa mbalimbali, kwa wanawake na watoto wakike na wakiume, ambapo watu hawa hupoteza muda wao kutafuta nishati zisizo safi, lakini nishati safi ikitumika watu hawa watapata fursa zakufanya mambo yao mengine kama vile fursa ya kupata elimu, kufanya biashara na kilimo.

Linaweza kuwa suala la kuongeza tija kwa wanawake na taifa kwani litaongeza idadi ya wasomi nchini ni baada ya watoto wakike wengi kupata elimu kwa ngazi mbalimbali.

**Kinamama watapata muda wa kujihusisha na shughuli mbalimbali za kiuchumi mfano kutengeneza vyakula mbalimbali, kushona, kulima bustani, kuuza na kusambaza bidhaa na kujiongezea kipato.**

Ni hakikisho la afya njema na kuondokana na magonjwa mbalimbali na hili litaongeza nguvu kazi ya taifa kwa sababu watu watakuwa na afya njema badala ya kusotea kuni vichakani au kwenye nyumba zinazoezekwa mijini.

Kinamama watapata muda wa kujihusisha na shughuli mbalimbali za kiuchumi mfano kutengeneza vyakula mbalimbali, kushona, kulima bustani, kuuza na kusambaza bidhaa na kujiongezea kipato.

Nishati salama itapunguza athari za mabadiliko ya tabianchi na uharibifu wa mazingira kwa sababu matumizi ya nishati chafu yaliyachafua.

Yote haya yatapunguza ukame, mafuriko na kuongezeka kwa hewa ya ukaa nchini kwa hiyo nishati safi ya kupikia ikitumika itaweka mzingira safi na salama kuanzia jikoni hadi angani, lakini ni muhimu kwa taifa na kwa dunia nzima sasa wakati kila taifa linakabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Ni pongeza kuwa ujio wake utapunguza vifo katika jamii, watu 30 hufariki kila mara kwa sababu ya magonjwa yanayoathiri mfumo wa upumuaji.

Miti itastawi na kufanikisha juhudi za utunzaji wa mazingira, kwa sababu nishati chafu ilichoma misitu, kukata miti, vichaka na mapori lakini miti itapata ahuweni.

Pamoja na hayo italeta maji kwa vile vyanzo vitatunzwa kwa kutumia nishati safi ya kupikia hivyo mito, maziwa, chemichemi kuwa safi na salama. Nishati safi italeta mabadiliko ya teknolojia, kwa sababu watajitokeza wawawekezaji watewekezaji kwenye nishati safi na salama ya kupikia katika uzalishaji Watanzania watapata ajira na wengine kujiajiri.

Hivyo nishati safi ya kupikia ni ukombozi kwa wananchi kwa sababu Tanzania itaondokana na matatizo mbalimbali kama vile ukatili wa kijinsia, ukame, maradhi na kuchochea uharibifu wa mazingira.



Diwani wa Kata ya Kivukoni Dar es Salaam, Sharik Choughule (wa pili kulia), akiwa na Injinia wa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) Wilaya ya Ilala, Regnald Mashamba, wakiangalia uwekaji wa lami kipande cha barabara ya Sea View jijini humo, mwishoni mwa wiki. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mbunge kuhojiwa mahakamani leo kesi ya CHADEMA

**Na Grace Gurisha**

MBUNGE wa Viti Maalum kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Cecilia Pareso, leo anatarajiwa kuhojiwa na jopo la mawakili wa chama hicho kuhusiana na kiapo chake alichokiwasilisha katika kesi ya kupinga kuvuliwa uanachama bila kupewa haki ya kusikilizwa.

Pareso atahojiwa mbele ya Jaji Cyprian Mkeha wa Mahakama Kuu Masjala Kuu Dar es Salaam na jopo hilo ambalo linaongozwa na Wakili Peter Kibatala, baada ya Mbunge wa Viti Maalum, Nursat Hanje kumaliza kuhojiwa, akidai walifanyiwa alichokiita umafia na chama hicho.

Nusrat pia alidai kwamba, akiwa mjumbe wa Sekretarieti ya CHADEMA, anajua mambo mengi ambayo yanafanywa na chama chake na kuna kipindi Msajili wa Vyama vya Siasa alikuwa akitaka taarifa, walikuwa wanazitengeneza na kuzipeleka.

Mbunge huyo alidai fomu ya uchaguzi ambayo aliijaza kwa ajili ya kupelekwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kwamba ameteuliwa katika nafasi hiyo na kwamba Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika ndiye alimpelekea mahabusu aijaze na kisha akaondoka nayo.

"Mambo mengine tukiyazungumza hapa tutakuwa tunakiabisha chama, ndiyo maana ninataka twende tukayamilize huko, maana kuna mambo ya kuvuana nguo hapa," alidai.

Nusrat alidai alifikia hatua hiyo baada ya kudai kuwa kuna mambo ambayo hayajui yapo kwenye muhtasari wa kikao cha Baraza la Kuu la CHADEMA, hajui yametoka wapi kwa sababu siku hiyo alikuwapo.

Pia alidai kwamba kwa siku 113 alizokuwa mahabusu Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe na Katibu Mkuu wa chama hicho, John Mnyika walikuwa wakimtembelea na kumwahidi kuwa nafasi alizoziomba atazipata na pia wanaendelea kumpambania.

Mdee na wenzake 18 walifungua kesi hiyo Julai 21, mwaka huu, mahakamani huko dhidi ya CHADEMA, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Tume ya Taifa ya Uchaguzi, wakipinga uamuzi wa Baraza Kuu la chama hicho kuwavua uanachama Mei 11 mwaka huu.

Katika shauri hilo namba 36 la mwaka 2022, wabunge hao pamoja na mambo mengine, wanaiomba mahakama hiyo ipitie mchakato na uamuzi huo wa CHADEMA kuwafukuza, kisha itoe amri tatu.

Wabunge hao wanaomba mahakama itengue mchakato na uamuzi wa kuwavua uanachama, iwalazimishe CHADEMA kuwapa haki ya kuwasikiliza na amri ya zuio dhidi ya Spika na Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuchukua hatua yoyote mpaka malalamiko yao yatakapotolewa uamuzi.


## NOTISI/TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD, NGOMENI AUCTION MART, REAL MASTER LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,YONO AUCTION MART &CO.LTD ,YARDLEY RECOVERIES AUCTION LTD,** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muunganowa Tanzania, chini ya benki ya AKIBA COMMERCIAL BANK PLC, tunatoa notisi ya kulipa madeni kwa wadaiwa wafuatao ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| UBUNGO | FELIX BIRCKMAS ALOYS | NYUMBA (2) | 1.KASSIAN ANTHON NINDI 2.BOSCO ULIRICK TARIMO | 1.TABATA KISUKULU 2.MANZESE | 22/11/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| TEGETA | MAULID SELEMANI KABATA | NYUMBA | MAULID SELEMANI KABATA | MAPINGA | 23/11/2022 SAA 5:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| TEMEKE | HOSEA MARCO OOKO | NYUMBA | KIBADENI J. NYATIENO | CHANIKA-ILALA | 24/11/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| TEMEKE | DAUDI JAKAMUGAH MAKOSIGAH | NYUMBA | KIBADENI J. NYATIENO | CHANIKA-ILALA | 24/11/2022 SAA 5:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| TEGETA | YUSUPH JULIAS MWAKIPESILE | NYUMBA | ERASTO KAMANI | BANGULO -PUGU | 25/11/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| UKONGA | LEONARD BAKUZA KABYILO | NYUMBA | LEONARD BAKUZA KABYILO | VIWEGE-MAJOHE, ILALA | 22/11/2022 SAA 5:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| UKONGA | JULIUS RYOBA DANIEL | NYUMBA | JULIUS RYOBA DANIEL | KITUNDA- MZINGA, ILALA | 22/11/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| UKONGA | ELIZABETH PHILIPO CHIWILI | NYUMBA | ELIZABETH PHILIPO CHIWILI | KITUNDA KATI, KITUNDA, ILALA | 22/11/2022 SAA 5:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| UKONGA | REHEMA NASIBU RAJABU | NYUMBA | REHEMA NASIBU RAJABU | KILIMA HEWA- KIBAHA, PWANI | 23/11/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| UKONGA | SALUM OMARY MTENGWA | NYUMBA | RAMADHANI NASSORO BOMBWE | MNYAMANI- BUGURUNI, ILALA | 24/11/2022 SAA 5:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| AGGREY | BENJAMIN JOACHIM MUSHI | NYUMBA | JOHN MROSHI MUSHI | KITUNDA ILALA | 22/11/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| AGGREY | GADNER HATWABY DIBIBI | NYUMBA | ZUWEJA SELEMANI KAZEMBE | CHARAMBE-NZASA "A" | 22/11/2022 SAA 5:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| AGGREY | KHAMIS HAJI FAKI | NYUMBA | KHAMIS HAJI FAKHI | CHANIKA-ILALA | 23/11/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| KIJITONYAMA | CHRISTOPHER ANDREW KADINDA | NYUMBA | CHRISTOPHER ANDREW KADINDA | BUNJU | 22/11/2022 SAA 5:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| KIJITONYAMA | NEEMA ELISANTE MANASE | NYUMBA | NEEMA ELISANTE MANASE | MTONGANI | 23/11/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| BUGURUNI | TAMIKA IZACK MWALUMU | NYUMBA | TAMIKA IZACK MWALUMU | KINYEREZI KIBAGA | 24/11/2022 SAA 5:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| BUGURUNI | PADONI KIBAYU SIMONI | NYUMBA | PADONI KIBAYU SIMONI | MAJOHE VIWEGE | 22/11/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| BUGURUNI | VIP PRODUCTION & SUPPLY | NYUMBA | HASSANI HASSANI MUMBI | MAJOHE RADA | 22/11/2022 SAA 5:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| BUGURUNI | MTUMWA SALUM HAMAD | NYUMBA | MATONGO NKWABI NSAGA | PUGU KAJIUNGENI | 23/11/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| MWANZA | ELSON YALEDI ENOSI | NYUMBA | ELSON YALEDI ENOSI | BUHONGWA-MWANZA | 23/11/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| MWANZA | NOZAWA G DAVID,MR. T/A BUSWELU SATELITE CABLE NETWORK | NYUMBA | KATONGOLE DASTAN | NORTH BUSWELU-MWANZA | 24/11/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| ARUSHA | FATUMA HASSAN LAIZER | NYUMBA | FATUMA HASSAN LAIZER | MLIMANI -SINONI ARUSHA | 23/11/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| ARUSHA | JONATHAN JOSIAH RUKUNTUKA | NYUMBA | JONATHAN JOSIAH RUKUNTUKA | KARATU | 24/11/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja, Gari au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie **simu no.0714939933/0692836202/0765999000/0674004524/0655715138/0754376493**
4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi benki bila gharama yeyote.

217136502

# ‘Vikao kujadili changamoto za Muungano vitaendelea kuwapo’

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SERIKALI imesema vikao vya kupokea na kujadili changamoto za Muungano vipo na vitaendelea kuwapo kutokana na umuhimu wake katika mustakabali wa Muungano.

Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Khamis Hamza Khamis, alitoa kauli hiyo jana bungeni jijini hapo alipojibu maswali ya wabunge.

Mbunge wa Mwera, Zahor Mohammed Haji alitaka kufahamu kama vikao vya kupokea na kujadili changamoto za Muungano kama vipo.

Katika majibu ya msingi, Khamis alisema vikao hivyo hufanyika kwa mujibu wa Mwongozo wa Utaratibu wa Vikao vya Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano (SJMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) ya kushughulikia Masuala ya Muungano ambao umeridhiwa na pande zote mbili za Muungano.

Alisema kuwa katika mwongozo huo, kikao cha Kamati ya Pamoja hufanyika mara moja kwa mwaka, kikao cha mawaziri hufanyika mara moja kwa mwaka, kikao cha makatibu wakuu hufanyika mara mbili kwa mwaka na kikao cha Sekretarieti ya Kamati ya Pamoja hufanyika mara nne kwa mwaka.

Khamis aliongeza kuwa kwa mwaka 2021/22 vikao hivyo vilifanyika kwa mujibu wa mwongozo huo ambapo kikao cha Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ ya kushughulikia Masuala ya Muungano kilifanyika Agosti 24, 2021.

Akiendelea kujibu swali hilo, Naibu Waziri Khamis alifafanua kuwa katika kikao hicho, hoja 11 kati ya 18 zilipatiwa ufumbuzi na kuondolewa kwenye orodha ya hoja za Muungano.

Alisema tayari hoja mbalimbali zimeshapatiwa ufumbuzi zikiwamo uvuvi wa Bahari Kuu, mgawanyo wa mapato, mapato yanayotokana na Jeshi la Uhamiaji kwa upande wa Zanzibar na ucheleweshaji wa miradi ya maendeleo.

“Katika hili kwa mfano, kutiwa saini kwa mikataba ya miradi ya maendeleo kule Zanzibar, hili limeshapatiwa ufumbuzi. Kutiwa saini kwa mkataba wa ujenzi wa Hospitali ya Biguni, ukarabati wa Hospitali ya Mnazi Mmoja, ujenzi wa Barabara Chake Macho Manne tayari, yote haya yameshapatiwa ufumbuzi,” alisema.



Kaimu Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai wa Polisi Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Teodori Njawa (kulia), akiwaelimisha wananchi wa Kijiji cha Mgome wilayani hapo kuhusu wajibu wa kuanzisha ulinzi shirikishi katika vijiji ili kupambana na wahalifu. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## Usiri wa harusi kikwazo kukabili ndoa za utotoni

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

OFISA Ustawi wa Jamii Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha mkoani Pwani, Yahaya Mbogolume, amesema kuna vikwazo katika kupata takwimu sahihi za ndoa za utotoni kutokana na ndoa hizo kufungwa kwa siri.

Mbogolume aliyasema hayo juzi alipozungumza na Nipashe ofisini kwake, akibainisha kuwa ndoa za utotoni katika kata za halmashauri hiyo zinafanyika kwa makabila ya wafugaji ambayo wanaozeshana wenyewe kwa wenyewe.

Alibainisha kuwa baada ya kufungwa kwa ndoa hizo, wanandoa wanakwenda kuishi mbali na eneo lilikofanyika tukio, jambo linalofanya hata kitengo kupata taarifa kwa kuchelewa na hivyo kuchelewa pia kuchukua hatua ya kuwakamata wahusika.

“Ndoa nyingi za utotoni zikishafungwa wanakwenda mbali, tunapata taarifa zao kwa kuchelewa, hata tunapokwenda kufuatilia ili tuchukue hatua tunakuwa tumeshachelewa na hivyo wahusika kutochukuliwa hatua za kisheria,” alisema.

Kwa mujibu wa Mbogolume, ndoa nyingi kwa makabila hayo ya wafugaji zinafanyika kwa ajili ya mali, akifafanua kuwa familia ikiwa na mtoto wa kike inakuwa ni mali na umri waliojiwekea ukifika wanawaozesha kwa kupewa mahari ya mifugo.

Alibainisha vikwazo vinavyozikumba ndoa hizo kuwa ni pamoja na kuvunjika muda mfupi baada ya kufungwa kutokana na kutokuaminiana kwenye uhusiano, kipato kidogo pamoja na familia za wanandoa kuwaingilia na kuwa waamuzi.

Alisema kuwa kutokana na hali hiyo, kitengo hicho kimeanza mikakati yake kukabiliana na ndoa za utotoni kwa kushirikisha kamati za ulinzi na usalama na kutoa elimu kwenye mikutano kuhusiana na madhara ya ndoa hizo.

# TAWIRI yatoa mafunzo kukabili wanyama wakali

**Na Thobias Mwanakatwe,** ITIGI

TAASISI ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI) chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii imetoa mafunzo kwa wananchi wa kata tano za Halmashauri ya Itigi wilayani Manyoni mkoani Singida namna ya kutumia njia rafiki za kudhibiti wanyamapori waharibifu, wakiwamo tembo.

Wataalamu kutoka TAWIRI walitoa mafunzo hayo mwishoni mwa wiki kwa wananchi wa kata za Mwamagembe, Sanjaranda, Itigi, Majengo na Kitaraka ambazo mara kwa mara tembo wamekuwa wakivamia mashamba yao na kufanya uharibifu wa mazao.

Timu hiyo ya wataalamu ikiongozwa na Dk. Janemary Ntalwila, iliwafundisha wananchi baadhi ya mbinu za kuwadhibiti tembo ikiwa ni pamoja na kutumia vitisho vya mwanga, sauti (vuvuzela au honi kali), mabomu ya pilipili, matumizi ya fataki, uzio wa vitambaa vyenye mafuta (oil) na pilipili, tofali la pilipili na matumizi ya fensi ya mizinga ya nyuki.

Wananchi pia wamefundishwa njia mbadala ya upandaji wa mazao kinga katika maeneo yanayoathirika na tembo kuwa ni njia nzuri ya kupunguza migongano na wanyamapori.

Baadhi ya mazao hayo ni pamoja na tumbaku, pilipili, ufuta na tangawizi ambayo yanaweza kupandwa kuzunguka shamba au kama mazao mbadala.

Dk. Ntwalwila alisema njia hizo zimethibitika katika maeneo mengi kuwa na matokeo chanya ya kupunguza uvamizi na uharibifu wa mazao na madhara mengine yanayotokana na uvamizi wa wanyamapori hao waharibifu.

Wananchi hao pia wamepatiwa elimu ya baadhi ya vyanzo vya migongano baina ya wanyamapori na binadamu ikiwa ni pamoja na ongezeko la watu jirani na maeneo ya hifadhi, mabadiliko ya tabianchi, kufungwa kwa mapito ya wanyamapori, mabadiliko ya tabia ya wanyamapori na kutokuwapo mipango ya matumizi bora ya ardhi.

Mwezi Septemba mwaka huu, madiwani wa Halmashauri ya Itigi waliitaka Idara ya Mazingira na Maliasili ichukue hatua za haraka kudhibiti tembo ambao wamekuwa wakiua na kujeruhi watu katika matukio yanayojitokeza mara kwa mara katika halmashauri hiyo.

Madiwani hao walitoa tamko wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Itigi kufuatia kutolewa taarifa za tembo kuua wanawake wawili na kujeruhi mmoja, tukio lililotokea Kata ya Mgandu.

Diwani wa Mgandu, Martin Kapona alisema wanawake hao waliuawa kwa kukanyangwa na tembo na kufa papo hapo wakati wakiwa shambani na kwamba aliyejeruhiwa alilazwa katika Hospitali ya Mtakatifu Gaspar iliyoko Itigi.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Itigi, Hussein Simba alisema maeneo mengi ya Itigi yameathirika kutokaka na tembo ambao wanavamia wananchi na kuharibu mazao mashambani.

Simba alisema tatizo lililopo ni kwamba Idara ya Mazingira na Maliasili ina mtumishi mmoja, hivyo inakuwa vigumu kufika kila kijiji kuangalia namna ya kutatua matatizo ya wanyamapori hao vijijini.

## HABARI KITAIFA

# Halmashauri yabanwa kulipa mawakala ukusanyaji mapato

**Na Thobias Mwanakatwe,** ITIGI

MADIWANI wa Halmashauri ya Itigi wilayani Manyoni mkoani Singida wameuagiza uongozi wa halmashauri hiyo kuwalipa mawakala wanaokusanya mapato katika halmashauri zaidi ya Sh. milioni 27 ili kuondoa vishawishi vya kutumia fedha wanazozikusanya.

Wakizumgumza jana katika kikao cha Baraza la Madiwani, viongozi hao walisema kitendo cha kutowalipa mawakala hao kwa zaidi ya miezi miwili sasa, kinawakatisha tamaa kuendelea kukusanya mapato na hivyo kuisababisha halmashauri upotevu wa mapato.

"Haiwezekani mkusanya ushuru akusanye Sh. milioni 100 halafu unashindwa kumlipa haki yake, hapa halmashauri tunakuwa tunajiweka kitanzi," alisema Mwenyekiti wa Halmashauri ya Itigi, Hussein Simba.

Kiongozi huyo pia aliwaagiza madiwani washirikiane katika kuwasimamia wakusanya ushuru ili wanapokusanya fedha wawe wanazipeleka benki badala ya kukaa nazo, hali inayosababisha kuwa na malimbikizo mengi.

Diwani wa Itigi Mjini, Ally Minja, alibainisha mawakala wana miezi miwili hawajalipwa na kuutaka uongozi wa halmashauri utoe ufafanuzi ni lini watalipwa fedha zao.

Minja alisema kitendo cha kutowalipa fedha mawakala hakileti afya kwa halmashauri, akionya kuwa hali hiyo ikiendelea itakuwa inasababisha halmashauri kushindwa kufikia malengo yake ya mwaka ya ukusanyaji.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Itigi, John Mgalula, akijibu malalamiko hayo ya madiwani, alisema suala la kuwalipa mawakala hao lilipitishwa na sasa lipo katika Ofisi ya Mweka Hazina wa Halmashauri (DT).

"Waheshimiwa madiwani, suala hili linashughulikiwa na hadi kufikia juzi wakusanya ushuru walikuwa wanaidai halmashauri Sh. milioni 27 na kuanzia wiki ijayo watalipwa fedha zao," alisema.Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Manyoni, Jumanne Makhanda, aliwataka madiwani kushirikiana na watendaji ili kuiletea maendeleo halmashauri hiyo kwa kuwa wananchi wanawategemea.

Alisema chama hicho kitaanza kufanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo ambayo serikali imetoa mamilioni ya shilingi ili kuangalia kama ilani imetekelezwa vyema.



Aliyekuwa Mkurugenzi wa Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), Madeni Kipande (kushoto), akiwa na wenzake katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu Dar es Salaam jana, wakisubiri kusikiliza kesi inayowakabili ya kuisababishia hasara mamlaka hiyo ya Sh. bilioni 4.2. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Madaktari bingwa UK watoa huduma Bombo

**Na Boniface Gideon,** TANGA

HOSPITALI ya Rufani ya Mkoa wa Tanga (Bombo) imezindua mpango wa matibabu ya kibingwa ukilenga kutoa huduma kwa wagonjwa 360 bila malipo ikishirikiana na madaktari bingwa wa Taasisi ya Pelecks ya Uingereza.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa huduma hiyo mwishoni mwa wiki, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu alisema Tanzania inakabiliwa na shida ya uhaba wa madaktari bingwa, akibainisha kuwa uhitaji kwa nchi nzima ni madaktari 1,782 huku waliowapo kwa sasa ni 992.

Waziri Ummy aliishukuru taasisi hiyo kwa kujitolea kutoa huduma hiyo bila malipo ambapo wagonjwa wenye shida mbalimbali za kiafya watapata huduma yakiwamo magonjwa ya moyo na upasuaji wa mishipa ya fahamu huku akiwaomba baada ya kumaliza kutoa huduma Mkoa wa Tanga, kuangalia uwezekano wa kufika katika mikoa mingine ya Tanzania kutoa matibabu hayo.

"Tuna uhaba mkubwa sana wa madaktari bingwa nchini. Tunatakiwa tuwe na madaktari bingwa 1,782 lakini walioko ni 992 tu. Kwa hiyo, utaona uhaba wa madaktari bingwa nchini ni asilimia 50 na Watanzania wanahitaji huduma hizi za matibabu ya kibingwa ikiwamo upasuaji wa magonjwa ya moyo, mishipa ya fahamu na masuala mengine.

"Kwa hiyo, tunapopata wadau wa kuja kutusaidia kama Pelecks, tunawashukuru sana na huduma hii isiishie Tanga tu nendeni na mikoa mingine ili tuweze kuwafikia wagonjwa wengi zaidi," alisema Ummy.

Mganga Mkuu Mkoa wa Tanga, Jonathan Budenu, alisema kutolewa kwa matibabu ya kibingwa kupitia ushirikiano wao huo, kutasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza au kuondokana na matatizo ya wagonjwa ambao wamekuwa wakihitaji huduma za kibingwa huku akikiri kuwa na uhaba wa vitanda vitakavyotumika katika kuwahudumia wagonjwa watakaokuwa wakipatiwa huduma hiyo.

Huduma hiyo itagharimu Sh. milioni 876 ikitolewa ndani ya siku saba ndani ya Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Tanga (Bombo).

## Bilioni 2/- kujenga daraja

**Na Ibrahim Yassin,** MOMBA

SERIKALI imeanza ujenzi wa daraja litakalogharimu Sh. bilioni 2.039 ili kuwaunganisha kwa mawasiliano ya barabara wananchi wa kata za pembezoni kwenda makao makuu ya Wilaya ya Momba mkoani Songwe yaliyoko Chitete.

Imebainisha kuwa asilimia 80 ya wakazi wa Wilaya ya Momba wanaendesha maisha yao wakitegemea kilimo cha mazao mbalimbali, ufugaji na uvuvi huku mazao yao wakiyasafirisha kupitia njia za mzunguko wakitumia fedha nyingi kutokana na ukosefu wa daraja linalowaunganisha ambalo kwa sasa limeanza kujengwa.

Akizungumza na Nipashe mwishoni mwa wiki, Ezekiel Mwashilindi, mkazi wa Momba, alisema kuwa tangu nchi ipate uhuru wamekuwa wakitumia njia za mzunguko kufuata huduma mbalimbali makao makuu ya wilaya kutokana na ukosefu wa daraja katika barabara hiyo iendayo makao makuu.

Sophia Nakandonga, mkazi wa Chitete, alisema kukamilika kwa daraja hilo kutafungua fursa za kiuchumi kwa wananchi wa vijiji vilivyoko pembezoni mwa wilaya hiyo ambao awali walitumia njia za pembezoni kusafirisha mazao yao na mifugo kupeleka mkoani Mbeya, akisisitiza kuwa wana kila sababu ya kuipongeza serikali.

Magreth Sinyangwa, mkazi wa Samang'ombe alisema kipindi cha mvua, maji huwa yanajaa katika eneo hilo na kufunga mawasiliano ya barabara hiyo, hivyo kujengwa kwa mradi huo kumewafanya watembee kifua mbele wakijivunia unakwenda kuongeza fursa za kiuchumi na hata kuwa na uhakika wa kusafirisha mazao yao.

Kwa mujibu wa mkandarasi anayetekeleza mradi huo kutoka Kampuni ya Kagwa Contruction ya jijini Dar es Salaam, Godfrey Mwampulo, utachukua siku 240 kukamilika, akibainisha kuwa tayari wamenunua mahitaji yote na watajenga usiku na mchana kuhakikisha unakamilika kwa wakati.

Meneja wa Wakala wa Barabara (TANROADS) mkoani Mbeya, Suleiman Bishanga, alisema wamepokea Sh. bilioni 2.039 kutoka serikali kuu kujenga mradi huo utakaokuwa mkombozi kwa wananchi.

Alisema TANROADS ikiwa wasimamizi wa mradi huo, itahakikisha unatekelezwa kwa ufanisi na kukamilika kwa wakati.

Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Waziri Kindamba, alisema serikali imesikia kilio cha wananchi kwa kutoa kiasi hicho cha fedha, akiwataka makandarasi waliopewa tenda hiyo kuhakikisha wanakamilisha ujenzi kwa wakati na kwa viwango na kuwataka wafunge taa ili wajenge mchana na usiku.

## MASWALI NA MAJIBU BUNGENI

# Serikali yaanika mikakati kuongeza bei ya korosho

NAIBU Waziri wa Kilimo amesema serikali itawawezesha wabanguaji wadogo wa korosho ghafi ili kukabiliana na kuporomoka kwa bei ya korosho nchini.

Anthony Mavunde alitoa kauli hiyo bungeni jana alipojibu maswali ya nyongeza ya Mbunge wa Nanyamba (CCM), Abdallah Chikota.

Mbunge huyo alisema kwa miaka miwili mfululizo serikali imekuwa ikiahidi viuatilifu lakini kiasi kinachotolewa na usambazaji hakiendani na kilichoahidiwa na kusababisha upungufu wa pembejeo kwa wakulima.

"Serikali inatoa kauli gani kuhusu pembejeo za unga na dawa za maji kupatikana kwa wakati na kufika kwa wakulima?" Alihoji.

Vilevile, Chikota alisema ongezeko la pembejeo litachangia uzalishaji kuongezeka ambapo kwa sasa kwenye minada ya korosho bei inaendelea kuporomoka.

"Je, serikali ina mkakati gani, ongezeko hili la uzalishaji litaendana na bei yenye tija kwa mkulima wa korosho?" Alihoji.

Akijibu maswali hayo, Mavunde alisema miongoni mwa mikakati waliyonayo ni kuhakikisha wabanguaji wadogo wanawezeshwa ili kuongeza ubanguaji wa korosho ghafi na kutengeneza masoko ya uhakika ya korosho ambayo imechakatwa.

Alisema hivi sasa wanaendelea kutafuta masoko nje ya nchi na wiki iliyopita alikwenda uwanja wa ndege kusindikiza kontena la korosho zilizobanguliwa ambapo soko limepatikana Marekani na kilo moja inauzwa Sh. 90,000.

"Hivyo, mkakati wa serikali ni kuwawezesha wabanguaji wadogo ili tuachane na soko la Vietnam na India ambako kumekuwa na changamoto kubwa ya bei," alisema.

Naibu Waziri huyo pia alisema kwenye kikao cha wadau wa korosho, wamekubaliana viuatilifu na pembejeo zote ziwafikie wakulima kabla ya msimu na kwa idadi ambayo vyama vya msingi vitakuwa vimewasilisha katika kamati ya pembejeo.

Alisema serikali itasimamia kuhakikisha viuatilifu hivyo vinafika kwa wakati na kuondoa kero zilizowakumba msimu iliyopita.

Katika swali la msingi, mbunge huyo alihoji mpango wa serikali kuhakikisha pembejeo za korosho kwa msimu unaofuata zinapatikana kwa wakati na kwa bei nafuu.

Mavunde, akijibu swali hilo, alisema mahitaji ya pembejeo za korosho katika msimu wa 2023/24 ni tani 70,000 za salfa ya unga na lita milioni 3.4 za viuatilifu vya maji, mabomba 10,000 na magunia milioni 6.2.

Alisema wizara kupitia Bodi ya Korosho Tanzania inasimamia upatikanaji wa pembejeo za korosho kabla ya msimu kuanza ambapo Oktoba 15, 2022, kamati ya ununuzi wa pembejeo kwa pamoja ilitia saini mikataba na kampuni 14 kwa ajili ya ununuzi wa pembejeo hizo.

"Serikali kupitia Bodi ya Korosho Tanzania inaendelea kuratibu zoezi hilo ili kuhakikisha pembejeo zinawafikia wakulima kwa wakati na bei itakayopangwa kulingana na mahitaji," alisema.



Baadhi ya wabunge kutoka nchini Msumbiji wakiingia Bungeni jijini Dodoma jana walipofika kutembelea Bunge hilo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Mbunge ataka uwakilishi kundi la wazee bungeni

MBUNGE wa Viti Maalum (CHADEMA), Conchester Rwamlaza, ametaka wazee kupewa nafasi ya uwakilishi bungeni kama ilivyo kwa vijana na wanawake ili kutoa ushauri na kusikilizwa.

Akiuliza swali bungeni jana, mbunge huyo alitaka utaratibu ufanyike kama ilivyo kwenye viti maalum ili vyama vya siasa viwajibike na wazee wapate nafasi za uwakilishi ndani ya Bunge.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu), Patrobas Katambi, alisema kwa mujibu wa Ibara ya 66(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, kuna sharti la aina sita (6) za wabunge wa kuchaguliwa kuwakilisha majimbo ya uchaguzi.

Pia alisema wabunge wanawake wasiopungua asilimia thelathini ya wabunge wote, wabunge watano kutoka Baraza la Wawakilishi, Mwanasheria Mkuu pamoja na wabunge wasiozidi 10 wa kuteuliwa na Rais, na Spika iwapo hatakuwa amechaguliwa kutoka miongoni mwa wabunge.

"Kwa kuwa Ibara ya 67(1) (b) ya Katiba imeainisha moja ya sifa ya mtu kuwa mbunge ni lazima awe mwanachama na mgombea aliyependekezwa na chama cha siasa, hivyo tunatoa wito kwa vyama vya siasa nchini kutenga nafasi za uwakilishi wa wazee kama ilivyo kwa watu wenye ulemavu na vijana ili waweze kupata nafasi ya uwakilishi bungeni," alisema.

Katambi alisema sheria inatoa haki kwa vyama vya siasa kupata wawakilishi kwenye vyombo mbalimbali.

"Kuna chama kina umoja wa vijana, umoja wa wanawake na wazazi na uwakilishi wake upo bungeni, hivyo nafasi hiyo inatolewa kulingana na utaratibu wa chama husika cha siasa," alisema.

## STAMICO yasuka mikakati kuinua wachimbaji wanawake

SHIRIKA la Madini (STAMICO) limeandaa mikakati kwa ajili ya wachimbaji wanawake ikiwamo kuwapatia mafunzo ya uchimbaji madini na maeneo mengine yanayohusiana na sekta hiyo.

Naibu Waziri wa Madini, Dk. Steven Kiruswa, alibainisha hayo jana bungeni alipojibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Neema Mwandabila.

Mbunge huyo alihoji mikakati ya serikali kuhakikisha wanawake wanakuwa miongoni mwa wachimbaji wa madini nchini.

Akijibu swali hilo, Dk. Kiruswa alisema serikali kupitia STAMICO ina jukumu la kuwasaidia wachimbaji wadogo wa makundi mbalimbali nchini, wakiwamo wanawake.

"STAMICO imeandaa na kutekeleza mikakati mbalimbali kuhakikisha wanawake pia wanakuwa wachimbaji madini nchini," alisema.

Alitaja mikakati hiyo inahusisha pamoja na mambo mengine, kutoa mafunzo mbalimbali ya nadharia na vitendo kwa wachimbaji wadogo wakiwamo wanawake kupitia vituo vya mfano vya Katente (Bukombe), Lwamgasa (Geita) na Itumbi (Mbeya).

"Pia kuwasaidia wachimbaji wadogo kupata taarifa sahihi za mashapo kwa kushirikiana na Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST) ambapo kwa sasa STAMICO imeagiza mitambo mitano ya uchorongaji maalum kwa ajili ya wachimbaji wadogo nchini ili kuwasaidia kufanya utafiti," alisema.

Pia alisema mkakati mwingine ni kuwaunganisha wachimbaji na taasisi za kifedha zikiwamo benki za CRDB, NMB na KCB kwa lengo la taasisi hizo kuwapa mikopo wachimbaji wadogo nchini, wakiwamo wanawake.

"Mkoa wa Songwe una leseni 15 za wanawake wanaojishughulisha na uchimbaji na biashara ya madini. STAMICO imeandaa mpango wa mafunzo kwa wachimbaji wadogo nchi nzima wakiwamo wachimbaji wanawake," alisema.

Alisema mpango huo katika Mkoa wa Songwe utatekelezwa ndani ya mwaka huu wa fedha 2022/23.




**Habari zote: Augusta Njoji**

**DODOMA**





## Ukosefu maji wawalazimu kununua dumu 500/-

**Na Mary Mosha,** ROMBO

WANANCHI wanaoishi na kufanya shughuli za kiuchumi katika ukanda wa tambarare wa Lower Rombo, mkoani Kilimanjaro, wanakabiliwa na tatizo la ukosefu wa majisafi na salama kwa zaidi ya miaka 50.

Kutokana na hali hiyo, wananchi wanalazimika kununua ndoo moja ya maji kwa Sh. 500.

Jana Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Msaranga, Fratern Arser, alisema wananchi wa kijiji hicho, wanakabiliwa na uhaba mkubwa wa maji hali inayowasababishia kukesha mtoni usiku kwa zaidi ya saa nne hadi tano wakigombania maji, ambayo hata hivyo, sio safi na salama kwa matumizi ya binadamu.

"Ni kweli tatizo la maji katika ukanda wa chini linawaathiri sana wanawake na watoto, hasa wanafunzi katika shule zetu za sekondari na msingi. Hali ni mbaya na wananchi masikini hawawezi kumudu kununua maji kwa kiwango hicho. Tunaomba serikali yetu itupie jicho eneo hili," alisema.

"Upatikanaji wa maji katika Wilaya ya Rombo, imekuwa ni tatizo kubwa na la muda mrefu. Kipindi cha kiangazi, tunakaa mtoni tukigombania maji hadi usiku wa manane."

Mkazi wa kijiji hicho, Julius Tarimo, akizungumzia kero hiyo alisema, kutokana na uhaba huo, baadhi ya watu wenye uwezo wamechimba visima na wamepata maji na kuanza kuuza kwa bei ghali.

Elizabet Simon, alisema kwa sasa wanalazimika kununua maji kwa bei ya Sh. 500 ili kujikimu na maisha ya kila siku.

Baadhi ya wanafunzi wa Shule ya Sekondari Kirachi, akiwamo Frank Joseph, alisema kwa sasa wanalazimika kukatisha vipindi darasani ili kwenda kutafuta maji kwa ajii ya matumizi mbalimbali ikiwamo kupikia, kufanya usafi wa nguo na mwili.

Vilevile, Diwani wa Kisale Msaranga, Mathius Assenga, alisema katika kata yenye shule za msingi sita na za sekondari mbili, zinakabiliwa na tatizo la maji na wanafunzi wake wanahaha kuhemea maji mtoni na vijiji jirani vya ukanda wa milimani.

Alipotafutwa kuzungumzia madai hayo, Msimamizi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira, Wilaya ya Rombo, Martin Kinabo, alisema kwa sasa wapo kwenye mchakato wa kukamilisha miradi mnne itakayosaidia upatikanaji wa maji ukanda huo.

"Tutakapoanza utekelezaji wa miradi hiyo, vijiji 41 vitanufaika. Kwa sasa vijiji vyenye hali mbaya ni 18. Kimsingi ni vijiji 30 vya ukanda wa kati tu, ambavyo vinapata maji mara tatu kwa wiki na ukanda wa chini ni vijiji 22 na ukanda wa juu vijiji 19.

"Ujenzi wa Mradi wa Mji wa Whona/ Marangu hadi Tangi la Amboni na Mradi wa Njoro II kutoka Rongai hadi Mashati, umetengewa zaidi ya bilioni 6.4 na mkandarasi yupo eneo la mradi tayari.

"Kwa Msaranga, tumetenga Sh. milioni 30 kwa ajili ya uchimbaji wa kisima kirefu kitakachosaidia vijiji vya Msaranga na Mahorosha."

Aidha, Kinabo alisema wametenga Sh. bilioni 1.4 kwa ajili ya uboreshaji wa huduma ya maji katika vijiji vya Holili Mjini, Holili Vijijini Mengwejuu, Ngoyoni, Kelamfua, Ibukoni, Ikuini, Mahorosha na Msaranga.

# Waonywa kugeuza chumba cha kuhifadhi maiti kukusanya mapato

**Na Hamida Kamchalla,** HANDENI

SERIKALI imeionya Menejimenti ya Hospitali ya Wilaya ya Handeni, mkoani Tanga, kutumia chumba cha kuhifadhia maiti kama chanzo cha ukusanyaji wa mapato.

Onyo hilo lilitolewa jana na Mkuu wa Mkoa huo, Omari Mgumba, baada ya kupokea malalamiko ya wakazi wa Kata ya Kibaoni, Wilaya ya Handeni, wanaolalamika kutozwa fedha nyingi wanapokwenda kuchukua au kuwahifadhi kwa muda ndugu zao.

"Naelekeza na haya ndio maagizo yangu. Mganga Mfawidhi wa Hospitalii hii ya Handeni na Mganga Mkuu wa Wilaya, kuanzia sasa msitumie tena chumba cha kuhifadhia maiti, kama chanzo kikuu cha kukusanya mapato ya ndani ya halmashauri.

"Mnapomhifadhi marehemu, ndugu zake wanapokuja kumchukua, wapeni, tena bure. Haya malalamiko ya wananchi wa Kata ya Kibaoni yana mantiki na yanasikilizika."

Kabla ya Mgumba kusitisha utozaji wa fedha katika chumba hicho, Ramadhan Kusaka, alisema mgonjwa anapoaga dunia ni lazima aingizwe kwenye chumba hicho na ndugu wanapokwenda kuichukua wanalazimishwa kulipia Sh. 10,000.

"Ikitokea huna pesa ya kuulipia, hawawezi kupewa mwili wa ndugu yako. Mheshimiwa Mkuu wa mkoa, tunaomba utusaidie hili suala.

Katika hatua nyingine, Mgumba, alipokea malalamiko ya wananchi hao kuhusu utata wa usajili wa walengwa wa kunusuru kaya masikini katika wilaya hiyo.

Akiwa Vibaoni, Mkuu wa Mkoa, alielezwa kuwa baadhi ya wananchi wanabaguliwa na kuna upendeleo unatumika kuwabaini na kuwaingiza watu kwenye mpango huo unaotekelezwa chini ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

Kutokana na malalamiko hayo, Mgumba aliwaelekeza Wenyeviti wa Serikali za Mitaa na Vijiji, wanao andikisha wananchi wasio na sifa za kupata fedha za mpango wa kunusuru kaya maskini kuacha upendeleo, vinginevyo watawajibika.

"Toeni elimu kwa wananchi ambao wanaostahili kupata fedha hizo na majina ya walengwa yasomwe na kupitishwa kwenye mkutano mkuu wa mtaa au kijiji na kila aliyekuwa na miaka kuanzia 18 anapaswa kushiriki.

"Mnachagua huyo mnayemuona ni maskini anajadiliwa na kila mtu ajiridhishe kweli ni maskini anastahili kupata hiyo hela, mridhie japo kwa asilimia 32 kati yenu, lakini msichague kwa ajili ya uzee maana kuna tofauti ya uzee na umaskini, unaweza ukawa kijana, lakini huna kipato chochote wala mtu wa kukusaidia na ukawa mzee na mali.

"Sasa utakuta Mwenyekiti, amejifungia ndani na washirika wake anachagua, fulani aliniunga mkono, kanipigia kura yule anafaa anaandikia na wengine anapeleka TASAF."

Kipindi cha pili cha awamu ya tatu ya mradi wa kunusuru kaya maskini nchini, unatekelezwa na TASAF katika halmashauri zote 185 za Tanzania Bara na Zanzibar.



Mkurugenzi wa Maipac na Mjumbe wa Bodi Misa-Tan, Mussa Juma akitoa nasaha kwa wahitimu na wageni katika mahafali ya Chuo cha Uandishi wa Habari Fanikiwa Arusha mwishoni mwa wiki jijini humo. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Serikali kuja na mpango maalumu kambi za upasuaji

**Na Oscar Assenga,** TANGA

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, amesema serikali inafikiria kuja na mpango maalum wa kambi za upasuaji za huduma za kibingwa ili kukabiliana na uhaba wa madaktari hao nchini.

Akizungumzia mpango huo, alisema uamuzi wa kuja na kambi hizo unalenga kuwasaidia Watanzania kufanyiwa uchunguzi, kupata matibabu, dawa na vifaa tiba bila gharama yoyote.

Ummy alikuwa akizungumza jana na wakazi wa Jiji la Tanga, wakati wa mpango wa kutoa huduma za upasuaji wa kibingwa bila malipo, kwa wakazi wa jiji hilo.

"Tanzania bado ina uhaba mkubwa wa madaktari bingwa, kwa hiyo mambo haya ya kuja na kambi ya upasuaji wa huduma za kibingwa unahitajika sana kwa sasa na sio Tanga peke yake, bali ni mikoa yote nchini," alisema.

Kambi hiyo inatekelezwa na madaktari bingwa kutoka Taasisi ya Peleks Humanitarian Organization ya Uingereza.

Jumla ya wagonjwa 380 hadi sasa wamekuwa na kambi hiyo kati ya watu 7,000 waliolengwa.

Kambi hiyo ya matibabu bingwa ya upasuaji imewezeshwa na Taasisi ya Watumishi Health Check, Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Tanga Bombo na Ofisi ya Mbunge wa Jimbo la Tanga mjini kwa pamoja wamewaleta wataalamu hao kutoka nchini Uingereza.


Mkurugenzi wa Watumishi Afya Check, Dk. Siraji Mtulia, alisema upasuaji huo ulianza Novemba 5 na utakoma ifikapo Novemba 11, mwaka huu na utagharimu Sh. milioni 876.

Kwa upande wake, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Dk. Seif Kallage, alisema uwapo wa kambi hiyo ni jitihada za Waziri Ummy kutokana na jukumu alilopewa na Rais Samia Suluhu kuhakikisha afya za Watanzania zinaimarika na kuboresha huduma.

Alisema hata kampeni ya Mama Samia aliiendeleza kwa kuanza na Tanga kushirikiana na Peleck na anaendelea na mikoa mengine nchini.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Dk. Jonathan Budemu, alisema kambi hiyo itawasaidia wananchi na katika watu 700 waliochunguzwa na madaktari walikuwa hawana uharaka na mwendelezo wa kambi hiyo utawasaidia kuwaona.

Alimuomba Mstahiki Meya kipindi cha uchunguzi, wananchi watakaokosa maeneo ya kuwaweka, wawaweke kwenye vituo vingine baada ya upasuaji kama Ngamiani na Makorora na vya jirani ili wote waweze kupata huduma kwa wakati.





## TFA yajivunia kujiendesha kifaida miaka sita

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MKURUGENZI Mtendaji wa Chama cha Wakulima wa Tanganyika (TFA), Justine Shirima, amesema kwa kipindi cha miaka sita kuanzia 2016 hadi 2021, chama hicho kimeimarika na kusimama upya kwa kuwa wamefanikiwa kujiendesha kwa faida.

Aidha, alisema kutokana na kuimarika kwa chama hicho, wanatarajia mwaka ujao wataanza kutoa gawio kwa wanachama wake.

Shirima aliyasema hayo jana jijini hapo wakati wa mkutano mkuu wa mwaka wa wanahisa wa TFA.

"Chama hiki kina historia ndefu kidogo, tangu ilipoanzishwa mwaka 1935 na katika kipindi chote cha uendeshaji ilipitia katika tatizo la kutokutengeneza faida na kwa mujibu wa utaratibu wa kampuni ili uweze kutoa gawio inabidi uwe umetengeneza faida.

"Kwa sasa tumetengeneza faida, lakini bado haijafikia kiwango cha kulipa gawio kwa kuwa bado hatujaandaa hasara zilizopatikana miaka ya nyuma," alisema.

Vilevile, alisema hadi walipofanya mkutano huo, kulikuwapo na ongezeko la ukusanyaji wa mapato kutoka Sh. bilioni 4.5 kwa mwaka 2017 hadi kufikia Sh. bilioni 12.9 na biashara yao imekuwa kwa asilimia 89.

Pia alisema TFA ndio taasisi pekee hapa nchini yenye mtandao mpana kuliko taasisi nyingine, katika mchakato wa usambazaji wa pembejeo za kilimo kwa wakulima kwa kuwa wana matawi zaidi ya 17.

Shirima, alisema kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa, aliwataka wakulima kuchukua tahadhari kwa kulima mazao ya muda mfupi yanayostahimili ukame ili wasipate hasara.

Akizungumza kwa niaba ya wanachama wanzake, John Mbanga, alisema kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa wanaiomba serikali kuwapatia ruzuku ya pembejeo za kilimo kwa wakulima hasa wa vijijini.

"Tunaiomba serikali kutoa ruzuku na kushusha gharama za pembejeo za kilimo ikiwamo mbegu, mbolea na viuatilifu ili wakulima waweze kufaidi kwa kuwa kwa sasa gharama ziko juu," alisema Mbanga.



Mkuu wa Kikosi cha Askari wa Usalama Barabarani Mkoa wa Manyara, Georgina Matagi (kulia), akiwasikiliza madereva pikipiki (bodaboda) wanaofanyakazi zao ndani ya ukuta unaozunguka migodi ya madini ya Tanzanite Mji Mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro, wakati akikagua vyombo vya moto na kutoa elimu ya usalama barabarani juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Milioni 480/- zapelekwa Pangani kutatua shida ya maji

**Na Oscar Assenga,** PANGANI

WAKAZI wa maeneo ya Madanga, Kimang'a na Jaira, Wilaya ya Pangani, mkoani Tanga, wako mbioni kuondokana na adha ya maji iliyodumu kwa zaidi ya miaka 25, baada ya serikali kupeleka zaidi ya Sh. milioni 480 za ufumbuzi wa tatizo hilo.

Msimamizi wa Mradi wa Uboreshaji wa Miundombinu wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira jijini Tanga, Aboubakari Mtili, alisema mradi huo ni mahususi kwa ajili ya kuhudumia wakazi wa Kijiji cha Madanga.

Mtili alikuwa akizungumza na wakazi wa kijiji hicho jana, wakati Tanga UWASA ilipokwenda kutambulisha mradi huo.

"Kutokana na kuwapo kwa tatizo hilo, Wizara ya Maji, ilifikiria kuchimba visima katika maeneo haya ili kuongeza upatikanaji wa maji, lakini havikuwa na maji ya kutosha.

"Kwa sababu hiyo basi, tumeamua kwenda kuchukua maji katika eneo la Boza, ambako kuna visima."

Aidha, alisema katika utekelezaji wa mradi huo, wamepanga kutumia vibarua kutoka kwenye eneo hilo, na wananchi watapata ajira ya kuchimba mitaro na kazi nyingine.

Alisema mradi wa Madanga na Kimang'a ulikuwa na shida ya maji muda mrefu na kupitia mradi huo, wananchi watapata maji ya kutosha.

Awali Ofisa Uhusiano wa Tanga UWASA, Devotha Mayalla, alisema mradi huo utasaidia kero ya maji kwa wananchi na kuwataka wawe mabalozi wa kuhakikisha wanautunza na kulinda.

# Wazazi wasiofuatilia watoto wao wapewa onyo

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

IDARA ya Udhibiti Ubora wa Shule ya Wilaya ya Arumeru, mkoani Arusha, imewashukia wazazi na walezi wanaowekeza nguvu zaidi kutafuta mali na kuacha jukumu la kulea watoto wao, wakiamini kazi hiyo ni ya walimu.

Imewakumbusha kujenga uhusiano wa karibu na watoto wao ili kusaidiana kufanya vizuri katika masomo yao na kuendeleza vipaji.

Mdhibiti Mkuu Ubora wa shule wa Halmashauri ya Meru, Aurelia Kiwale, alieleza kutofurahishwa na hali inayoendelea sasa, wakati alipokuwa akizungumza katika mahafali ya 13 ya kidato cha nne ya Shule ya Sekondari St. Mary's Duluti.

Alisema kumekuwapo na tatizo kubwa la ukosefu wa ajira kwa vijana wengi wanapohitimu elimu mbalimbali, walimu wakibuni njia za kuendeleza vipaji vya watoto, itawasaidia wanapohitimu kuwa na ajira kulingana na kipaji alichonacho.

"Lakini ili kufikisha ndoto hii lazima wazazi na walimu washirikiane pamoja na hii itasaidia sana taifa, kwani wengi wakijiajiri kwa kuwa na shughuli mbalimbali za ujasiriamali, kulingana na vipaji vyao walivyoendelezwa, itawasaidia na kuacha kulilia serikali kutowaajiri," alisema.

Kiwale alisema kwa sasa serikali inakusanya maoni kwa wadau namna ya kuboresha mitaala, ili mwanafunzi anapohitimu ajiajiri na kuondokana na changamoto ya ajira, huku akiwataka kutoa maoni endapo watahitajika kufanya hivyo, ili kuwezesha vijana nchini kuondokana na changamoto ya ajira.

"Sasa hivi hatutaki tena suala la watoto wetu kuzunguka na bahasha mtaani kwani limekuwa ni kero kubwa, unakuta mtoto amefaulu vizuri changamoto inakuja kwenye ajira, hivyo nawaomba walimu kuendeleza na kukuza vipaji vya watoto wetu, ili suala la ajira liweze kuwa historia kwa nchi yetu," alisema.

Mkuu wa Shule ya Sekondari ya St. Mary's Duluti, Essau Mlengule, alisema shule imekua ikifanya vizuri katika matokeo kwa kila mwaka na hiyo ni kutokana na elimu nzuri ambayo wakifundishwa na walimu hao, hasa somo la ujasiriamali ambalo linawawezesha kuwa wabunifu.

Mlengule aliwataka wahitimu hao kutambua kuwa kufika kidato cha nne sio mwisho wa elimu na kutaka wajiendeleze zaidi kwa kuwa wamesoma ili wakatatue changamoto zinazoikabili jamii inayowazunguka, huku akiwataka kuwa wabunifu na kushiriki kikamilifu kwenye kazi za mikono na ujasiriamali.

Alisema kwa sasa wanapambana kutafuta vyanzo mbadala vya fedha ili kuboresha mazingira ya kusomea na kujifunzia kwa wanafunzi na walimu na kuomba msaada wa upatikanaji wa jengo la utawala.

"Pia hatuna viwanja bora vya michezo, lakini tunakabiliwa na tatizo kubwa la mwamko mdogo wa wanafunzi kujisomea bila kusimamiwa, pamoja na kuwapo kwa ushiriki mdogo kwa baadhi ya wazazi katika malezi ya pamoja kwa vijana wawapo shuleni," alisema.

Aliwataka wahitimu hao kutambua mafanikio ya kweli hayaji kwa njia za mkato, kutokufuata taratibu za jumuiya husika, kujichukulia maamuzi bila ruhusa ya mamlaka husika, bali kufanya kazi kwa bidii, maarifa na kwa malengo, kujiamini, kuwa weledi katika kazi zao sambamba na kutanguliza nidhamu katika kila jambo.

Wahitimu kwa upande wao, Eben Liston na Alphonsia Mlengule, walisema kuna uboreshaji mkubwa wa miundombinu ya shule hiyo ikiwamo bwalo la chakula, maabara ya kisasa, pamoja na uboreshaji mazingira ya shule kwa kupanda miti ya kivuli vyote vimewezesha kuboresha kiwango cha elimu shuleni hapo.

"Tunashukuru shule hii kwa kuweza kutuandaa kujiajiri kwa kutusisitizia somo la ujasiriamali ambalo litatuwezesha kujiajiri na kuondokana na changamoto ya kuanza kusaka ajira mtaani," alisema.



Ukurasa 16

NDIVYO ULIVYO UMUHIMU BIMA YA AFYA KWA WOTE



Monica, mwalimu wa ufundi ujenzi anayevuta wasichana kuwa wajenzi

Ukurasa 15

SAYANSI

NA DK. FELICIAN B. KILAHAMA

## NGORONGORO NI ZAIDI YA WANYAMA, WATU (2)

# Kumesheheni maajabu viumbe adhimu na adimu, nyayo mtu wa mwanzo, mchanga unaotembea

TUNAMSHUKURU Mwenyezi Mungu anayetuhurumia na kutupa tena nafasi ya kuishi na kuendelea kujifunza mambo mengi yakiwamo maajabu yaliyoko Tanzania.

Katika toleo lililotangulia nilifafanua kuhusu kuanzishwa kwa Hifadhi ya Ngorongoro na jinsi shimo au kreta ilivyotokea.

Katika mwendelezo wa leo makala inatazama vitu gani mtalii awe wa ndani au nje ataweza kuviona na kufurahia urithi asilia unaopatikana Tanzania pekee.

Neno 'crater' au 'kreta' kwa Kiswahili, wataalamu walioko Ngorongoro, wanathibitisha kuwa Kiswahili sanifu kwa jina hilo ni 'kasoko' hivyo, eneo hujulikana kama 'kasoko ya Ngorongoro'.

Nimefuatilia asili ya jina 'Ngorongoro' hivyo kulingana na ufafanuzi wa Wamasai wakazi wa eneo hilo, ni muunganisho wa maneno mawili 'ngoro' na 'ngoro'.

Inasemekana Wamasai walioku-wapo zama za kale, walikuwa na ng'ombe waliofungwa kengele shingoni inayoitwa 'ngoro' hivyo, walipokuwa wakichunga katika 'kasoko' ya Nogorongoro wakawa wanasikia mlio au sauti iliyotolewa na hizo kengele: 'ngoro;'ngoro'.

Kutokana na hali hiyo Wamasai wakawa wanatumia hayo maneno na hatimaye wakoloni kuanzia Wajerumani miaka ya 1800' na Waingereza kwenye miaka ya 1900 wakalipa jina eneo hilo likajulikana kama 'Ngorongoro' mpaka sasa.



Maajabu katika kreta ya Empakaai. **PICHA: MTANDAO**

**UPEKEE WA HIFADHI**

Ngorongoro inatokana na upekee wa vivutio vilivyoko katika eneo hilo, ambavyo ni pamoja na 'kasoko' au kreta kadhaa iko ya Ngorongoro, kreta ya Empaakai na kreta ya Olmoti.

Kreta hizo tatu zipo sehemu moja na zote zina wanyama ndani yake ni vivutio vya aina yake ulimwenguni kote.

Isitoshe kuna tambarare katika eneo la Ndutu maarufu sana kama sehemu ya kuzalia nyumbu. Hivyo mtalii yeyote akitembelea Ngorongoro ataweza kuziona kasoko hizo za aina yake katika sehemu moja na eneo la uzazi wa wanyama hao.

Aidha, atatembelea eneo la kuzalia nyumbu, kadhalika, katika Hifadhi ya Ngorongoro, kuna vivutio vingine licha ya wanyama mbalimbali wakiwamo tembo, simba, nyati, faru (hasa mweusi) na chui.

Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa sababu Tanzania imejaliwa kuwa na faru wa kutosha ndani ya Hifadhi ya Ngorongoro peke yake.

Kuna faru wanaoishi ndani ya kasoko ya Ngorongoro lakini baadhi wakiwa nje ya kasoko hususani katika msitu mnene wa hekta 89,200, wa nyanda za juu kaskazini.

Pamoja na hayo wapo wanyama wengine wengi kama nyumbu, pundamilia, duna, fisi, mbwamwitu, swalapala, kongoni, mbweha ambao mtalii ataweza kuwaona na kuwafurahia.

**MALIKALE OLDUVAI**

Kusema kweli, Ngorongoro ni sehemu pekee nchini yenye vivutio vya malikale vya aina yake. Mathalani, yapo makumbusho ya "Olduvai" inayoaminika kuwa chimbuko la binadamu wa kale (earliest humans' settlements).

Tafiti za wataalamu wa malikale na historia ya binadamu zinaonyesha kuwa eneo hilo ndilo lilikaliwa na binadamu wa kale kuliko sehemu nyingine duniani; mpaka kufahamika kama "eden ya Afrika inayopatikana Ngorongoro nchini Tanzania.

**MCHANGA MIUJIZA**

Vilevile, kuna eneo la 'Laetoli' lenye nyayo za binadamu wa

INAENDELEA UK. 18

ELIMU

NA MICHAEL ENEZA

# Redio sasa zinapenya, kutumika kama fasihi shirikishi kila kona

## Ni kuingia ngazi mpya, kuizungumzia jamii kwa undani



Vituo vya matangazo ya redio visivyohitaji miundombinu mikubwa vikifanya kazi ndani ya jamii. **PICHA: MTANDAO**

UWEPO wa redio masafa mapana ya maeneo madogo (FM) bila kuhitaji mitambo mikubwa na kusikika kila mahali umewezesha taifa kuwa na wingi wa vyombo vya habari vinavyohudumia Watanzania wengi hata walioko vijijini wakitumia redio za jamii.

Aidha, idadi ya washiriki wa fani ya habari, inaungana na sanaa za maonyesho redioni, kuleta sura mpya katika baadhi ya vyombo vya tasnia hiyo kwenye juhudi za kuwafikishia ujumbe wasikilizaji.

Ni mazingira ambayo katika historia ya sanaa na fasihi yanakumbushia kilichotokea katika bara la Ulaya kuelekea mwisho wa enzi ya utawala wa kifalme na mfumo wa kimwinyi, kabla ya kuingia mfumo wa mali binafsi na siasa za ushindani za kidemokrasia.

Fasihi ilikuwa njia ya kujieleza kwa kificho bila kuulizwa, tofauti na kutoa maoni, au uhojiwe ana kwa ana na wenye utaalamu wa kuuliza maswali.

Leo pia mitandao inapasua mawingu na kusambaza habari bila kungoja kuhojiwa huku mingine ikirusha ujumbe na taarifa kutoka mbali na kuwafikia wengi wanaotumia majukwaa hayo.

Wapo wengi wanaotoa ujumbe mfano tiktok kwenye video za aina mbalimbali zinaonyesha yale ambayo si lazima yatoke Tanzania.

Ipo angalau hadithi moja ya mazungumzo mitaani kati ya watu kadhaa, iwe ni wanafamilia na wengine ni marafiki, kuzungumzia masuala kadhaa ya Sheria ya Maudhui ya Mawasiliano (mitandao ya kijamii).

Hivi karibuni lilitolewa onyo kuhusu aina za maudhui (ambayo ni tafsiri ya neno 'content' ambalo ni pana zaidi, kugusa kinachoonyeshwa kwa jumla kwenye mitandao iwe twiter, WhatsApp , TV mtandaoni, redio na blog wakati maudhui ni mwelekeo au hisia za kinachoonyeshwa, kimojawapo au kadhaa.

Kiuhalisia maudhui ni kama ushauri wa hadhi, kwa mfano ushauri unaotolewa na kuhani katika madhababu ya aina hii au ile. Kuna uhusiano kiasi fulani kati ya jamii ya Tanzania hivi sasa na mfumo huo wa Ulaya, ambako kuna maeneo kadhaa ya maingiliano ya kijamii yasiyojadiliwa waziwazi.

Ni kutokana na vizuizi vya kisheria kwani mjadala unatoa mwanya kwa wanaopendelea mwelekeo tofauti na kilichoainishwa katika sheria kujieleza, suala ambalo si muafaka kwa chombo cha habari. Kwa hali hiyo msukumo wa jinsi hisia zinavyojiinua kwa masuala kama hayo zinaelekezwa kwingine, si kwa hoja.

Tofauti hii inaingia katika mtazamo wa fashihi kwa jumla kuwa ni mtiririko wa kinachotokea katika jamii, familia, marafiki, vijiweni au kwenye starehe na siyo kilichorasimishwa au kinachotaka kuwa rasmi kwa kujieleza.

Watu wakiwa wanaongea nyumbani kwao au vijana wakiwa vijiweni wakibishana kuhusu jambo fulani, kimsingi wanabadilisha mawazo na kinachoongelewa hapo hakina uwezo wa kutafsiriwa kama mwelekeo rasmi kwa mtu yeyote.

Na mara nyingi kinachoongelewa katika mazingira hayo husahaulika, hakuna kumbukumbu ya soga za jana au juzi, hivyo mtiririko wa hadithi kuhusu soga hizo pia hauna madhara; hakuna aliyesimama akajitambulisha na kuongea hili au lile.

Inafahamika kuwa kazi ya vyombo vya habari kimsingi ni kuhabarisha, kufurahisha au kuburudisha, kuonya, kuweka mwelekeo fulani wa kitaifa au ajenda.

> Tofauti hii inaingia katika mtazamo wa fashihi kwa jumla kuwa ni mtiririko wa kinachotokea katika jamii, familia, marafiki, vijiweni au kwenye starehe na siyo kilichorasimishwa au kinachotaka kuwa rasmi kwa kujieleza.

Iwe ni redio, runinga, mitandao au magazeti jukumu kubwa ni hilo. Pale inapotolewa habari za tukio fulani, wahusika ni wenye mamlaka ya kutoa maelekezo au kufafanua maelekezo yaliyopo kuhusu suala husika. Ila kuhusisha mara nyingi ni kwa utashi tu wa chombo husika, kutafuta mtaalamu wa suala husika ili atoe mawazo kama raia mwenye uelewa mpana au wa kina wa suala hilo, na siyo kama msemaji wa kitaaluma wa jambo lenyewe. Hapo ingebidi atafutwe msimamizi wa kisera atoe ufafanuzi unaoitwa 'elimu' ya suala hilo.

Ina maana kuwa katika mawasiliano kila kitu kina mahali pale na umuhimu wake, kuwa akizungumza msimamizi sera au utaratibu katika eneo fulani yale atakayosema ni msimamo au elimu. Akiongea mtaalamu anaweza kutoa elimu au ushauri wa kina kwa maana ya maoni ambayo si rahisi kuonyesha udhaifu wake, na ndiyo maana anakuwa mtaalamu.

Akiongea mtu mwingine katika hali kwa mfano ya kuhojiwa anatoa maoni ambayo yanaweza kuchangia kupima uadilifu au usahihi wa kilichotangulia kusema au kujadiliwa, iwe ni mtazamo wa mtu mwingine, na hata elimu au msimamo wa awali.

Ukitaka kukwepa yote hayo unatoa hadithi ya mazungumzo ya nyumbani, mtaani au kijiweni, ambako hakuna mwenye hadhi kutoa elimu.

Ndiyo maana redio zama hizi zipo kuzungumzia mengi katika jamii na kuhoji kunakoonekana kuna changamoto au tatizo ambalo halipati mzungumzo rasmi anayetoa mwelekeo pengine wa kile kinachotakiwa kuonekana ndani ya maudhui.

Wasanii wakiwamo wa filamu, michezo ya kuigiza, wana muziki nao wamo wakifikisha ujumbe ambao jamii inauhitaji zaidi ili kuifundisha, kuiburudisha na hata kuionya kuwa mwelekeo au jambo au baadhi ya mambo ni kinyume.

ELIMU

NA PILLY KIGOME

# Monica, mwalimu wa ufundi ujenzi anayevuta wasichana kuwa wajenzi



Mwalimu Monica akiwa kazini, wanafunzi wake wakiendelea na ujenzi. **PICHA: PILI KIGOME**

TUNAPOZUNGUMZIA mama si lazima awe mzazi, hata yule aliyekutoa kutoka hatua moja kwenda nyingine ya kukuinua kielimu, mtaji, ushauri tena akikupa mwanga wa kumuda maisha yako ni mama.

Anachukua nafasi hiyo maana anakuonyesha njia ya kutoka iwe kwa kuajiriwa au kujiajiri na kufanikiwa kuendesha maisha yako ya kila siku, naye anabaki kuwa mama, hata kama hukunyonya maziwa yake.

Monica Ndalilileko (56) anayefundisha Chuo cha Ufundi Uhuru Mchanganyiko jijini Dar es Salaam ni 'mwalimu mama' aliyewakwamua vijana wengi na kuwatoa woga, kuwaondoshea fikra mgando za mfumo dume wasichana waliokuwa wakiogopa kazi za ufundi kwa mawazo kuwa ni fani ya kiume.

Waliamini kuwa iwe kujenga, kupiga matofali, kupaka rangi, kuchora ramani za majengo, kuezeka ni majukumu ya kina kaka pekee.

Kupitia ushawishi wake, kuwatia moyo na kufuatilia wanachopata baada ya kuhitimu darasani, tayari vijana wengi wake kwa waume wamepata ajira sehemu tofauti na kufanyaka kazi zilizodhihirisha vipaji vyao katika jamii walikojiajiri au kuajiriwa katika fani ya ufundi ujenzi.

Monica anasema ni kutokana na ajira hizo na kufundisha mafundi kadhaa waliopitia mikononi mwake limekuwa jambo linalomheshimisha na kukuza jina lake.

"Ni kitu kinachoniletea faraja kubwa katika ualimu wangu huu wa ufundi ambao sijajuta kuusomea na kuufundisha." Anaongeza.

Anapozungumza na Nipashe hivi karibuni, anasema kuwa ilikuwa ni ngumu kwa ndugu hata wazazi kukubali maamuzi yake ya kuchagua kusomea ufundi ujenzi kwani wengi walimkatisha tamaa kwa chaguo lake hilo lilionekana halikuwa sahihi.

Anasema alipenda ufundi kutoka moyoni ufundi na alisonga mbele bila ya kumsikiliza mzazi au yeyote asemalo kumpinga na tayari anamshukuru Mungu kwa mafanikio makubwa.

Monica ni muhitimu kutoka Sekondari ya Moshi Technical mkoani Kilimanjaro ambaye baadaye aliendelea na fani ya ufundi katika Chuo cha Ualimu cha Ifunda mkoani Iringa akipata mafunzo ya ngazi ya cheti.

Baada ya kuajiriwa akiwa kazini, hakuchoka aliongeza kielimu katika Taasisi ya Ufundi Dar es Salaam -DIT miaka mitatu kuanzia 2006 hadi 2009 akisomea uhandisi.

> "Ilionekana kama ufundi ujenzi ni jukumu la wanaume pekee na waliokuwa tayari washashindwa maisha, hivyo hamasa ilihitajika kwenye kuwasukuma vijana kupenda kujifunza ufundi wa eneo hilo."

Monica alianza ualimu wa ufundi ujenzi katika mazingira magumu akiwa na wanafunzi wanne darasani mnamo Julai 1990, akiwafundisha nadharia, vitendo pamoja na somo la michoro ya majengo au technical drawings, anasema.

Anakumbusha kuwa hapo awali wakati ameajiriwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwenda Chuo cha Ufundi Uhuru Mchanganyiko, hakukuwa na mwamko wa jamii kuanzia wazazi hadi walezi kuwapeleka watoto wao kwenye fani ya ufundi ujenzi.

"Ilionekana kama ufundi ujenzi ni jukumu la wanaume pekee na waliokuwa tayari washashindwa maisha, hivyo hamasa ilihitajika kwenye kuwasukuma vijana kupenda kujifunza ufundi wa eneo hilo."

Anasema kituo kilianza na vijana wachache lakini aliamua kukitangaza katika vyombo vya habari ikiwamo redio ya umma na za binafsi kama Radio One ndipo wanafunzi wakaanza kujitokeza na kuongezeka kidogo kidogo kadri siku zinavyoenda na sasa kimekuwa ni kituo kikubwa na kinatoa mafundi bora wanaoajiriwa na kujiajiri sehemu mbalimbali.

Anasema chuo hicho awali kilikuwa kinapokea wanafunzi waliomaliza shule ya msingi pekee wale ambao walikuwa hawajachaguliwa kuendelea na sekondari ila kwa sasa wanapokea hata wale waliomaliza kidato cha nne kutoka shule mbalimbali.

"Leo imeonekana kuwa kumbe ufundi ni ajira ambayo inaweza ikamtoa mtu na kumwajiri au kuajiriwa kama ilivyo kazi zingine." Anasema Monica.

Aidha, hapo awali kulikuwa na hofu ya wasichana kujifunza ufundi, walikuwa hawajitokezi lakini kwa sasa uelewa katika jamii unakua wakati wote hata wasichana wanajitokeza kujifunza fani hiyo ya ufundi ujenzi.

Anaeleza kuwa chuoni hapo katika fani ya ufundi ujenzi anawafundisha wanafunzi kozi mbalimbali kama za bomba, kupaka na kuchanganya rangi, kuezeka na kuchora ramani za majengo.

### CHANGAMOTO

Mwalimu Monica anakabiliwa na changamoto ya wazazi wanaojitokeza kuleta wanafunzi chuoni hapo na kutaka watoto wao wasomeshwe bure bila gharama yoyote kwa madai ya kuwa serikali inatoa gharama na kwamba elimu ni bure.

Anasema hilo ni tatizo kubwa linalomkabili kwasasa kwakuwa jamii, walezi na wazazi hawana uelewa wa tangazo hilo la serikali kuwa elimu inagharamiwa na serikali, hivyo ufundi umekuwa ni tofauti na elimu za kawaida kwa kuwa kumekuwa na gharama ya kununua vifaa katika somo la vitendo na licha ya taifa kugharamia elimu haijigusi kwenye gharama hizo.

Anafafanua: "Kwa miaka hii kumekuwa na changamoto ya kupatikana kwa wanafunzi kwasababu ya tangazo kuwa elimu ni bure nchi nzima hivyo wazazi na walezi wanafahamu kuwa elimu na hata vyuo vya ufundi elimu hutolewa bure jambo ambalo si sahihi."

Anasema hata hivyo ni ngumu kumpokea mwanafunzi mwenye dhana hiyo kwakuwa Wizara ya Elimu haina bajeti ya kugharamia elimu ya ufundi.

Kituo hicho kwa sasa kinatoa wanafunzi wa ngazi ya cheti daraja la pili kitaalamu wanaitwa mafundi mchundo (mafundi wasaidizi).

Katika kilele cha Siku ya Elimu ya Watu Wazima banda la Chuo cha Uhuru Mchanganyiko alikokuwa Monica likiwa na wanafunzi anaowafundisha lilikuwa moja ya maeneo ya mvuto katika maonyesho hayo yaliyofanyika katika Chuo Kikuu cha cha DUCE jijini hapo.

Banda hilo lilikuwa na mwanafunzi kiziwi anayependa fani hiyo kutokana na kumwelewa mwalimu wake tofauti na kozi nyingine ambazo aliwahi kupelekwa na wazazi wake lakini akiishia njiani kutokana na kutokukifahamu anachofundishwa.

ELIMU

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

# NDIVYO ULIVYO UMUHIMU BIMA YA AFYA KWA WOTE



Daktari Bingwa wa Macho kutoka Nazneen Shariff akiwapatia tiba wananchi waliojitokeza kupata huduma hiyo. **PICHA: MARCO MADUHU**

WAKATI uliopo ni sasa hasa kwa kila mmoja kupata huduma ya afya sheria itakayowawezesha wananchi kulipia huduma ya afya kabla ya kuumwa ili maradhi yanapojitokeza iwe rahisi kutibiwa.

Ni vyema kuanzia sasa wananchi kuhamasishwa umuhimu wa kuwa na bima ya afya na kuchangia kiasi kitakachoelekezwa na serikali kwa kiwango cha familia na kwa mtu mmoja mmoja, ili unapougua utibiwe.

Hamasa na kuelimishwa wananchi kuchangia tiba ni muhimu kwa sababu umaskini unaweza kusababisha ulemavu na kifo hasa mgonjwa anapokosa fedha za matibabu anapoyahitaji.

Hilo linadhihirishwa mbele ya mbunge wa viti maalum mkoa wa Shinyanga Lucy Mayenga, anayeratibu zoezi la kutoa matibabu ya macho bure kwa wananchi, wanaomweleza kuwa wengine wangekuwa vipofu kutokana na kukosa fedha za kutibiwa macho.

Matibabu ya macho bure kwa wananchi wa mkoa wa Shinyanga yanayotolewa na madaktari bingwa wa macho kutoka Taasisi ya Bilal Muslim Mission of Tanzania Free Eye Camp, yanawafikia watu mbalimbali mwezi uliopita, mamia wakijitokeza kupata huduma.

Wananchi wengi waliojitokeza wanasema ukosefu wa fedha za matibabu umekuwa kikwazo kwao na hata wengine wakikaribia kuwa vipofu, wakati kambi hiyo ikipokea utitiri wa wenye matatizo ya uoni kwa kuanzia mtoto wa jicho na presha ya macho wakihitaji kupata huduma hiyo, hali iliyoonyesha watu wengi wanakabiliwa na matatizo ya magonjwa mbalimbali si macho pekee.

Mratibu wa Taasisi ya Bilal Muslim Mission of Tanzania Free Eye Camp, ambaye ni kiongozi wa jopo la madaktari bingwa wa macho Ain Sharif, anasema katika mkoa wa Shinyanga wamewafanyia watu 167 upasuaji wa mtoto wa jicho, huku wengine zaidi ya 4,000 wakipata huduma ya macho ya kawaida.

Anasema idadi kubwa ya watu wamejitokeza kupata huduma ya matibabu ya macho bure na kwamba ndani ya miaka yao 25 tangu waanze kutoa huduma hiyo hawajawahi kuwafanyia upasuaji wa macho wagonjwa 116 kwa siku, akiongeza kuwa Shinyanga imeweka rekodi mpya.

Madaktari bingwa wanatoa elimu ya usafi wa macho na kutahadharisha wananchi kuwa usafi na kujikinga na vumbi ni jambo la kuzingatia na muhimu pia kunawa mikono na uso wa macho ili kuepuka uchafu au mchanga kuingia machoni na kusababisha maradhi.

Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Shinyanga, Lucy Mayenga, anasema uamuzi wa kuleta madaktari wabobezi wa macho ni ili kutoa matibabu bure kwa wananchi na kuwaokoa na upofu kutokana na magonjwa mengi kama mtoto wa jicho, ukungu na presha za macho hasa kwa wagonjwa wenye kisukari.

Anasema Shinyanga ina uhaba wa madaktari bingwa wa macho, jambo lililomgusa kuamua kuratibu zoezi hilo la kutoa matibabu bure ya macho, ili wananchi watibiwe hasa kwa sababu wengine hawana uwezo wa kulipia gharama za tiba.

"Shinyanga kuna uhaba wa madaktari bingwa wa macho na pia wananchi wengi hawezi kumudu gharama za matibabu ya macho kutokana na hali ngumu ya maisha, kama mama na mbunge nikaona ni vyema nilete madaktari hawa wabobezi kuwatibu bure wananchi wetu," Lucy.

Mganga Mfawidhi Hospitali ya Rufani Shinyanga, Dk. John Luzila, anakiri hospitali hiyo ina uhaba wa madaktari bingwa wa macho, na kubainisha kuwa juhudi zimefanyika na serikali imeshawapeleka masomoni kusomea fani hiyo.

Anaeleza kuwa tatizo la macho ni kubwa lakini tiba yake ni ghali kwa mfano kufanya upasuaji wa mtoto wa jicho unagharimu kati ya Shilingi 300,000 hadi 350,000 kwa jicho moja iwapo ni yote mawili gharama ni takribani 700,000.

Anaongeza kuwa kama uvimbe ni mkubwa zaidi gharama ni kubwa pia inagharamu Shilingi 700,000 kupasua jicho moja na kwamba ni gharama kubwa na mambo yanakuwa magumu hasa kutokana na kukosa bima ya afya na fedha mfukoni shida inapotokea.

Baadhi ya wananchi waliopatiwa huduma akiwamo Robert Mkangala, aliyetolewa mtoto wa jicho analalamikia gharama kubwa za matibabu ya macho akisema wenye hali ya chini wamekuwa na wakiumia zaidi ndiyo wengi wanaoshindwa kuzimudu na kusababisha kuendelea kuumizwa na magonjwa na hata kupata upofu.

"Kwa mfano hapa Shinyanga ukienda hospitali kupata huduma ya matibabu ya macho, jicho moja linatibiwa kwa Sh. 230,000, ukienda Bugando kwenye matibabu ya rufani mkoani Mwanza ni Sh. 320,000, anasema Mkangala.

"Mwaka jana nilipoona nazidiwa sioni vizuri ilibidi nitafute pesa na kufanyiwa upasuaji jicho la kushoto katika Hospitali ya Kolandoto hapa Shinyanga nikatoa Sh. 230,000, japo nilipaswa kufanyiwa upasuaji macho yote, kutokana na ukosefu wa fedha nikatibiwa moja," anaongeza.

Mkangala anaeleza kuwa ujio wa madaktari bingwa wa macho mkoani Shinyanga umemaliza tatizo lake kwani amekamilisha upasuaji wa jicho la kulia ambalo halikutibiwa kwa kukosa fedha.

Mwaka 2013, Happiness William, anasema aligundulika na tatizo la mtoto wa jicho na kuhitajika kufanyiwa upasuaji, lakini kutokana na ukosefu wa fedha za matibabu na pia hana bima ya afya alilazimika kutumia dawa na siyo upasuaji macho yakazidi kuharibika.

Anasema mwaka huu hali yake ilikuwa mbaya zaidi, kwa sababu ilifikia hatua ya kutumia miwani lakini nayo ikiwa changamoto huku akiingiwa na hofu ya kuwa kipofu kwa sababu hakuwa na fedha wala bima ya afya na akakwama kufanyiwa upasuaji.

"Umaskini ni kitu kibaya nilikuwa naelekea kuwa kipofu tena nikijiona nashukuru juhudi za mbunge Lucy Mayenga kwa kutuletea hawa madaktari wabobezi nimefanyiwa upasuaji macho yote mawili na sasa naona vizuri," anasema Happiness.

Nchambi Ndiganya ambaye amepokea matibabu anaiomba serikali kupunguza gharama za matibabu ya macho, ili wenye kipato kidogo wamudu na kuepushwa na upofu.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, anapongeza juhudi za wadau kutoa huduma hiyo ya matibabu kwa wananchi wa mkoa huo, akitoa wito kwa wananchi kufuatilia taarifa za masuala ya bima ya afya kwa wote na pia kupima afya zao mara kwa mara ili kujiepusha na gharama kubwa zinazosababisha kushindwa kumudu matibabu.




Wananchi wakipatiwa tiba ya macho iliyoendeshwa kwa hisani ya Taasisi ya Bilal Muslim Mission of Tanzania Free Eye Camp.

SAYANSI

NA GAUDENSIA MNGUMI

KUELEKEA NISHATI SAFI

# Kazi ianzie kuondoa kodi majiko ya umeme ya presha

## Daladala, mwendokasi ziwekwe gesi kupunguza uchafuzi wa hewa mijini




Punguzo la kodi kwenye majiko ya umeme yanayotumia presha linaweza kuwa mwanzo wa kutumia nishati safi jikoni. **PICHA: MTANDAO**

HAKUNA utafiti unaoweza kutoa takwimu za moja kwa moja zinazoonyesha idadi ya watu waliopoteza maisha kutokana na kutumia nishati isiyo salama au chafu hasa kuni, mbolea ya mifugo na mabaki mengine ya taka.

Lakini, ukweli unabakia kuwa kupikia mbolea ya ng'ombe, mbuzi, magunzi na mabaki mengine ya mimea kumesababisha vifo vya watu wengi hasa wanawake kutokana na kuuliwa kwa kisingizio kuwa ni wachawi kwa vile wana macho mekundu.

Mamia ya kinamama hao walihukumiwa kifo kwa kukatwa katwa mapanga na watoto waliowazaa. Aidha, wapo waliowakodishia wauaji kutoka vijiji jirani.

Ni mauaji yaliyotokea Kanda ya Ziwa mikoa ya Mwanza, Simiyu, Geita, Shinyanga, Tabora pia yakisambaa maeneo ya Kigoma na Kagera tena yakipewa jina la 'mauaji ya vikongwe wanawake'.

Nishati chafu pamoja na kusababisha magonjwa ya njia ya mapafu kuanzia homa ya mapafu, saratani, maradhi ya moyo na macho, kuna simulizi nyingi zilizotokana na mateso ya kutumia kuni na nishati nyingine zilizowatesa kinamama na wasichana jikoni ambao leo hawapo.

Licha ya tatizo kuwepo kwa miongo kadhaa ni sasa serikali imetangaza kuwa inaandaa mkakati na itaunda kikosi kazi cha kuishauri na kuibua mipango ya kutekelezwa kuhakikisha kuwa Watanzania wanakuwa na nishati safi na bora.

Waziri wa Nishati, Januari Makamba, anautangazia umma mwisho wa kupika na kulia machozi, kupata mafua na kuungua na kuteseka kwa joto kali litokanalo na nishati chafu jikoni.

Ni hatua bora inayosisitizwa na Rais Samia Suluhu Hassan, kuwa kikosi hicho kitakachoundwa na wadau kutoka sekta ya umma, binafsi na washirika wa maendeleo kitaleta mapendekezo na masuala ya kutekelezwa ili kupata nishati mbadala na bora ya kupikia.

Wakati serikali inasubiri mapendekezo ya kikosi kazi, ni muda wa kuamua kuondoa kodi kwenye vifaa vya umeme vya kupikia kama majiko yanayotumia nishati kidogo yakipika kwa mvuke.

Majiko hayo ya 'electric pressure cooker' yanauzwa kuanzia 200,000 lakini kama kodi zitaondolewa au kupunguzwa na pia waagizaji kupewa ruzuku huenda yakapatikana kwa bei nafuu na kufikishwa vijijini kwenye nishati chafu zaidi na uharibifu wa mazingira.

Ruzuku kwa gesi ni jambo muhimu lakini gharama za kutumia gesi ni kubwa kwa vile Watanzania wengi wanazungumzia kuchemsha maharage, makande na vyakula vigumu ambavyo vinahitaji kiasi kikubwa cha gesi.

Mbadala wa gesi unaweza kuwa umeme na hasa kwenye majiko ya presha yanayopika kwa uniti chache ikimaanisha kuwa kilo mbili za maharage zinaweza kuivishwa na uniti chache karibu Shilingi 700, hivyo kuweka mkazo kwenye umeme ni jambo jema.

Uchunguzi unaofanywa na Nipashe maeneo mengi unagundua kuwa majiko ya umeme ya presha yapo madukani lakini mengine hufikia hata Shilingi 300,000 na kukwamisha wenye kipato kidogo kuyanunua.

Nishati chafu kama kuni huuzwa ghali na haipatikani kwa wingi kutokana na uharibifu wa mazingira na kuvuna miti na mazao mengine ya misitu ya asili hali inayochangia kukosekana huduma hiyo sokoni.

Kadhalika mkaa nao unafikia Shilingi 2,000 kwa kipimo kidogo ambacho licha ya kuwa ni vipande vidogo vya matawi ya miti hakiwezi kupika hata kilo moja ya maharage bila kuongeza kingine.

Kwa uwiano huo ni wazi kuwa nishati safi na salama kwa wakati huu ni umeme hivyo serikali ianze mchakato wa kupunguza au kuondoa kodi ili kushusha bei ya vifaa vya kupikia.

Kodi zikipungua kuanzia majiko na gharama ya 'uniti' ya umeme hatua kwa hatua, Tanzania itaanza kupikia nishati safi, kama serikali inavyofikiria.

Lakini ni vyema kuhamasisha wananchi vijijini na kuwafundisha matumizi ya majiko hayo na kuachana na upishi wa kuni na nishati zisizo salama.

### GESI ASILIA

Gesi asilia (LNG) au hata hiyo ya kwenye mitungi (LPG) haikubaliki tena duniani licha ya kuwa nayo ni nishati salama. Ni kutokana na kuchangia kuongeza hewa ukaa 'carbon dioxide' na kuchangia kuzalisha joto zaidi na kuchochea mabadiliko ya tabianchi.

Gesi iwe asilia iliyoshindiliwa kwenye mitungi LNG na iliyo ile iliyochunjwa kutoka kwenye mafuta na kupakiwa kwenye mitungi si salama kwa mazingira ikielezwa kuwa inatokana na mabaki ya viumbe hai au visukuku-fossils ambavyo huzalisha hewa ukaa.

Hata mkaa wa mawe nao unaoelezwa na serikali kuwa unasafishwa na kuandaliwa na wataalamu wa Tanzania nao kwa mujibu wa wataalamu wa usalama wa mazingira si salama kwa vile kadhalika ni masalia ya viumbe hai hao au fossils.

### MAGARI YA GESI

Hamasa iliyoko duniani leo ni kuachana na matumizi ya nishati zinazotokana na visukuku na kujikita kwenye nishati safi ya jua, upepo, maji bahari, joto ardhi na taka za mimea, hivyo kikosi kazi kiliangalie suala hilo pia.

Licha ya nchi zinazoendelea kujiaminisha kuwa matumizi ya nishati hizo za makaa ya mawe na gesi hayakwepeki kwa mataifa hayo ikiwamo Tanzania.

Ukweli unabakia kuwa hewa ukaa au 'carbon' husafiri duniani kote na hubebwa na upepo, unaoutoa Afrika hadi Ulaya, Amerika na China,

ukitawanya hewa ukaa ardhini na angani duniani kote bila kujali mzalishaji wa hewa ukaa ni taifa gani.

Hata hivyo, haiwezekani kuachana na matumizi ya gesi au makaa ya mara moja kama ambavyo hatua zinachukuliwa na mataifa ya Ulaya na Magharibi kwa ujumla, nchi zinazoendelea kama Tanzania pamoja na kufikiria kutumia nishati safi jikoni ni muhimu pia kuitumia gesi kwenye vyombo vya barabarani.

Magari yaanze kutumia gesi ya LPG na LNG pengine juhudi zinaze na yale yanayotoa huduma za usafiri mijini hasa daladala lakini pia na ya mwendokasi ili kupunguza kiwango cha takasumu zinazozalishwa na moshi wa injini za magari na vyombo vingine barabarani.

Vituo vya gesi vya kujaza nishati hiyo kwenye magari viwekwe vya kutosha kazi ikifanywa zaidi na sekta binafsi kwa kuwa ndiyo wamiliki wa biashara ya mafuta maeneo mbalimbali.

Kwa sababu kuna watalamu wa kubadili injini za mafuta na kuzipeleka kwenye muundo unaotumia gesi ambao ni Chuo Kikuu cha Usafirishaji (NIT), mabadiliko hayo yapewe nafasi ili nishati safi isiishie jikoni bali na barabarani pia.

Kwa Tanzania nishati safi inayotazamiwa kuanzia kutumiwa jikoni inalenga kuachana au kukomesha ukataji miti ovyo ili kupata mkaa na kuni.

Ujio wa nishati safi ni mkombozi wa mengine mengi maana uhaba kuni na utafutaji wake ulichochea ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto, wanapokwenda porini au shambani kusaka kuni.

Ni wazi wamekutana na machungu kama kuuliwa baada ya moshi kuwaumiza macho kwa muda mrefu hasa mikoa ya Mwanza, Simiyu, Geita, Shinyanga, Rukwa na Kigoma.

Pamoja na wanawake wazee kuuliwa kinamama na mabinti wamebakwa, kulawitiwa, kupigwa nyumbani kuchelewa porini na hata kutelekezwa na mume kuwakimbia.

Lakini nishati chafu ilipoteza sana muda au wakati wa wanawake vijijini na hata mijini wakitembea maporini, mashambani na vichakani tena wakishindwa kufanyakazi nyingine za uzalishaji na kuzidi kuwa maskini.

Watoto walishindwa hata kwenda shuleni na hili liliwaathiri wasichana ambao walikuwa wakijiunga na mama na walezi wao kusaka nishati hiyo maporini, yote hayo yakiwasababisha udhalilishwaji kijinsia kama kubakwa, kuozwa utotoni na hata kushambuliwa na wanyamapori.

NGORONGORO NI ZAIDI YA WANYAMA, WATU (2)

# Kumesheheni maajabu viumbe adhimu na adimu, nyayo mtu wa mwanzo, mchanga unaotembea

INATOKA UK. 13

kale au zamadamu, walioishi hapo zamani sana miaka zaidi ya 3,000,000 iliyopita.

Kulingana na ufafanuzi nilioupata kutoka kwa mmoja wa wataalam walioko Ngorongoro Kassim Nyaki, Hifadhi ya Ngorongoro pia inatukio linalovutia la 'mchanga' unaohama kimujiza.

Inaaminika mchanga huo unahama bila kuachana unaondoka kama lundo katika umbo la nusu mwezi na hufanya hivyo kwa kutumia wawimbi ya upepo kuelekea upande wa mashariki mwa Hifadhi ya Ngorongoro.

Uzoefu unaonyesha kwamba mchanga huo unahama kwa umbali wa mita 17 hadi 20 kwa mwaka. Hii ina maana kwamba ukitembelea eneo hilo ukaukuta sehem fulani, ukaweka alama, ukirejea pale baada ya mwaka mmoja utakuta rundo hilo la mchanga lipo umbali wa takribani mita 20 kutoka ulipouacha.

Aidha, mchanga huo unaaminika kuwa ulitokana na mlipuko wa volkano katika Mlima Oldonyo-Lengai, wakati huo majivu yenye asili ya 'volkano' yalirushwa na hatimaye kujikusanya na kutengeneza kitu chenye umbo la nusu-mwezi.

Hata hivyo, hakuna maelezo ya kuaminika ilikuwaje mpaka itatokea umbo la aina hiyo na hatimaye kuwa na kanuni ya kusogea taratibu sana, kutoka sehemu moja kwenda nyingine, bila kuachana.

**UTALII IKOLOJIA**

Tasnia ya utalii ina mambo mengi pia watalii wenyewe wana mahitai tofauti. Hivyo, wapo wenye kupenda kuona na kufurahia uumbaji wa ajabu wa Mungu.

Hali hiyo inajulikana kuwa ni utalii wa Kiikolojia na au jiolojia, lakini pia tukihusisha na masuala yanayohusu malikale mfano, Korongo la Olduvai ndani ya hifadhi ya Ngorongoro kuna masuala ya zamadamu

Vilevile, kuna Laetoli inayofahamika kama ni maajabu kuhusiana na 'nyayo za binadamu wa kale ambazo bado zinaonekena hadi leo. Ni vyema kutembelea Ngorongoro ushuhudie mwenyewe maajabu ya uumbaji wa Mungu. Miamba katika maeneo ya Olduvai, Laetoli; Jabali la Nasera, ni moja ya maeneo ya utalii wa kuangalia miamba (Geopark); 'kasoko' ya Ngorongoro na Kreta ya Empaakai iliyoko karibu na Mlima, Oldonyo-legai ni vivutio muhimu kuona.

Kwa upande mwingine, miongoni mwa vivutio muhimu vilivyoko katika Hifadhi ya Ngorongoro, ni 'msitu wa Nyanda za Juu Kaskazini'.



Faru weusi ni wanyama wanaopatikana ndani ya kreta-kasoka. Watalii wakisafiri kutembelea maajabu ya Ngorongoro yaliyo ya kipekee duniani. **PICHA: FELICIAN KILAHAMA**

Msitu huu una sifa ya makazi muhimu mahususi kwa wanyama wakubwa mathalani, nyati, faru, tembo, pofu, chui na wanyama wengine adimu kama chui, faru mweusi, na duma.

Inasadikiwa kwamba wanyama hawa watatu ni vigumu kuwaona mchana. Vilevile, kuna ndege adimu kama 'European Bee-eater'; 'Palled Harrier', na 'Lesser Kestrel'.

Ndege na wanyama wanategemea sana rasilimali misitu kwa maisha yao hivyo eneo la msitu likiharibiwa, wanahamia sehemu nyingine lenye ikolojia sahihi ya kuwafaa kwa maisha yao.

Kuwepo misitu ndani na nje ya eneo la hifadhi ni neema maana licha ya kuwa makazi ya wanyama ni chanzo kikubwa cha mvua na maji yanayotumiwa na wanyama pamoja na binadamu katika maeneo mbalimbali yanayozunguka hifadhi ikiwa ni pamoja na vijiji vya Wilaya za Karatu, Monduli, Loliondo na Meatu.

Baadhi ya mito yenye vyanzo vyake kutokana na misitu na uoto wa asili uliohifadhiwa vizuri katika eneo la hifadhi ni pamoja na Mito 'Munge', 'Mama Hhau', 'Mto wa Mbu', Mto 'Oltogon' katika kijiji cha Endulen, na mingine inayotiririsha maji kutoka ndani ya hifadhi kwenda kwenye mashamba ya vitunguu eneo la Mang'ola wilayani Karatu.

Hivyo juhudi za serikali zinazolenga kuhifadhi rasilimali zilizomo katika Hifadhi ya Ngorongoro ni vizuri jamii iziunge mkono ili uhifadhi katika eneo hilo uwe endelevu na kwa faida ya kizazi cha sasa na vitakavyofuata.

Ikolojia ya Ngorongoro ina manufaa mengi siyo tu kwa wanyama na Wamasai wanaoishi humo bali hata kwa jamii nje ya mipaka ya Hifadhi. Kwa pamoja tutafanikisha maana umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu.

## WANENAVYO MALENGA

# UNAZIBA

Kama wewe unaziba, jua nawe utazibwa,
Kama wewe unakaba, jua nawe utakabwa,
Kama wewe unaiba, vyako pia vitaibwa,
Mpende jirani yako, ujipendavyo mwenyewe.

Ya watu unayabeba, yako pia yatabebwa,
Wasababisha misiba, nawe jua utakumbwa,
Huzingatii katiba, na yako yatasiribwa,
Mpende jirani yako, ujipendavyo mwenyewe.

Unamcheka kahaba, kwamba dhambi yake kubwa,
Lakini chako kiroba, ni mla rushwa mkubwa,
Hata penati wakaba, masahibu wanakumbwa,
Mpende jirani yako, ujipendavyo mwenyewe.

Ule wosia wa baba, kwa wadogo na wakubwa,
Upendo usiwe haba, beba wanotaka bebwa,
Wa njaa weze shiba, huo hasa ni ukubwa,
Mpende jirani yako, ujipendavyo mwenyewe.

Njia unazosiriba, asali isijelambwa,
Na makufuli ya shaba, milango inavyopambwa,
Watakaokwenda ghuba, na balaa wamekumbwa,
Mpende jirani yako, ujipendavyo mwenyewe.

Ulipo wewe mjomba, sitaki hadi kulambwa,
Wanakuja wanaomba, mikono sijekufumbwa,
Fanya jambo wataimba, kupata kilichoombwa,
Mpende jirani yako, ujipendavyo mwenyewe.

Maisha kama yabamba, ni nakshi imepambwa,
Furaha raha kutamba, mkononi una mbwa,
Uwe mjini na shamba, mabaya si wa kukumbwa,
Mpende jirani yako, ujipendavyo mwenyewe.

Ziada kwenye kiroba, na jirani unaombwa,
Mlango usijeziba, na balaa utakumbwa,
Toa hata mara saba, Baraka hazitaombwa,
Mpende jirani yako, ujipendavyo mwenyewe.

Ubakie unatamba, na hata nyimbo kuimbwa,
Mwenzio akate kamba, iwe sherehe kuimbwa,
Mchanga utaulamba, na dhoruba utakumbwa,
Mpende jirani yako, ujipendavyo mwenyewe.

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**

ELIMU

**NA SABATO KASIKA**

# Kiarabu kupewa msukumo kidato cha tano, sita sekondari za umma

## Ni juhudi kupata wataalamu kutafsiri lugha za kimataifa



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, akimpa cheti mmoja wa wahitimu, Sarah Kirorombo. **PICHA ZOTE: SABATO KASIKA**

KIARABU, ni miongoni mwa lugha kubwa zinazotumika duniani hata ndani ya Umoja wa Mataifa (UN). Kutokana na ukubwa huo, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inaahidi kulipa msukumo somo la lugha hiyo, ili ifundishwe kidato cha tano na cha sita kwenye sekondari za umma.

Kwa nini? Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, anataja sababu ya kufanya hivyo kuwa ni kutaka kuzalisha wataalamu watakaokwenda kufanya kazi za tafsiri lugha hiyo kimataifa.

Ni katika mahafali ya kidato cha nne ya Shule za Kiislamu za Ilala Mkoa wa Dar es Salaam, yaliyofanyika katika uwanja wa Garden jijini Dar es Salaam juzi, ambapo alikuwa mgeni rasmi.

"Ambalo ninapenda kuahidi hapa, ni kulipa msukumo mara moja, ni hili la 'kombinesheni', tuwe na kombinesheni au tahasusi ambayo mojawapo ni hili somo la Kiarabu kwenye shule za serikali," Prof. Mkenda anasema.

Anasema lugha ya Kiarabu inatumika na dini ya Kiislamu, na pia lugha kubwa barani Afrika na ni ya kwanza kutoka nje ya nchi ya Tanzania na kwamba si vizuri kufundisha, Kifaransa, Kichina, Kiingereza na kuacha Kiarabu.

"Hatua hii ya kufundisha lugha ya Kiarabu itatusaidia sisi kuandaa watu watakaokwenda kutumia Kiswahili kama wakalimani, kwa sababu huwezi kuwa mkalimani kama unajua Kiswahili halafu hujui lugha nyingine," anasema.

Prof. Mkenda anasema ukalimani ni lazima mtu ajue lugha kadhaa, na kwamba Kiarabu ni lugha barani Afrika na inaweza kuwa ni ya kwanza au ya pili na kufafanua kuwa inatambulika na Umoja wa Mataifa.

**MAADILI MEMA**

Aidha, Prof. Mkenda anageukia jamii na kusema, haiwezi kukwepa kwenye suala la malezi bora kielimu na kimaadili na kwamba ushirikiano wa pamoja unahitajika kati ya jamii na walimu.

"Ni wajibu wa walimu na wenye shule kuhakikisha kuwa watoto wanapata malezi ambayo wazazi wanataraji ikiwamo kuwapo maadili mema, ambayo ni msingi wa kuimwezesha mwanafunzi kufanya vizuri katika masomo.

Prof. Mkenda anatoa wito kwa viongozi wa dini kwa kushirikiana na wamiliki wa shule, huku akihimiza walimu kusimamia malezi ya vijana, ili kuhakikisha suala la maadili mema linakuwa la muhimu.

Waziri Mkenda anaongeza kuwa suala la maadili linatakiwa kuwapo hata katika kusimamia mitihani, kwa kuwa watoto wanapofundishwa kuibia mitihani, ni sawa na kuwafundisha kuwa wezi wa baadaye.

Ni kutokana na video zilizosambaa katika mitandao ya kijamii zikionyesha baadhi ya wanafunzi wakifanya mambo ambayo ni kinyume na maadili, ambazo anasema zilishtua serikali, viongozi wa dini na jamii. "Ninalaani vikali wale walioruhusu ule mchezo wa shule hizo pale Kisarawe na picha zikapigwa. Haiwezekani walimu hawakujua, hairuhusiwi na tunaahidi kwamba tutachukua hatua zaidi," anasema.

Anasema huo ni utovu wa nidhamu uliofanywa na baadhi ya wanafunzi wa shule wilayani Kisarawe wakati wa mahafali ya kidato cha nne, na kwamba kuwa uchunguzi wao wa awali umebaini walimu wamewapa wanafunzi uhuru kufanya mambo yasiyokuwa na maadili katika sherehe za shule.

**ELIMU KWANZA**

Shekhe wa Mkoa wa Dar es Salaam, Alhaj Dk. Musa Salim, anasema katika uislamu, suala la elimu limepewa kipaumbele, na kwamba tangu mtu anapozaliwa hadi anapofariki anapaswa kuendelea kujifunza, ambapo anawataka wanafunzi hao kuishika elimu.

"Tunawahusia watoto wetu, tunaowaaga leo na watakaoendelea, kushikamana na maadili, elimu haina maana yote mbele ya jamii iliyokosa maadili, ninyi ndio taifa la baadaye, nchi hii inawategemea katika suala la maadili, endapo taifa litakosa maadili ni sawa na kusema taifa hilo ni mfu," anasema Alhad Musa.

Aidha, anaitaja jamii ya kiislamu kujitafakari kwa kuwa ndio inayoongoza kwa mmomonyoko wa maadili, akitolea mfano kuwa kati ya panya road 10, saba ni waislamu, jambo linaloitia aibu serikali na jamii kwa ujumla.

"Jamii isieneze picha au video zinazoonyesha vitendo visivyo na maadili katika mitandao ya kijamii kwani hiyo inachangia kuporomosha maadili mema. Mfano mojawapo ni video iliosambazwa ikionyesha wanafunzi wa shule ya mkoani Pwani wakifanya matendo yasiyo na maadili," anasema.

**MMOMONYOKO**

Akitoa taarifa ya maendeleo ya shule hizo kwa niaba ya wakuu wenzake, Mkuu wa Shule ya Al Haramain, Buhero Issa anasema shule 11 zinakabiliwa na mmomonyoko wa maadili ya wanafunzi, kutokana na somo la dini kutotahiniwa na Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA).

"Mahafali haya yanafanyika kwa mara ya 11 yakihusisha sekondari 11 za Kiislamu kutoka Dar es Salaam, ambazo ni Kunduchi, Ununio, Tekeme Islamic, Muzdarfa Islamic, Dar es Salaam Islamic, Al Haramain, Hijra Islamic, Nuru Islamic na Kinondoni Muslim," anasema Issa.

Issa anaongeza kuwa shule hizo zimekuwa zikifanya vizuri kitaaluma na kutolea mfano kwamba, mwaka jana asilimia 98 ya wanafunzi katika shule hizo walifanikiwa kujiunga na kidato cha tano.

"Lakini shida iliopo ni kwamba zinakabiliwa na mmomonyoko wa maadili kwa wanafunzi, na sababu ni somo la dini kutotahiniwa na Baraza la Mitihani (NECTA) na kutohesabiwa katika madaraja kidato cha nne," anasema.

Mmoja wa wanafunzi wanaohitimu kidato cha nne, Mwanaisha Khadir anasema wanategemea kupata matokeo mazuri na kuendelea na masomo ya juu kwa kuwa wameandaliwa vyema na walimu wao.

Mwanafunzi huyo anasema hayo kupitia risala ya wahitimu aliosoma mbele ya mgeni Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda kwa niaba ya wanafunzi wenzake.



# HABARI PICHANI



Waenda kwa miguu wakipita juu ya daraja kuvuka upande wa pili wa Barabara ya Morogoro eneo la Mbezi Mwisho Dar es Salaam juzi, baada ya kuwekwa uzio eneo hilo ili kuepusha ajali za barabarani. **PICHA: SABATO KASIKA**



Mkurugenzi wa Taasisi ya Taka ni Ajira Foundation, Allen Kimambo (wa pili kushoto), akizungumza jijini Dar es Salaam jana, wakati wa uzinduzi wa programu ya Siku ya Waokota Taka Duniani ambayo kila mwaka huadhimishwa Novemba 2-9. Kushoto ni Mratibu wa Sera wa Taasisi ya Nipe Fagio, Veronica Hollela. **PICHA: MIRAJI MSALA**



Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Omari Mgumba (kulia), akipata maelezo kwa Diwani wa Kata ya Ngomeni wilayani Muheza, Bakari Mhando (kushoto) baada ya kufanya ziara katika Kitongoji cha Tononoka, Kijiji cha Kigongomawe wilayani humo. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## CHEMSHABONGO NA -00 21 00-

Na Felix Magezi
felixmagezi@gmail.com

Dondoo: Kulia
1. papasa kidogo
5. chukuliwa mgongoni
8. hali ya kuwa sawasawa
10.kamilifu 11. Uo
12.hali ya kuongea kwa gadhabu
13.mtu anayebagua watu wasiofuata misingi yake ya dini
15.Kaka yake Mama
16.malizika kwa kitu 19.kielekezi
20.kiitikio cha shikamoo
23.hekima 24.karatasi ngumu
25.kilevi cha sukari na mchele

Chini:
1. kibubutu
2. kinyume cha mchana
3. mbolea 4. mwanzo
6. elimu ya uuzaji na ununuzi wa bidhaa 7. jambo la kushangaza lisilo la kawaida 9. sadikisha
14.dalili ya jambo fulani
17.taarifa 18.mzazi wa kiume
19.mji mkuu wa zamani Romania
21.rejea 22.msimu wa mavuno wakati wa kipupwe

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 2 | 3 | 4 | ■ | 5 | | 6 | | 7 |
| 8 | | | | 9 | ■ | ■ | | ■ | |
| 10 | | | | | | ■ | 11 | | |
| 12 | | | | | ■ | ■ | | ■ | |
| ■ | 13 | | | | 14 | ■ | 15 | | |
| ■ | ■ | | ■ | 16 | | 17 | | ■ | ■ |
| ■ | 18 | ■ | 19 | | | | | | ■ |
| 20 | | 21 | | | | | | ■ | 22 |
| ■ | 23 | | | | | | ■ | ■ | |
| 24 | | | | ■ | 25 | | | | |
| ■ | ■ | | ■ | ■ | ■ | | ■ | ■ | |

Kamilisha jedwali kwa kujaza maneno yafuatayo:

KAMISHENI
BALAKI
KOMESHA
BAMAKO
AMALI
AMINA
LALAMISHA
MILANGO
ALASIRI
KINASA
BANDIA
NAAM
UTAMU
SHAIRI

ASI
IRA
KAA
SAA
AHA
UMA
URU
UANGA
ATIA
USO

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | ■ | ■ | |
| | | | | | ■ | K | A | A |
| | | | | | | | ■ | |
| | | | | | ■ | | ■ | |
| | | | | | | | | |
| | ■ | | | | ■ | | | |
| ■ | | | | ■ | | | | ■ |
| | ■ | | ■ | | | | | |
| | | | | | | ■ | ■ | |
| | ■ | ■ | ■ | | | | | |

Majibu toleo lililopita

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| K | E | N | Y | A | ■ | A | G | U | A |
| A | ■ | A | ■ | ■ | ■ | D | ■ | ■ | D |
| K | A | M | A | T | W | A | ■ | ■ | A |
| A | M | B | I | A | ■ | B | ■ | M | ■ |
| ■ | B | A | B | A | ■ | U | M | B | A |
| H | A | R | I | R | I | ■ | ■ | A | ■ |
| A | ■ | I | K | A | M | A | ■ | O | A |
| M | ■ | ■ | A | B | A | D | I | ■ | S |
| A | D | A | ■ | U | R | A | T | H | I |
| K | ■ | G | ■ | ■ | A | M | A | A | ■ |
| I | J | A | P | O | ■ | U | ■ | I | ■ |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| D | A | M | U | ■ | ■ | M | ■ | L |
| H | ■ | T | H | A | M | A | N | I |
| A | G | U | A | ■ | ■ | M | ■ | B |
| N | ■ | M | B | A | B | A | N | E |
| A | N | W | A | N | I | ■ | ■ | R |
| ■ | ■ | A | ■ | G | A | I | D | I |
| M | ■ | ■ | ■ | U | ■ | D | U | A |
| K | U | J | I | K | W | A | A | ■ |
| U | ■ | U | ■ | I | ■ | D | ■ | ■ |
| U | T | A | K | A | T | I | F | U |



# Jela maisha kwa kuongoza ubakaji wa makundi

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Mkoa wa Mbeya, imemhukumu kifungo cha maisha jela, Hance Mwakyoma (22) baada ya kupatikana na kosa la ubakaji wa makundi.

Mwakyoma alishtakiwa kwa kuwaongoza wenzake wawili kumbaka binti mwenye umri wa miaka 18.

Mshtakiwa alitenda kosa hilo Mei 20, 2022 usiku wakati binti huyo akitoka kwenye sherehe ya kumuaga (send-off) dada yake ambayo haikuwa mbali na nyumbani kwao.

Akisoma hukumu hiyo juzi, Hakimu Mfawidhi Mkoa wa Mbeya, Zawadi Laizer, alisema mahakama imeridhika na ushahidi wa upande wa mashtaka kupitia vielelezo na mashahidi wasiopungua watatu akiwamo binti aliyetendewa unyama huo. Alisema ushahidi wa Jamhuri ulibainisha mtu huyo kutenda kosa hilo kwa kushirikiana na wenzake wawili na ushahidi uliotolewa na mtendewa.

Ilidaiwa mahakamani hapo kuwa mtendewa alikutana na mshtakiwa na kumwita ili kufanya naye tendo la ndoa, lakini alikataa ndipo aliposhirikiana na wenzake wawili kumchukua hadi kwenye nyumba ya binti huyo.

Ushahidi huo ulidai kuwa baada ya kufika katika nyumba yake yenye vyumba vitatu alimlazimisha kufanya naye kitendo hicho na baadaye akawaita marafiki zake wawili kufanya naye kitendo hicho bila ridhaa yake hali iliyomsababishia maumivu.

Hata hivyo, ilidaiwa mahakamani hapo kuwa wawili hao hawakukamatwa na kufikishwa mahakamani kwa kosa hilo.

"Maelezo hayo yanaelezwa kutotikiswa na ushahidi wa upande wa utetezi ambapo mshtakiwa alikuwa akikana kutenda kosa hilo akisema alisingiziwa licha ya kwamba wakati watatu hao walitekeleza azma yao hiyo majira ya saa nne usiku, ilionekana watu hao walikuwa wamelewa na kuwa mshtakiwa na mwathiriwa walikuwa wanafahamiana kabla ya tukio hilo," alisema Laizer.

Mwendesha Mashtaka Mwandamizi wa Serikali, Wakili Deusdedit, aliiomba mahakama kutoa adhabu kali kwa mshtakiwa ili iwe funzo kwake na jamii kwa ujumla kutokana na baadhi ya watu kuendekeza vitendo vya ubakaji na ulawiti katika jamii.

Mshtakiwa aliiomba mahakama kumwachia huru kwa madai ya kutotenda kosa hilo.

Hata hivyo, Hakimu Mkazi Mfawidhi Laizer alimhukumu kifungo cha maisha jela na kuweka wazi haki ya kukata rufani kwa upande usioridhika na hukumu.

## Umoja waendesha guta wapata mkopo pikipiki 6

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

UMOJA wa waendesha pikipiki za magurudumu matatu (Guta) na wamiliki Tanzania (BOTRAMBE), Tawi la Mbeya umepata mkopo wa pikipiki sita zenye thamani ya Sh. milioni 22.2 kutoka Taasisi ya Tulia Trust.

Mkopo huo ulikabidhiwa jana na Meneja wa Taasisi hiyo, Jackline Boaz kwa Makamu Mwenyekiti wa umoja huo, Amani William ili kuwawezesha kujiajiri na kujikwamua kiuchumi.

Jackline alisema, lengo la kutoa mikopo hiyo kwa makundi ya vijana ni kuwainua kiuchumi na kujiajiri wenyewe ili kuondokana na hali ya utegemezi na wakati mwingine kujihusisha na vitendo vya kihalifu.

Dereva bodaboda na mfanyabiashara wa nafaka, Erasto Nzengo, alisema usafiri wa pikipiki ya matairi matatu utamwezesha kuwafikia wateja wake katika maeneo yaliyokuwa hayafikiki kwa wakati na kuongeza wigo wa masoko.

"Lengo langu lilikuwa ni kupata usafiri ambao utanisaidia kusambaza mzigo mkubwa wa nafaka kama unga wa sembe, lishe, mchele kwa wakati, ndoto yangu imetimia nitarejesha mkopo kwa wakati ili wengine wanufaike," alisema Nzengo.

Makamu Mwenyekiti wa umoja huo, Amani William, alisema mkopo huo ni ombi walilopeleka kwa Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini ambaye ni Spika wa Bunge la Tanzania, Dk. Tulia Ackson, baada ya uhitaji.

"Nitoe angalizo kwa vijana ambao wamenufakia na mkopo kuzingatia muda wa marejesho ili kujenga heshima na kuwezesha taasisi hiyo kuendelea kutoa mikopo kwa wahitaji wengine," alisema William.

**"Lengo langu lilikuwa ni kupata usafiri ambao utanisaidia kusambaza mzigo mkubwa wa nafaka kama unga wa sembe, lishe, mchele kwa wakati, ndoto yangu imetimia nitarejesha mkopo kwa wakati ili wengine wanufaike," alisema Nzengo.**



Dereva bodaboda Asumwisye Bakari wa Kata ya Mpuguso wilayani Rungwe akipakia mzigo wa ndizi kwa ajili ya kupeleka soko la Ushirika lililoko wilayani humo jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Waanza ujenzi kituo cha afya kwa kuchangishana

**Na Grace Mwakalinga,** SONGWE

WANANCHI wa Kijiji cha Isangu, Kata ya Hasanga, Wilaya ya Mbozi mkoani Songwe, wameanza ujenzi wa kituo cha afya kwa kuchangishana fedha na nguvu kazi yao baada ya kata hiyo kutokuwa na zahanati wala kituo cha afya.

Kata ya Isangu haina zahanati wala kituo cha afya, matibabu huyapata maeneo mengine ambayo hulazimika kutumia gharama kubwa kufuata huduma.

Nguvu kazi ya ufyatuaji matofali, mchango na shughuli nyingine imefikia thamani ya Sh. milioni 80. Wakizungumza na Nipashe jana, wananchi hao walisema wajawazito wanapata adha kubwa ya kutembea umbali mrefu kufuata huduma za matibabu. Mkazi wa eneo hilo, Lydia Swebe alisema wajawazito wanatumia nauli kuanzia Sh. 5,000 hadi 10,000 kwenda Hospitali ya Mbozi Mission.

"Kutokana na kukosekana kwa kituo cha afya, wananchi tulikubaliana tuanze na nguvu kazi kila mmoja alikubali kutoa chochote ili ujenzi uanze mara moja kunusuru maisha ya mama na mtoto, ujenzi umefikia hatua ya kupaua tunaiomba serikali kuunga mkono juhudi zetu," alisema Swebe.

Alisema hata watoto hukosa huduma za matibabu na watu hupoteza maisha baada ya kushindwa kulipia gharama za usafiri na matibabu.

Mbunge wa Jimbo Mbozi, Japhet Hasunga, alilazimika kutoa mabati 288 yenye thamani ya Sh. milioni 10 yaliyofadhiliwa na Benki ya Biashara nchini TCB.

Meneja wa TPB Kanda, Saimon Mlelwa, alisema walipokea maombi kutoka kwa Mbunge Hasunga kuwapo kwa mahitaji mbalimbali kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa kituo hicho cha afya.

"Kama ulivyo utaratibu wa benki katika sehemu yetu ya faida tunachangia miradi ya maendeleo ya wananchi katika sekta ya afya na elimu, tukaona ni vyema sasa kuchangia mabati 288 yenye thamani ya Sh. milioni 10 na hatutoishia hapo tutaendelea kuunga mkono juhudi za wananchi," alisema Mlelwa.

Mbunge wa Jimbo la Mbozi, Japhet Hasunga, alisema kwa muda mrefu kata hiyo haina kituo cha afya na kupongeza jitihada zilizofanyika na wananchi hao kuanza ujenzi, pia aliahidi wadau na serikali wataendelea kuwaunga mkono.

Diwani wa Kata ya Hasanga, Mirick Nzowa, alisema wananchi hao wanahitaji ujenzi wa kituo hicho kukamilika haraka ili kuokoa maisha ya wananchi wa eneo hilo.

"Tunarajia kituo hiki baada ya kukamilika kitahudumia wananchi 12,000 na kupunguza msongamano wa wagonjwa wanaotibiwa hospitali binafsi ya Mbozi Mission," alisema Nzowa.



# Mpango kuweka jiwe la msingi ujenzi nyumba 3,500

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, leo anatarajiwa kuweka jiwe la msingi mradi wa ujenzi wa nyumba 3,500 za watumishi unaotekelezwa na Wakala wa Majengo nchini (TBA), katika eneo la Nzuguni jijini hapa Dodoma.

Akikagua eneo hilo jana, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, alisema mradi huo mkubwa utaongeza hadhi ya makao makuu ya nchi.

Alitoa wito kwa wananchi kujitokeza kwa wingi kushuhudia tukio hilo na hadi sasa nyumba 150 za awamu ya kwanza kati ya 3,500 zimeshakamilika.

"Dodoma inakua kwa kasi kwa takwimu za sensa mwaka huu inaonekana watu zaidi ya milioni moja wameongezeka ndani ya miaka 10, si jambo dogo maana watu wakiongezeka wanahitaji makazi, hivyo tunapongeza TBA kwa kuliona hili," alisema.

Senyamule alisema nyumba hizo ni kati ya majengo mengi yanayojengwa na TBA Dodoma na nchini.

"Dodoma ya Samia ni fahari ya Watanzania, tunajivunia TBA kwa kufanya uwekezaji huu mkubwa," alisema.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, alisema mradi huo utakapokamilika utatatua tatizo la makazi na kuongeza hadhi ya jiji hilo.

"Napongeza jitihada kubwa zinazofanywa na TBA katika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwa ni pamoja na ujenzi wa nyumba hizo mpya," alisema.

Alipongeza pia TBA kwa kutekeleza mradi wa ujenzi wa nyumba za viongozi eneo la Kisasa kwa ufanisi.

Mtendaji Mkuu wa TBA, Daudi Kondoro, alisema nyumba hizo ni za bei nafuu kuwasaidia kujikimu kimaisha.

"Kumekuwa na changamoto kubwa ya uhaba wa nyumba kwa watumishi wa serikali wanaohamia Dodoma kutokana na idadi yao kuwa ni kubwa kulinganisha na nyumba zilizoko, lakini TBA imeendelea kujitahidi kutatua changamoto hiyo kwa kubuni na kujenga nyumba," alisema.



Wakazi wa Jiji la Dodoma, Mtaa wa Majengo, wakifanya usafi wa kuondoa taka na tope kwenye mfereji unaopitisha maji machafu ili usiziba mvua za msimu zitakapoanza kunyesha, (kulia) Ofisa wa Kitengo cha Idara ya Mazingira, Ally Mfinanga. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Vijana watakiwa kujenga utamaduni wa kujiajiri

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Elimu Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, amewataka vijana kujenga utamaduni wa kubuni na kujiajiri kulingana na walichosomea ili kuisaidia serikali kupunguza kundi la wasio na ajira.

Prof. Mkenda alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki alipokuwa akizindua kituo cha habari cha WazoHuru jijini hapo.

Alisema mpaka sasa serikali imepiga hatua kubwa kuwajengea vijana uwezo wa kujiajiri na uzinduzi wa kituo hicho ni chachu kwa vijana wengine kuona ni namna gani wanaweza kujiajiri na kuajiri wengine.

"Sisi Watanzania tuongeze bidii ya kufurahia mafanikio ya wenzetu, tukiona mwenzetu mwenye ndoto anafanikiwa tunamuunga mkono kwa kumwombea na kumtakia kila la heri na tumekuja hapa na wabunge kuunga mkono jitihada hizi," alisema.

Naye Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhandisi Andrea Kundo, alimpongeza Mtendaji Mkuu wa WazoHuru kwa kuhakikisha anafuata sheria na kanuni za uanzishwaji wa kituo hicho.

Alisema kwa sasa kuna mapinduzi ya teknolojia badala ya kusubiri taarifa kwenye runinga nyumbani, sasa watu wanapata habari hata kwa simu zao za mkononi.

Awali Mkurugenzi wa Wazohuru, alisema mipango yao ni kuwa na vyombo mbalimbali vya habari ili kutoa fursa kwa vijana kupata ajira.

Alisema atahakikisha vyombo hivyo vinafuata misingi na maadili ya uandishi wa habari.

# Tengeru yapatiwa bil. 2.3/- ujenzi bweni la kike

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIKA mwaka wa fedha 2022/2023 serikali imeipatia Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru, Sh. bilioni 2.3 kwa ajili ya ujenzi wa bweni la kike ambalo litasaidia kuondoa kero wanazokabiliana nazo ikiwamo vitendo vya ukabaji.

Mkuu wa Taasisi hiyo, Dk. Bakari George, alibainisha hayo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habri kuhusu utekelezaji majukumu mbalimbali ya taasisi hiyo.

Alisema, wanaishukuru serikali ambayo imeendelea kuipa kipaumble taasisi hiyo ili iweze kujiimarisha na kutoa elimu yenye viwango kwa vijana wa kitanzania.

Dk. George alisema fedha hizo watazitumia katika ujenzi wa bweni hilo kwa wanafunzi wa kike ili kuwasaidia kuondokana na adha mbalimbali walizokuwa wakikabiliana nazo kwa muda mrefu.

Aidha, alisema kutokana na serikali kufungua fursa za kiuchumi nchini kumewezesha wahitimu wa taasisi hiyo kupata ajira katika kampuni ya biashara na mashirika yasiyo ya kiserikali na kupunguza kero ya ajira iliyokuwapo awali.

"Serikali ya awamu ya sita imesaidia upanuzi wa fursa mbalimbali za mikopo ya kutoka sekta binafsi na kuwezesha wahitimu kujikwamua kiuchumi," alisisitiza.

Akieleza mwelekeo wa taasisi hiyo, Dk. George alisema kwa mwaka 2022/2023 inatarajia kuongeza programu sita za mafunzo zitakazoanza kutolewa dirisha la Machi 2023 ambazo zimezingatia mahitaji ya soko la ajira kwa sasa na umuhimu wa kuandaa wahitimu wenye fikra sahihi na uwezo wa kujiajiri.

Taasisi hiyo inaendesha programu 15 za mafunzo na mitaala inayotolewa imezingatia uwiano kati ya nadharia na vitendo.

Kadhalika, alisema ongezeko la udahili wa wanafunzi katika taasisi hiyo linachagizwa na uwekezaji mkubwa uliofanywa na serikali katika uimarishaji wa elimu kwa ngazi za msingi na sekondari na umuhimu wa fani ya maendeleo ya jamii katika muktadha wa upatikanaji wa ajira.

Hata hivyo, Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, alisema kuwa kwa kutambua umuhimu wa sekta hiyo tayari imeajiri maofisa maendeleo ya jamii 3,000 huku mahitaji yakiwa ni zaidi ya 5,000.





## Wakulima watakiwa kutunza miundombinu ya umwagiliaji

**Na Mwandishi Wetu**

WAKULIMA wa Bonde la Mlemele Mkoa wa Kusini Pemba wametakiwa kuitunza miundombinu iliyoko katika bwawa linalotumika kwa umwagiliaji.

Mratibu wa Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji, Jokha Salim Moh'd, alitoa rai hiyo jana wakati akifungua mafunzo ya uzalishaji, uendeshaji na matengenezo ya miundombinu ya umwagiliaji kwa kamati na wakulima viongozi wa bonde hilo.

Alisema serikali imetumia zaidi ya Sh. bilioni nane kujenga bwawa hilo kwa lengo la kuwasaidia wananchi wake, hivyo ni vyema wananchi hao kuheshimu na kuthamini jitihada hizo za serikali.

"Kamati mna jukumu la kuitunza na kuilinda miundombinu ambayo ipo kwenye bwawa lakini pia iliyopo kwenye bonde ili itumike vizuri kama serikali ilivyokusudia," aliagiza.

Mratibu huyo pia aliitaka kamati hiyo kushirikiana na Idara ya Umwagiliaji kufanya ukarabati mdogo pindi uharibifu utakapotokea katika miundombinu hiyo.

Mkufunzi wa Mafunzo hayo, Ali Said ambaye ni Ofisa Mipango Idara ya Umwagiliaji Pemba, aliwataka wakulima hao kulima kilimo bora kwa kuanza utayarishaji mzuri wa kitalu na kutumia mbegu bora.

"Wakulima ambao mmefaidika na kilimo, itumieni fursa hii kulima kilimo bora na kwa kutumia mbegu bora na si za kubahatisha," aliagiza.

Wajumbe wa Kamati wa Bonde hilo waliwataka wakulima kuhakikisha hawabezi jitihada ambazo zimefanywa na serikali yao kwa kuongeza ulinzi wa miundombinu ambayo ipo katika bonde hilo ili itumike kwa muda mrefu.

Jumla ya wakulima wa mpunga 375 watanufaika na mradi huo ambao umetekelezwa na serikali ya Zanzibar.

# Z'bar kuzalisha umeme wake

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

ZANZIBAR inatarajia kuwa na chanzo chake cha umeme ambacho kitakuwa na uwezo wa kuzalisha MW 18 za umeme wa jua.

Waziri wa Maji, Nishati na Madini, Hassan Kaduara, alibainisha hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio ya wizara yake katika miaka miwili ya uongozi wa Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Alisema Shirika la Umeme Zanzibar limepata mafanikio makubwa ambapo hivi karibuni litakuwa na mradi mpya wa uzalishaji wa umeme wa jua na pia kuwa na vituo viwili vya kupozea umeme.

Alisema miongoni mwa mafanikio ya shirika hilo ni kuwapunguzia gharama wananchi wanaounga huduma hiyo ambapo awali wananchi waligharamika kulipia nguzo moja Sh. milioni 1.7 lakini kwa sasa wanapatiwa bila ya malipo.

Alisema mwamko wa wananchi kuunga nishati ya umeme umeongezeka na kwa mwaka huu kuna wateja wapya zaidi ya 18,000.

Alisema Shirika la Umeme linaagiza nguzo hizo kutoka mkoani Iringa na Afrika Kusini lakini mikakati yao ni kuwa na nguzo za saruji ili kupunguza ukataji wa miti kwa kuwa nguzo wanazoagiza ni za miti.

Alisema nguzo hizo mbadala zitasaidia kuhifadhi mazingira na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabinachi.

Akizungumzia kuhusu huduma ya majisafi na salama, waziri huyo alisema sekta ya maji imepewa kipaumbele, ikiwa ni sehemu ya mikakati ya utekelezaji wa ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020-2025 ambayo lengo lake ni kuona huduma hiyo inawafikia wananchi pamoja na kusaidia sekta ya kilimo.

Waziri huyo alisema kwa sasa serikali iko katika hatua za mwisho za kukamilisha mradi wa Exim Benki ambao unajenga jumla ya matangi 10 ya chini ya ardhi yenye uwezo wa kuzalisha maji lita milioni 32. Mradi huo unajumuisha kujenga jumla ya visima vya maji 14 katika maeneo mbalimbali ikiwamo Kiembesamaki na Kidutani Unguja ambako kwa sasa kazi za ulazaji wa mabomba zinaendelea.

Alisema mradi huo ambao unatarajiwa kukamilika mwanzoni mwa mwaka ujao utayanufaisha maeneo ya Maungani ambako pia litajengwa tangi la kuhifadhi maji chini ya ardhi lenye uwezo wa lita milioni 1.5 na kufaidisha maeneo mengi ya Mkoa wa Mjini Magharib Unguja.

Alisema serikali kupitia fedha za UVIKO-19 imetenga jumla ya Sh. bilioni 34 kwa ajili ya upatikanaji wa huduma za majisafi na salama ambao pia unahusisha ujenzi wa matangi na ununuaji wa mita za kisasa kwa ajili ya kuwawezesha wananchi na wawekezaji kulipia huduma ya majisafi na salama.

Aliwataka wananchi kuchangia huduma ya majisafi na salama ambapo kwa sasa mamlaka ya majisafi (ZAWA) kupitia fedha za UVIKO- 19 imetenga fedha na kununua mita ambazo zitatumika kwa ajili ya kurekodi matumizi sahihi ya maji kwa wananchi na wawekezaji.



Kombo Hamad, mfanyabiashara wa soko la Darajani mjini Unguja anayeuza samaki wakavu akionyesha pweza mkavu. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Tani 8,700 za karafuu zanunuliwa mwaka 1

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SHIRIKA la Biashara la Taifa Zanzibar (ZSTC) limesema kwa kipindi cha mwaka 2021/22 limenunua tani 8,738 za karafuu, Sh. bilioni 114.1 zikitumika.

Meneja Uhusiano wa Shirika hilo, Ali Mohammed Ali, alibainisha hayo jana wakati akizungumza na Nipashe ofisini kwake Maisara mjini Zanzibar.


Alisema kiwango cha karafuu walichonunua kwa mwaka huu ni kikubwa kulinganishwa na misimu miwili iliyopita, akibainisha kuwa kwa mwaka 2020/2021, ZSTC ilinunua tani 213 na mwaka 2019/2020 shirika hilo lilinunua tani 4,497 kwa shilingi bilioni 62.9. Akizungumzia mauzo ya zao hilo la kibiashara nje ya nchi, ofisa huyo alisema katika msimu wa mwaka 2021/22, ZSTC imeuza nje ya nchi zaidi ya tani 8,322, ambazo ziliingiza dola milioni 62.46 ambazo ni sawa na Sh. bilioni 144.915.

Alisema kuwa katika msimu wa mwaka 2020/21, waliuza nje ya nchi tani 260.6 zilizoingiza zaidi ya dola 1,287,120 ambazo ni sawa na Sh. bilioni 2.947 na mwaka 2019/20 waliuza nje ya nchi tani 5,005.7 kwa dola 23,850,704.

Ofisa huyo alitumia fursa hiyo kuwataka wakulima kutodharau zao hilo na kwa kuwa ni muhimu sana kwa uchumi wa nchi, pia lina tija ya kumpatia kipato mkulima. "Ninawashauri wakulima wapanue kilimo cha zao hili, wasipuuze hasa ikizingatiwa kuwa linamwezesha mkulima kupata kipato na nchi kuingiza fedha nyingi za kigeni," alisema.

Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Shamata Shaame Khamis, alisema wizara yake ina mipango na mikakati ya kuhakikisha uzalishaji wa zao hilo unaongezeka nchini.

Alisema zao la karafuu lina historia ya kipekee kwa visiwa vya Zanzibar na limekuwa muhimu kwa uchumi, hivyo atasimamia mikakati iliyoko ya kuongeza uzalishaji na kuinua zaidi mapato ya nchi.



# RC ataka mbinu kuyakabili magonjwa yasiyoambukiza

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Adam Malima, amewahimiza wataalamu kutoka Wizara ya Afya kutoa elimu na mbinu saidizi kwa wananchi katika kujikinga na magonjwa yasiyoambukiza.

Hatua hiyo inakuja kutokana na kuongezeka kwa kasi magonjwa yasiyoambukiza na kuwa tishio katika jamii ya Watanzania na ulimwenguni kote, yakisababisha vifo vingi kulinganishwa na yanayoambukiza.

Malima alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho ya kukabiliana na magonjwa hayo yanayofanyika kitaifa jijini hapo.

Alisema magonjwa yasiyoambukiza yana madhara kimaisha, kiuchumi, kiafya, kijamii na kusababisha vifo vya mapema kwa watu wengi, hivyo wataalamu wa afya watumie maadhimisho ya mwaka huu kutoa elimu na mbinu kwa wananchi kuyaepuka na kuyakabili magonjwa hayo.

Malima alisema magonjwa yasiyoambukiza athari zake katika mfumo wa maisha na kiuchumi ni kubwa kwa kuwa mapato ya mtu yanatumika kugharamia matibabu, pia mwili huathirika.

Mkuu wa Mkoa huyo alisema suluhisho la ukubwa wa gharama hizo za matibabu ni kupima afya mapema na kupuuza misemo kuwa kupima ni kumchokoza Mungu.

Alionywa kuwa watu wasiofanya mazoezi na ulaji usiofaa wako hatarini zaidi kwa afya zao kwa kuwa wako karibu na chanzo cha kupata magonjwa yasiyoambukiza kama matatizo ya moyo, shinikizo la juu la damu, mafuta mengi, kisukari, saratani na uzito uliopitiliza.

Meneja wa Mradi wa Shirikisho la Magonjwa Yasiyoambukiza (TANCDA), Dk. Happy Nchimbi, alisema wakati maadhimisho ya kitaifa ya kuzuia na kudhibiti magonjwa yasiyoambukiza yanafanyika, takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO) zinaonyesha magonjwa hayo yanaongezeka duniani kote na kuathiri nyanja zote kimaisha, kiuchumi, kiafya na kijamii.

"Takwimu za WHO za mwaka 2016 zinaonyesha magonjwa hayo ya shinikizo la juu la damu, kisukari, saratani, pumu, magonjwa ya afya ya akili na selimundu yanachangia zaidi ya vifo milioni 41, sawa na asilimia 71 ya vifo vyote (milioni 57 vilivyotokea katika mwaka huo)," alisema.

Akiwa Arusha, Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, alisema kwa Tanzania, magonjwa yasiyoambukiza kwenye jamii yamekuwa na ongezeko kubwa, akibainisha kuwakumba watu 800,000 kwa kipindi cha kati ya mwaka 2018 hadi 2020.

"Mwaka 2020 waliongezeka hadi kufikia 4,795,827 na inakadiriwa wagonjwa wenye shinikizo la juu la damu ni asilimia 26, zaidi ya asilimia 90 ya wagonjwa hao hawatumii dawa zozote," alisema.

Alibainisha kuwa utafiti uliofanyika nchini mwaka 2018, ulibaini watu wazima milioni 2.6 sawa na asilimia 8.7 wanatumia tumbaku na utafiti mwingine wa mwaka 2012 ulibaini matumizi ya pombe kupita kiasi (asilimia 29.3) na asilimia 34.7 ya watu wana unene uliopitiliza.

Alisema takwimu za Shirika la Maendeleo Duniani (UNDP) zinabashiri miaka 20 tangu mwaka 2013 gharama zitokanazo na magonjwa hayo zitafikia dola za Marekani trilioni 47, fedha ambazo zingeweza kupunguza umaskini kwa watu bilioni 2.5 kwa miaka 50.



Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Adam Malima, akipokea kitabu cha historia ya siasa ya Tanzania na viongozi wake kwa Spika mstaafu, Pius Msekwa, alipotembelea nyumbani kwake Ukerewe kwa ajili ya kumjulia hali. Kitabu hicho kiitwacho 50 Years of Independence, A Concise Political History of Tanzania kimeandikwa na Pius Msekwa. **PICHA: VITUS AUDAX**

# Wananchi wapewa pembejeo za kilimo

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANANCHI wa Kijiji cha Bushora, Kata ya Mwamalili, Manispaa ya Shinyanga wamepatiwa msaada wa pembejeo za kilimo ambazo ni mbegu za mahindi na majembe kwa ajili ya kuimarisha kilimo katika msimu wa mwaka 2022/23.

Pembejeo hizo za kilimo ziligawiwa juzi na Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko kupitia hafla ya utoaji wa pembejeo iliyoandaliwa na Jeshi la Jadi (Sungusungu) katika kijiji hicho kwa lengo la kuimarisha kilimo na kupunguza kasi ya vitendo vya uhalifu.

Mboneko, akizungumza kwenye ugawaji wa pembejeo hizo za kilimo, aliwataka wananchi wa kijiji hicho wafuate ushauri wa wataalamu wa kilimo kwa kulima kilimo cha kisasa ambacho kitawapatia mavuno mengi.

"Ninaombeni wananchi kulingana na hali ya hewa, tufuate ushauri wa wataalamu wetu wa kilimo kwa kulima mazao ya muda mfupi ili tupate chakula," alisema Mboneko.

Awali akisoma risala wakati wa ugawaji wa jembejeo hizo za kilimo, Katibu wa Jeshi la Jadi (Sungusungu) katika kijiji hicho cha Bushora, Sebastian Salamba alisema kijiji kina jumla ya kaya 350 na kila kaya imepewa mbegu za mahindi mifuko miwili na majembe mawili.

Alisema Sungusungu wametoa pembejeo hizo za kilimo kwa wananchi ili wasikwame kufanya shughuli za kilimo katika msimu wa mwaka huu 2022/23 kutokana na hali ya ugumu wa maisha ambayo wanakabiliana nayo kwa sasa.

Baadhi ya wananchi waliopata pembejeo hizo za kilimo waliahidi kufuata ushauri wa wataalamu ili kulima kisasa na kupata mavuno mengi, hali ambayo itawasaidia kukabiliana na uhaba wa chakula.

# Ulinzi wa hifadhi za misitu kuimarishwa

**Na Vitus Audax,** MAGU

MKUU wa Wilaya ya Magu, Salum Kali, amesema serikali kwa kushirikiana na Jeshi la Akiba itaendelea kuimarisha ulinzi katika hifadhi za misitu wilayani humo ili kukabiliana na uharibifu wa mazingira unaofanywa kutokana na shughuli za kibinadamu na kuathiri uoto wa asili unaoanza kupotea katika wilaya hiyo.

Kali alitoa kauli hiyo juzi wakati akihitimisha mafunzo ya awali ya Jeshi la Akiba katika Tarafa ya Ndagalu wilayani hapo, akisisitiza kuwa kupitia jeshi hilo, wataweka kambi katika Msitu wa Sayawa na maeneo mengine ili kuyalinda dhidi ya shughuli za kibinadamu zinazoharibu mazingira.

Alisema jeshi hilo litalinda hifadhi za misitu zilizoko katika wilaya hiyo kwa kuwa inachangia hali nzuri ya hewa ikiwa ni pamoja na kuwa chanzo cha mvua.

Aliwataka kujiandaa kisaikolojia kufanya kambi ya muda mrefu katika hifadhi hiyo ambayo pia wataitumia katika mazoezi na mafunzo mengine ya ukakamavu na uzalendo huku akiwaahidi kuwaandalia fungu kwa ajili ya posho na fedha za kujikimu kutoka katika mfuko wake ili wahakikishe wanafanya kazi hiyo kwa weledi.

Kali pia aliliagiza jeshi hilo kuhakikisha linapambana na vitendo vya rushwa, ujauzito kwa wanafunzi na vitendo vya kikatili dhidi ya watoto na wanawake kwa kuwafikisha watu wanaojihusisha na vitendo hivyo katika vyombo vya sheria.

Baadhi ya wahitimu wa mafunzo hayo waliahidi kupambana na vitendo vya uharibifu wa mazingira na kuimarisha amani na utulivu katika wilaya.

Erasto Thomas, mhitimu wa mafunzo hayo, alisema kuwa kupitia mafunzo hayo, wamejifunza ukakamavu na uzalendo huku akiahidi kutumia weledi wake katika kuisaidia jamii dhidi ya vitendo vya uvunjifu wa amani.

Akihitimisha mafunzo hayo, Ofisa Mteule Daraja la Kwanza kutoka Jeshi la Wananchi wa Tanzania, Thobias Charles, ambaye ni mshauri wa Jeshi la Akiba Wilaya ya Magu, alisema jeshi hilo limepokea mafunzo ya ukakamavu, utimamu, matumizi ya silaha na mabomu ya kurushwa, vyote hivyo ni kwa ajili ya kushiriki kikamilifu katika ulinzi na usalama wa raia na mali zao kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi wilayani humo.

Askari 62 wamehitimu mafunzo ya awali ya Jeshi la Akiba katika Wilaya ya Magu huku wakisisitizwa kuwa na nidhamu na utii kwa serikali na Watanzania kwa kusimamia kulinda na kutunza amani na utulivu.

## HABARI KIMATAIFA

# Uganda yapiga marufuku matumizi vipimo vya RDT

**Na Maulid Mmbaga**

WIZARA ya Afya ya Uganda (MoH) imesema vipimo vya uchunguzi wa haraka (RDT) vinavyotumika kupima virusi vya ebola katika masoko na baadhi ya vituo vya afya vya binafsi havikuidhinishwa.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi Mkuu wa Huduma za Afya nchini humu, Dk. Henry Mwebesa, kitendo hicho ni haramu na hatari kwasababu kinafichua umma kwa ujumla na wafanyakazi wa afya katika hatari ya kuambukizwa.

"Shirika la Afya Duniani (WHO) halijawahi kuidhinisha matumizi ya RDTs kuthibitisha ugojwa wa ebola. Kipimo cha Haraka cha (PCR) ndiyo njia pekee ya kupima iliyoidhinishwa na inafanywa ndani ya maabara za serikali bila malipo katika Taasisi ya Utafiti wa Virusi vya Uganda (UVRI).

"Sehemu nyingine ni katika Maabara Kuu ya Afya ya Umma (CPHL) inayohamishika katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mubende, pia taarifa hiyo tumeitumia kuutaarifu umma kwa ujumla kuwa upimaji wa ebola na usimamizi wa mgonjwa unazuiliwa kwa vituo vilivyoteuliwa vya serikali," alisema Mwebesa.

Aliongeza kuwa, utaratibu huo umewekwa kutokana na hatari kubwa inayoletwa na virusi vinavyoambukiza sana na kwasababu ya kiwango cha juu cha vifo.

Aidha, alieleza kuwa kizuizi cha upimaji na usimamizi wa kesi za ebola kinafaa kwa mahitaji ya vifaa maalum vya usalama na kwamba hatua za kuzuia hazipatikani katika vituo vya afya vya kibinafsi.

Hata hivyo, alisema suala hilo pia linahitaji wataalamu waliofunzwa vizuri na kujua njia sahihi za kinga na SOPS.

"Wizara ya Afya inahimiza vituo vya afya vya umma na vya kibinafsi kuripoti lolote ikiwamo mshukiwa wa ebola katika vituo vya afya vya umma vilivyo karibu au awasiliane na simu ya dharura bila malipo laini 0800100066," alisema Mwebesa.

Pia alisisitiza kwamba utaratibu huo utasaidia MoH kutenga, kupima na kutibu kesi zilizothibitishwa na kufuatilia mawasiliano yao ili kuzuia maambukizi zaidi ya virusi vya ebola nchini humo.



Rais wa Rwanda, Paul Kagame, João Lourenço wa Angola na Félix Tshisekedi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) wakiwa pamoja baada ya mkutano wa pande tatu uliofanyika juzi mjini Luanda, ukilenga kurejesha hali ya kuaminiana kati ya DRC na Rwanda. **PICHA: RFI**

# UN yatoa onyo kuzorota juhudi kulinda mazingira

**SHARM EL-SHEIKH,** MISRI

KATIBU Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Antonio Guterres, ametoa onyo kuhusu kulegea kwa juhudi za kulinda mazingira ya dunia, baada ya kufunguliwa rasmi kwa mkutano wa kimataifa wa mazingira nchini Misri, akieleza kwamba sayari inaomba msaada.

Umoja wa Mataifa umetoa ripoti inayoonyesha kuwa miaka minane iliyopita ndiyo ilikuwa ya joto kali zaidi kuwahi kurekodiwa, kukiwa na ongezeko la kasi ya kupanda kwa kina cha bahari, kuyeyuka kwa barafu, mawimbi ya joto na viashiria vingine vya tabianchi.

Shirika la Hali ya Hewa na Tabianchi la UN, lilisema shabaha ya kupunguza ongezeko la joto hadi nyuzi 1.5 za celsius inazidi kuwa ngumu kufikiwa.

"Kuongezeka kwa mawimbi ya joto, kuyeyuka kwa barafu na mvua za masika kumesababisha ongezeko la majanga ya asili," lilisema Shirika la Hali ya Hewa la Umoja wa Mataifa wakati wa ufunguzi wa mkutano wa COP27 katika mji wa mapumziko wa Sharm el-Sheikh nchini Misri.

Guterress, alisema sayari inatuma ujumbe wa dhiki, huku akiitaja ripoti hiyo kama historia ya machafuko ya hali ya hewa.

"Tunapaswa kujibu ishara ya dhiki ya sayari kwa kuchukua hatua pana na za kuaminika za kimazingira, COP27 lazima pawe ndiyo mahala pa kuchukuwa hatua hizo na huu sasa ndiyo unapaswa kuwa wakati," alisema Guterres.

Pia alisema katika muda wa miezi michache iliyopita, mafuriko yameacha madhara makubwa nchini Pakistan na Nigeria, akieleza kuwa hali ya ukame imezidi kuwa mbaya barani Afrika na Marekani na kwamba vimbunga viliacha uharibifu katika kanda ya Carribbean na mawimbi ya joto yameyakumba mabara matatu.

Mkutano huo unakuja pia katika wakati ambapo dunia inashuhudia vita vya uvamizi vya Urusi dhidi ya Ukraine, mzozo wa nishati, mfumuko wa bei unaozidi na athari zinazoendelea za janga la virusi vya corona.

**MABADILIKO YA NYAKATI**

Simon Stiell, Katibu Mkuu wa Shirika la Mabadiliko ya Tabianchi la UN, alisema hatokuwa msimamizi wa kile alichokiita kurejea nyuma katika utekelezaji wa malengo ya kupunguza utoaji wa gesi chafuzi kwa asilimia 45 kufikia mwaka 2030, ili kubakisha joto la dunia kwa nyuzi 1.5 za celsius, juu ya viwango vya mwishoni mwa karne ya 19.

"Leo inaanza enzi mpya na tunaanza kufanya mambo kwa tofauti, Paris ilitupa makubaliano, Katowice na Glasgow zilitupa mpango, Sharm El-Sheikh inatuhamishia kwenye utekelezaji, hakuna anayeweza kuwa abiria tu kwenye safari hii, hii ndiyo ishara kwamba nyakati zimebadilika," alisema.

Mkutano wa COP27 utajikita kwenye fedha, suala kuu ambalo limevuruga uhusiano kati ya mataifa yaliyotajirika kupitia kuchoma mafuta ya kuchimbwa ardhini, na yale maskini yanayoteseka kutokana na madhara mabaya zaidi ya mabadiliko ya tabianchi. **DW**

## Wahofia kukoma jitihada kuzuia unyanyasaji wafanyakazi wa kigeni

**DOHA,** QATAR

MASHIRIKA ya kutetea haki za binadamu yamehofia kwamba dirisha la kushughulikia unyanyasaji mkubwa wa wafanyakazi wa kigeni linaweza kufungwa hivi karibuni, zikiwa zimesalia siku chache tuu kabla ya Qatar kuandaa Kombe la Dunia.

Ilielezwa kuwa muda mrefu wa maandalizi ya Kombe la Dunia la mwezi huu umeleta hali ya uchunguzi ambayo haikuwa imeshuhudiwa awali, kuhusu jinsi gani mamilioni ya wafanyakazi wa kigeni katika taifa la Uarabuni ambao walijenga viwanja na miundombinu mingine, na ambao watafanya kazi kwenye hoteli na kufagia barabara wakati wa michuano hiyo mikubwa zaidi ya michezo ulimwenguni.

Kutokana na ukosoaji mkubwa wa kimataifa, Qatar ilipitisha mageuzi kadhaa katika miaka ya hivi karibuni, ikiwa ni pamoja na kuvunjwa kwa kiasi fulani sehemu ya mfumo uliowafunga wafanyakazi kwa waajiri wao na kuweka kima cha chini cha mshahara, mabadiliko yaliyosifiwa na Umoja wa Mataifa (UN) pamoja na makundi ya haki za binadamu.

Hata hivyo, wanaharakati walidai kuwa unyanyasaji kuanzia mishahara isiyolipwa hadi mazingira magumu ya kazi katika mojawapo ya nchi zenye joto kali duniani, bado umeenea, na kwamba wafanyakazi ambao wamezuiwa kuunda vyama vyao au kugoma wana njia chache za uhakika za kufuata haki.

Pia inaelezwa kuwa wana wasiwasi kuhusu kitakachotokea baada ya mashindano hayo ya mwezi mzima kukamilika mwezi Desemba, wakati uangalizi wa kimataifa utakapoondoka na waajiri kupunguza mishahara yao.

Qatar ilisema inaongoza kanda hiyo katika mageuzi ya ajira na kwamba mabadiliko hayo yataendelea baada ya Kombe la Dunia. Maofisa kutoka kwa Emiri mkuu anayetawala hadi chini waliwasema wakosoaji, wakiwashutumu kwa kupuuza mageuzi hayo na kulitenga isivyo haki taifa hilo la kwanza la Kiarabu au Kiislamu kuandaa kombe hilo. **VOA**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**FRANK LEONARD** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1022-0039** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia KAMBANGWA SECONDARY SCHOOL mwaka 2003. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA : **CD/IR/RB/8006/2016**

## KUPOTEA KWA CHETI



**USRA .A. HUSSEIN** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1197-0080** kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia GREEN ACRES SEKONDARI mwaka 2014. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha Polisi.
Taarifa ya Polisi: **WMB/RB/437/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**LAMECK OBED NKAMBI** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **HAOJUE** yenye namba za usajili **MC 244 DGZ.** Engine no. **152 fmi – a *a3r006490*.** Chassis no. **1c6pcjbj3n0031912.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi: **DOD/BAH/RB/251280/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**DAVID TUKUNDONDA CHAULA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili namba: **T508 DLL.** kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: **IRI/IRI/RB/425772**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MPWAPWA.**

**TAARIFA KWA UMMA.**


**KUPOTEA KWA KITABU CHA ANIMAL HEALTH LIVESTOCK MOVEMENT PERMIT.**

LAURIANUS PASCHAL NKUHI mwenye namba ya simu 0628673292 Anatangaza kupotelewa na Kitabu cha Animal Health Livestock Movement Permit chenye namba ya Usajili **00807851** Hadi **00807900** mali ya **WIZARA YA MIFUGO.**

Kurasa zilizotumika ni kuanzia namba **00807851** hadi **00807869** na kurasa ambazo hazijatumika ni kuanzia **00807870** hadi **00807900.**

Kwa yeyote atakayekiona kitabu hiki atoe taarifa kituo cha police.

**TAARIFA YA POLISI DOM/MPW/RB/270278/2022.**



Incorporation No: 121475

EXTRACT OF THE BOARD'S SPECIAL RESOLUTIONS
*At the meeting of the Members of ZENNET HR AND FINANCE SERVICESLIMITED Called and held at their registered office on The 18 day ofAugust 2021.*

Agenda:
1. Pass a resolution for Members Voluntary Winding Up.
2. Declaration of solvency of the company
3. Appointment of a Liquidator

**RESOLVED THAT** the Members of the Company have reached a consensus to voluntarily cease operation and wind up the company.

**RESOLVED FURTHER THAT**the Board of Directors have made a pragmatic assessment of the of the affairs of the company and have reasonable grounds to form the opinion that the company will be able to pay its debts in full.

**RESOLVED FURTHER THAT**the Declaration of Solvency is hereby considered and approved and all the directors of the company be and are hereby authorised to sign the declaration and to file the same with the Registrar of Companies.

**RESOLVED FURTHER THAT** Mr EMMANUEL WILLIAM KESSY of Makoa Law Chambers (Advocates) PSSSF Twin Tower Building, Mission Street, P.O. Box 71393 Dar es Salaam the appointed liquidator of the company is hereby authorised to do all such acts, deeds and things as may be required to implement the above said decision of the Board.

**IT WAS UNANIMOUSLY RESOLVED** as forestated.

It is hereby certified by the undersigned, duly passed the foregoing Resolution on ....10th........August 2021 and is true extract of the resolution in consonance with the Memorandum and Articles of Association of the Company and the Companies Act; therefore, certified as true extract of the resolution.

(Name)
Chairperson

P. O. Box 11008 DAR ES SALAAM TANZANIA

(Name)
Secretary

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042,**
**DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**




TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# DIMPOZ AMSHUKURU KIKWETE

**Na Mwandishi Wetu**

MSANII wa Bongo Fleva, Omar Nyembo maarufu Ommy Dimpoz, ameeleza jinsi alivyopata msamaha wa matibabu baada ya kuzungumza kwa simu ya video na Rais mstaafu wa Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete.

Dimpoz ametoa ushuhuda huo usiku wa kuamkia juzi katika hafla ya uzinduzi wa albamu yake ya Dedication, ikiwa ni ya kwanza kuitoa tangu kuanza muziki miaka kumi iliyopita.

Akielezea ilivyokuwa, Dimpoz alisema wakati yupo kwenye matibabu mwaka 2018, rais huyo mstaafu alikuwa akimfuatilia mara kwa mara hali yake na siku moja alimpigia video call akiwa na madaktari ambao walitaka kujua ni nani aliyekuwa akizungumza naye na kuhisi kuwa ni baba yake.

"Niliwajibu ndio ni baba yangu lakini ndio rais wa Tanzania, wakaniuliza wewe ni mtu maarufu huko kwenu?

"Nikawaambia waka-google kunijua zaidi na wakaona nyimbo zangu kuanzia pale wakawa wanaambizana wenyewe kwa wenyewe kuwa mimi ni maarufu na wakawa wanaimba baadhi ya nyimbo zangu.

"Kama haitoshi kuna vipimo vya mapafu nilitakiwa kufanyiwa na ilihitajika euro 25,000 daktari wa pale aliagiza nisamehewe yote haya yote ni kwa ajili ya wewe baba yangu Jakaya Kikwete," alisema Dimpoz.

Kwa upande wa Kikwete aliyekuwa mgeni rasmi katika uzinduzi huo, amempongeza Dimpoz kwa hatua ya kuja na albamu hiyo na kukumbushia changamoto za maradhi alizozipitia kuwa hakuna aliyejua kuwa angerudi tena kuimba.

# IZZO BIZNESS AMPOTEZA SHANGAZI AJALI YA NDEGE

**Na Mwandishi Wetu**



MSANII wa Hip Hop, Izzo Bizness, ameshea taarifa ya kumpoteza shangazi yake kwenye ajali ya ndege ya abiria ya Kampuni ya Precision Air.

Ndege hiyo ilianguka Jumapili asubuhi kwenye Ziwa Victoria mkoani Kagera na kusababisha vifo vya watu 19 na wengine 26 kuokolewa na wavuvi.

Izzo Bizness ameshea ujumbe huu kwenye ukurasa wake wa Twitter akiandika "Shangazi yangu amefariki kwenye ajali ya ndege iliyotokea leo (juzi)".

Ndege hiyo ilikuwa na jumla ya watu 45 japo taarifa ya awali ilisema ina watu 43, miili iliyopatikana 19 na waliookolewa ni watu 26.

# RADO AMJIA JUU BABA LEVO

**Na Mwandishi Wetu**

MSANII wa Bongo Muvi, Rado, ameonyesha kukerwa na kauli ya Baba Levo ya kusema wasanii wa tasnia hiyo ni manyumbu na unaweza



ukawaita hata 300 ukawapa elfu 30 na wasiseme jambo lolote.

Baada ya kauli hiyo wasanii wa Bongo Muvi wamekuja juu sana mmojawao akiwa ni Rado na kusema kuwa Baba Levo amekosea sana kutoa kauli hiyo kama angekuwa anamsema mtu mmoja bora angemtaja tu ila si kutaja tasnia nzima.

Rado ameongeza kuwa tasnia ya Bongo Muvi imejaa watu wengi sana wa heshima.

Rado ameenda mbali sana akimuonya Diamond kuwa makini na watu anaowaajiri waheshimu brand ya media yake.

Rado ameongeza kuwa ili Baba Levo awe salama lazima aombe msamaha juu ya kauli hiyo.

# 'DABI' LIGI KUU SIMBA QUEENS, YANGA PRINCESS DESEMBA 16

**Na Adam Fungamwango**

LIGI Kuu ya Soka ya Wanawake Tanzania Bara msimu huu wa 2022/23, inatarajiwa kuanza Desemba 5, huku 'dabi' ya watani wa jadi, Simba Queens na Yanga Princess wakitarajiwa kupambana Desemba 16, mwaka huu.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa na Shirikisho la Soka nchini (TFF), Mabingwa Watetezi, Simba Queens, watakata utepe wa msimu mpya wa ligi hiyo Desemba 5 watakapocheza dhidi ya JKT Queens kwenye Uwanja wa Mo Simba Arena, Bunju, Dar es Salaam, huku Yanga Princess ikianza ligi siku inayofuata katika Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam dhidi ya Fountain Gate Princess.

Siku hiyo hiyo kwenye Uwanja wa Ilulu Lindi, Amani Queens itaikaribisha Baobab Queens, Alliance Girls itakuwa Uwanja wa Nyamagana kucheza dhidi ya Ciassia Queens, wakati The Tigers Queens na Mkwawa Queens zitakipiga kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid.

Raundi ya pili ya ligi hiyo kwa mujibu wa ratiba hiyo, itaanza Desemba 9 wakati The Tigers Queens itaikaribisha Simba Queens kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha, Alliance Girls itakuwa nyumbani, Nyamagana kuipokea JKT Queens, wenyeji Boabab Queens watakuwa Jamhuri Dodoma kuikaribisha Ciassia Queens, Yanga Princess itakuwa Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam kucheza dhidi ya Mkwawa Queens na Amani Queens itacheza na Fountain Gate Princess kwenye Uwanja wa Ilulu.

Desemba 16, mwaka huu Simba Queens itacheza dhidi ya Yanga Princess, lakini mpaka sasa uwanja bado haujajulikana, na unatarajiwa kutangazwa baadaye.

## BABA NA MWANA!...



Mchezaji wa Timu ya NSSF Veterani, Hamis Msumi, akiwatoka wachezaji wa timu ya vijana wanaolelewa na Kituo cha Michezo cha Jakaya Kikwete, wakati wakicheza mechi ya kirafiki jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Polisi Tanzania yageukia usajili

**Adam Fungamwango na Hadija Mngwai**

BAADA ya kuchapwa bao 1-0 dhidi ya Singida United juzi kwenye Uwanja wa Black Rhino, Karatu, Arusha, na kuifanya timu hiyo kuendelea na mlolongo wake wa kufanya vibaya msimu huu wa Ligi Kuu 2022/23, klabu ya Polisi Tanzania imesema kwa sasa inasubiri dirisha dogo la usajili ili kufanya marekebisho ya kikosi chake.

Licha ya kuliondoa benchi lake la ufundi lililokuwa likiongozwa na Mrundi Joslin Sharif na sasa kuwa chini ya John Tamba ambaye anakaimu nafasi hiyo, bado timu hiyo imeendelea kufanya vibaya kwa kushindwa kupata ushindi mechi tatu mfululizo, tangu ilipoifunga Namungo bao 1-0, Oktoba 19, mwaka huu.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Frank Lukwaro, amesema bado hawajakata tamaa na timu yao na kwamba kwa sasa imebadilika tofauti na mwanzo kabla ya kuliondoa benchi la ufundi.

**"Kwa sasa timu imebadilika, inashambulia sana tofauti na mwanzo, tatizo kubwa ni kushindwa kutumia nafasi, lakini kwa bahati nzuri tunakwenda sasa kwenye kip indi cha usajili, tutakitumia kwa kuziba nafasi zote am bazo tunaziona zina mata tizo, hasa sehemu ya ushambuliaji," alisema.**

Bao pekee la Singida Big Stars lililoizima Polisi Tanzania, lilifungwa dakika ya 23 na straika wa zamani wa Simba, Meddie Kagere na kuiwezesha timu yake kukwea hadi nafasi ya nne ya msimamo wa Ligi Kuu, ikifikisha pointi 17.

Kwa sasa Polisi Tanzania inashika nafasi ya 15 ambayo ni ya juu kutoka mwisho, ikiwa na pointi sita tu baada ya kucheza mechi 11, ikishinda moja, sare tatu na kupoteza mechi saba.

# FA Cup yarindima, JKT Tanzania yachanua

**Na Adam Fungamwango**

HATUA ya awali ya mechi za Kombe la Shirikisho la Soka nchini maarufu FA Cup, kwa ajili ya kusaka bingwa wa michuano hiyo atakayeiwakilisha nchi kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika, zimeanza rasmi, huku Ligi ya Championship kusaka timu ya kucheza Ligi Kuu msimu ujao nayo ikizidi kupamba moto nchini.

Katika Uwanja wa Minaki Pwani, wenyeji timu ya Kibadeni FC ilichapwa bao 1-0 dhidi ya Tandika United, huku Dimba la Mkwakwani jijini Tanga, wenyeji Misitu FC ikiiadhibu Kawele SC mabao 2-1.

Wakati utepe wa Kombe la FA ukiwa umekatwa na timu hizo mbili zikitinga raundi ya kwanza, Ligi ya Champinship nayo imeendelea tena juzi, kwa JKT Tanzania kuifunga Pan African bao 1-0, mechi ikipigwa Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

Ni ushindi ambao umeipeleka timu hiyo hadi nafasi ya tatu, ikifikisha pointi 19 na kuiengua Mbuni FC iliyotupwa kwenye nafasi ya nne kwa pointi 18.

Mbeya Kwanza ikiwa Uwanja wa Meja Jenerali iliichapa African Sports mabao 2-1 na katika Dimba la Nyamagana jijini Mwanza, wenyeji Pamba walibanwa mbavu, wakilazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Ndanda FC.

Katika ligi hiyo, timu za Ndanda na Gwambina ambazo zimeshawahi kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara kwa nyakati tofauti, zipo hoi.

Ndanda ipo nafasi ya 15 ikiwa na pointi tatu na haijashinda mechi yoyote kati ya nane ilizocheza, huku Gwambina ambayo nayo imecheza idadi hiyo ya mechi ikiwa na pointi nne zinazoifanya kushika nafasi ya 14.

## ZISIKUPITE

**SOUTHAMPTON YATIMUA KOCHA**

KLABU ya Southampton imeamua kumfukuza kazi kocha Ralph Hasenhuttl, baada ya kichapo cha mabao 4-1 kutoka kwa Newcastle United Jumapili na kuiacha klabu hiyo katika hatari ya kushuka daraja. (*Athletic*)

**HAZARD KUREJESHWA EPL**

NEWCASTLE United na Aston Villa zinataka kumrejesha Ligi Kuu ya England (EPL), mshambuliaji wa Real Madrid na Ubelgiji, Eden Hazard mwenye umri wa miaka 31. (*El Nacional*)

**GORDON ATAKIWA SPURS**

KLABU ya Tottenham Hotspur inafikiria kumnunua winga wa Everton, Anthony Gordon mwenye umri wa miaka 21, katika dirisha la uhamisho la Januari. (*Sun*)

**MUDRYK ATAKIWA ARSENAL**

ARSENAL bado inataka kumsajili winga wa Shakhtar Donetsk na Ukraine, Mykhaylo Mudryk, mwenye umri wa miaka 21. (*CaughtOffside*)

**NKUNKU AISIKILIZIA MADRID**

MSHAMBULIAJI wa RB Leipzig, Christopher Nkunku, mwenye umri wa miaka 24, yuko tayari kuisubiri kwanza Real Madrid kabla ya kuamua kama atahamia Chelsea. (*El Nacional*)

**NYOTA ARSENAL NA MIKATABA**

ARSENAL I iko katika harakati za kuwaongezea mikataba mipya mlinzi wa Ufaransa William Saliba mwenye umri wa miaka 21, winga Bukayo Saka (21) na mshambuliaji wa Brazil, Gabriel Martinelli. (Fabrizio Romano)

**GAKPO NA OFA PSV**

MKURUGENZI wa PSV Eindhoven, Marcel Brands, amesema Leeds ilitoa ofa ya pauni milioni 30 pamoja na pauni milioni 11 kama bonasi kwa winga wa Uholanzi, Cody Gakpo, mwenye umri wa miaka 23, katika dirisha la msimu uliopita la majira ya joto. (*ESPN*)

**DAVID AFUATILIWA EPL**

MSHAMBULIAJI wa Lille na Canada, Jonathan David, mwenye umri wa miaka 22, anafuatiliwa na klabu kadhaa za Ligi Kuu England zikiwemo Everton, Tottenham na Arsenal. (*NipeSport*)

**TONEY NA KOMBE LA DUNIA**

MSHAMBULIAJI wa Brentford, Ivan Toney, mwenye umri wa miaka 26, yuko tayari kwenda Kombe la Dunia akiwa na England. (*Sun*)

**ZAHA AITULIZA PALACE**

WINGA wa Crystal Palace na Ivory Coast, Wilfried Zaha, mwenye umri wa miaka 29, anakataa kubashiri juu ya mustakabali wake licha ya mkataba wake kumalizika msimu wa majira ya joto. (*Sky Sports*)

**DIAZ ANUKIA WEST HAM**

KLABU ya West Ham inapanga kumnunua mshambuliaji wa Blackburn Rovers na Chile, Ben Brereton Diaz, mwenye umri wa miaka 23, katika dirisha lijalo la Januari. (*Football Insider*)

**HALL ATAKIWA LEEDS**

LEEDS United inaongoza katika kinyang'anyiro cha kumsajili kiungo wa kati wa Birmingham mwenye umri wa miaka 18, George Hall. (*Sun*)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# ARTETA AWAPIGIA SALUTI NYOTA WAKE ARSENAL

**Kwa timu changa kama hii, ukomavu waliouonyesha, utulivu, uimara na ujasiri wa kucheza...**

**LONDON,** England

MIKEL Arteta ameipigia saluti ya "ajabu" Arsenal baada ya kurejea kileleni mwa Ligi Kuu England kwa ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Chelsea, Jumapili.

Gabriel Magalhaes alifunga bao pekee la ushindi kipindi cha pili, akiunganisha kona ya Bukayo Saka.

Chelsea hawakuwa tishio kwani mbio zao za nyumbani za kutopoteza mechi 12 zilifikia kikomo, huku Pierre-Emerick Aubameyang katika mechi yake ya kwanza dhidi ya klabu yake ya zamani akitolewa kipindi cha pili.

Arsenal walipata ushindi wa tatu mfululizo kwenye Uwanja wa Stamford Bridge kwa mara ya kwanza tangu 1974, na kusonga mbele kwa pointi mbili dhidi ya Manchester City kwenye kilele cha msimamo wa ligi hiyo.

**Kocha Mkuu wa 'Washika bunduki' hao, Arteta anatarajia maonyesho mengine bora zaidi kutoka kwa wachezaji wake na ana imani zaidi kwamba wanaweza kudumu katika mbio za ubingwa.**

Aliiambia BT Sport: "Tulitaka kurejea kileleni, lakini ushindani ni mgumu sana katika ligi hii. Changamoto yetu ilikuwa ni kufika hatua hii na kucheza dhidi ya timu ya juu na kushinda mchezo."

Alipoulizwa ni kipi kilimvutia zaidi, Mhispania huyo alijibu: "Nadhani kwa timu changa kama hii ukomavu waliouonyesha, utulivu, uimara na ujasiri wa kucheza jinsi tulivyotaka kucheza ulikuwa wa ajabu.

"Kushinda dhidi ya wapinzani hawa katika uwanja huu nadhani ni hatua nyingine kwa wachezaji hawa kuendelea kuamini kuwa wanaweza kufanya hivyo kwa shinikizo dhidi ya wapinzani wakubwa na lazima tufurahie."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,048,8

JACKPOT MECHI WIKI HII

TAREHE: 08, 09 NA 10 NOVEMBA 2022

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 08/11/22 | 20:30 | Hannover vs Fortuna Dusseldorf | 2.68 | 3.28 | 2.48 |
| 02. 08/11/22 | 21:00 | Elche vs Girona | 2.90 | 3.20 | 2.42 |
| 03. 08/11/22 | 22:45 | Bournemouth vs Everton | 2.63 | 3.33 | 2.53 |
| 04. 08/11/22 | 22:45 | Birmingham vs Swansea | 2.39 | 3.27 | 2.82 |
| 05. 09/11/22 | 20:30 | Hansa vs Nurnberg | 2.48 | 3.22 | 2.73 |
| 06. 09/11/22 | 20:30 | Jahn Regensburg vs Eintracht Braunschweig | 2.42 | 3.33 | 2.73 |
| 07. 09/11/22 | 20:30 | FC Koln vs Bayer Leverkusen | 2.83 | 3.42 | 2.30 |
| 08. 09/11/22 | 21:00 | Sevilla FC vs Real Sociedad | 2.50 | 3.14 | 2.85 |
| 09. 09/11/22 | 22:00 | Espanyol vs Villarreal | 3.16 | 3.36 | 2.20 |
| 10. 09/11/22 | 22:30 | FC Luzern vs FC Basel | 2.60 | 3.60 | 2.45 |
| 11. 09/11/22 | 22:45 | Wolverhampton vs Leeds | 2.25 | 3.44 | 2.94 |
| 12. 09/11/22 | 22:45 | Shrewsbury vs Oxford Utd | 2.81 | 3.21 | 2.43 |
| 13. 10/11/22 | 21:00 | Rayo Vallecano vs Celta Vigo | 2.27 | 3.15 | 3.20 |

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa
vodacom m-pesa
airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MOURINHO: DYBALA ATARUDI KABLA YA KOMBE LA DUNIA



**ROME, Italia**

JOSE Mourinho alisikitika kukosekana kwa Paulo Dybala baada ya AS Roma kuchezea kichapo cha bao 1-0 dhidi ya Lazio, lakini akafichua matumaini yake kwamba mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina atarejea kabla ya Kombe la Dunia.

Felipe Anderson alitumia makosa ya Roger Ibanez wakati timu ya Maurizio Sarri ilipopata ushindi muhimu dhidi ya wapinzani wao wa jiji moja, Jumapili, na kusonga hadi nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Serie A.

Wakati Lazio hawakuwa na wachezaji wawili mashuhuri, Sergej Milinkovic-Savic na Ciro Immobile kwenye Uwanja wa Olimpico, Roma waliweza kupiga mashuti mawili pekee yaliyolenga lango huku wakifanya kazi ngumu bila Dybala - mfungaji bora wao akiwa na mabao matano ya ligi msimu huu.

"Tulizungumza kuhusu Milinkovic-Savic na Immobile, hatukuzungumza kuhusu Dybala," alisema Mourinho akiwaambia waandishi wa habari baada ya mechi.

"Nadhani yeye ni muhimu zaidi, kwa sababu ndiye anayetusaidia kufunga mabao. Wachezaji fulani wanapokosekana, tunaingia kwenye matatizo."

Dybala amekosekana tangu Oktoba 9, mwaka huu baada ya kupata jeraha la msuli wa paja, lakini Mourinho anatumaini kuwa atarejea dhidi ya Torino Jumapili ijayo, jambo ambalo pia litakuwa ni ngumu kwa Argentina kabla ya safari yao ya Qatar.

"Ni wazi anataka kwenda Kombe la Dunia, ni vigumu kukataa hilo," alisema Mourinho. "Ikiwa kuna mabadiliko mazuri ya jeraha lake, tunatumaini kuwa atarejea Jumapili dhidi ya Torino."

# Ancelotti: Hatusajili Januari

**MADRID, Hispania**

KOCHA wa Klabu ya Real Madrid, Carlo Ancelotti, ameweka bayana kuwa klabu hiyo haina mpango wa kufanya usajili wowote kwenye dirisha dogo la usajili la Januari.

Kocha huyo ameeleza hayo kabla ya mchezo wao wa jana Jumatatu dhidi ya Rayo Vallecano ugenini.

Ancelotti amekua akisisitiza jambo hilo mara kadhaa na hii inatokana na klabu hiyo kuhusishwa na wachezaji kadhaa.

Kocha huyo amekua akiamini kikosi cha klabu hiyo kimeimarika na kina wachezaji wa kujitosheleza kabisa na wenye ubora wa hali ya juu.

Real Madrid imekuwa ikifanya kazi ya kuongeza mikataba kwa wachezaji wake nyota klabuni hapo kama Karim Benzema, Luca Modric na wengine wakiwa kwenye mazungumzo.

Ancelotti ambaye amefanikiwa kuipatia klabu hiyo taji la 14 la Ligi ya Mabingwa Ulaya huku yeye akifikisha mataji manne na kuweka rekodi kuwa kocha wa kwanza kufanya hivyo, anaamini klabu yake ipo kwenye wakati mzuri na ina wachezaji wazuri hivyo haina haja ya kuingia sokoni Januari.



## HABARI MICHEZO

375,802/-

# YANGA YASHAURIWA KUMULIKA KIMATAIFA SI KUIFUNGA SIMBA

**Na Saada Akida**

ALIYEKUWA mshambuliaji wa Yanga, Mkenya Boniface Ambani, amewataka viongozi wa klabu yake hiyo ya zamani kuweka mikakati kwenye mashindano ya kimataifa na kuacha utamaduni wa kusajili kwa ajili ya kuifunga Simba tu kwenye mashindano ya ndani.

Ambani ameyasema hayo baada ya kikosi hicho kushindwa kutinga hatua ya makundi Ligi ya Mabingwa Afrika na kujikuta kikiangukia kucheza mechi ya mchujo kuwania kufuzu hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho.

Yanga waliianza michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika wakiibuka na ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Zalan fc ya Sudan Kusini kabla ya kushinda tena mabao 5-0 mchezo wa marudiano mechi zote zikipigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Baada ya kuvuka hatua hiyo ya awali, raundi ya kwanza ilikutana na wakongwe wa michuano hiyo, Al Hilal ya Sudan, ambapo mchezo wa kwanza uliochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa ililazimishwa sare ya bao 1-1 kabla ya kufungwa 1-0 ugenini na kuangukia Kombe la Shirikisho ambapo kesho inakibarua kigumu ugenini dhidi ya Club Africain ya Tunisia baada ya mechi ya awali hapa nchini kulazimishwa sare tasa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ambani, alisema uongozi wa klabu hiyo unatakiwa kujipanga vizuri mwanzo wa msimu ili kufanya vizuri kimataifa, hivyo unapaswa kufanya usajili wa wachezaji wenye uwezo mkubwa kwa ajili ya michuano hiyo.

Alisema Yanga imekuwa ikishindwa kufanya vizuri kwa sababu ya kutokuwa na mipango ya kuandaa timu ikiwamo kusajili wachezaji ambao wataenda kupambania timu kimataifa.

"Viongozi wa Yanga ni shida hasa upande wa usajili wa wachezaji kwa ajili ya mechi za kimataifa na mipango yao ni kuangalia kuwafunga Simba na kushinda ligi ya ndani tu.

"Tofauti na Simba wametoka huko baada ya kufanya vizuri misimu minne nyumbani na kuweka mipango ya kwa ajili ya kufanya vizuri kimataifa, hivyo [kumulika] usajili na hata mipango yao ya mwanzo wa msimu," alisema Ambani.

Alisema uongozi unatakiwa kufanya usajli mkubwa ukiachilia wale 11 ambao wanacheza kikosi cha kwanza lakini kuna wanaokaa benchi kunatakiwa kuwapo na watu wenye uwezo wa kucheza hizo mechi.

"Yanga wana kila kitu ikiwamo fedha ambazo wanaweza kusajili mchezaji yeyote, kwa mfano ukiangalia safu ya ushambuliaji, Fiston Mayele ni mshambuliaji mzuri, lakini hana mwenzake wa kumsaidia.

Panatakiwa kusajiliwa mshambuliaji mwingine mwenye uwezo kama wa Mayele au zaidi ya hapo. Naamini wakifanya hivyo na maeneo mengine wanaweza kufika mbali. Walisajili kwa ajili ya kuwafunga Simba tu," alisema Ambani.

## KIKAPU...



Vijana wakiwania mpira wakati wakifanya mazoezi ya mpira wa Kikapu katika viwanja vya michezo vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Simba Queens

INATOKA UK. 32

Zambia na Determine Girls ya Liberia wakati Kundi B waliofungasha virago ni TP Mazembe Queens ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na mabingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Misri, Wadi Degla.

Fainali za michuano hii inayofanyika kwa mara ya pili barani Afrika chini ya usimamizi wa CAF, zitafanyika Jumapili na bingwa atazawadiwa kitita cha Dola za Marekani 400,000.

# Yanga mzuka juu

INATOKA UK. 32

alisema.

Kuhusu kukosekana kwa Shaban Djuma katika safu ya ulinzi, Nabi alisema Kibwana Shomari, anaweza kucheza nafasi hiyo kwa ufanisi mkubwa. Akizungumza na gazeti hili jana kwa simu kutoka Tunisia, Nabi alisema licha ya kukosekana Djuma lakini hakutaathiri mipango yao kwani wachezaji wa kuziba nafasi yake wapo akiwamo Kibwana ambaye amekuwa akifanya vizuri.

Alisema wanaingia kwenye mchezo huu wakiwa na lengo moja la kutafuta ushindi, jambo ambalo wanaimani utakuwa mchezo mgumu kwa sababu ya Club Africain nao wataingia kivingine kwa kucheza kwa kushambulia zaidi. "Tutamkosa Djuma kutokana na majeraha yanayomkabili, tuna wachezaji wazuri sana akiwamo Shomari anacheza nafasi hiyo, kushoto yupo Joyce Lomalisa na Faridi Musa, hatuna hofu yoyote,"alisema Nabi.

Yanga inahitaji ushindi au sare yoyote ya mabao kuweza kutinga hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho barani Afrika ambayo droo yake inatarajiwa kufanyika Novemba 16, Makao Makuu ya CAF, Cairo nchini Misri.

Yanga iliangukia kwenye michuano hiyo baada ya kutolewa Ligi ya Mabingwa Afrika raundi ya kwanza kwa jumla ya mabao 2-1 dhidi ya Al Hilal ya Sudan.

## SUPA JACKPOT
## MECHI WIKI HII
### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 12/11/22 | 18:00 | Nottingham vs Crystal Palace | 3.04 | 3.19 | 2.37 |
| 02. 12/11/22 | 18:00 | Bristol City vs Watford | 2.89 | 3.39 | 2.36 |
| 03. 12/11/22 | 18:00 | Bournemouth vs Everton | 2.78 | 3.23 | 2.53 |
| 04. 12/11/22 | 18:00 | Huddersfield vs Swansea | 2.80 | 3.25 | 2.50 |
| 05. 12/11/22 | 18:00 | Preston vs Millwall | 2.41 | 3.13 | 3.03 |
| 06. 12/11/22 | 18:00 | Coventry vs QPR | 2.36 | 3.22 | 3.02 |
| 07. 12/11/22 | 20:00 | Basaksehir vs Galatasaray | 2.42 | 3.40 | 2.80 |
| 08. 12/11/22 | 20:00 | Sampdoria vs Lecce | 2.54 | 3.08 | 2.89 |
| 09. 12/11/22 | 20:00 | FC Sion vs St. Gallen | 2.80 | 3.60 | 2.37 |
| 10. 12/11/22 | 20:30 | Newcastle vs Chelsea | 2.32 | 3.34 | 2.99 |
| 11. 12/11/22 | 22:45 | Bologna vs Sassuolo | 2.38 | 3.34 | 2.89 |
| 12. 13/11/22 | 14:30 | Atalanta vs Inter | 2.90 | 3.54 | 2.29 |
| 13. 13/11/22 | 16:15 | FC Zurich vs Servette Geneva | 2.37 | 3.30 | 2.95 |
| 14. 13/11/22 | 17:00 | Istanbulspor vs Hatayspor | 2.58 | 3.22 | 2.73 |
| 15. 13/11/22 | 17:00 | Kayserispor vs Konyaspor | 2.58 | 3.28 | 2.68 |
| 16. 13/11/22 | 17:00 | Montpellier vs Reims | 2.45 | 3.38 | 2.73 |
| 17. 13/11/22 | 17:30 | Mainz vs Eintracht Frankfurt | 2.44 | 3.41 | 2.72 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMANNE- 08/11/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 3304 | FC Metalist Kharkiv vs FC Metalist 1925 | 1.92 | 3.45 | 3.45 |
| 14:00 | 3660 | FC Ingulets vs Zorya Lugansk | 5.07 | 3.61 | 1.60 |
| 15:00 | 3123 | Shenzhen vs Dalian Aerbing | 2.48 | 3.25 | 2.57 |
| 15:15 | 3491 | Ho Chi Minh City vs SHB DA Nang | 1.63 | 3.80 | 4.49 |
| 15:35 | 5009 | Sur vs Al Nasr Salalah | 4.00 | 2.92 | 1.97 |
| 15:40 | 1572 | Rustaq Club vs Al Nahda (Oman) | 4.10 | 2.70 | 2.20 |
| 16:00 | 2306 | Rudes Zagreb vs Istra | 3.56 | 3.17 | 1.99 |
| 17:00 | 5089 | Spartak Trnava vs Zemplin Michalovce | 1.31 | 4.67 | 7.98 |
| 19:30 | 4878 | Gornik Leczna vs GKS Piast Gliwice | 3.45 | 3.35 | 1.95 |
| 19:45 | 5968 | Jeddah Club vs Najran SC | 1.91 | 3.12 | 3.90 |
| 20:00 | 2844 | Nykobing FC vs Sonderjyske | 5.46 | 4.29 | 1.46 |
| 20:00 | 5067 | Bnei Sakhnin vs FC Ashdod | 2.29 | 3.17 | 2.88 |
| 20:30 | 4525 | Spezia vs Udinese | 4.17 | 3.57 | 1.79 |
| 20:30 | 4892 | VfL Wolfsburg vs Borussia Dortmund | 3.27 | 3.52 | 2.04 |
| 20:30 | 5462 | Napoli vs Empoli | 1.16 | 7.14 | 12.89 |
| 20:30 | 5620 | Vilniaus Riteriai vs Zalgiris Kaunas | 2.53 | 3.07 | 2.63 |
| 21:00 | 1298 | Maccabi Netanya vs Ironi Kiryat Shmona | 1.92 | 3.36 | 3.56 |
| 21:00 | 2476 | Elche vs Girona | 2.89 | 3.24 | 2.40 |
| 21:00 | 2964 | Aris Salonica vs Lamia | 1.50 | 3.72 | 7.15 |
| 21:15 | 4454 | Hapoel Katamon vs Maccabi Tel Aviv | 5.63 | 4.08 | 1.48 |
| 21:45 | 3869 | Gil Vicente vs FC Arouca | 2.18 | 3.12 | 3.12 |
| 22:00 | 2043 | Athletic Bilbao vs Valladolid | 1.43 | 4.49 | 6.79 |
| 22:00 | 2917 | MSK Deinze vs Eupen | 2.81 | 3.40 | 2.30 |
| 22:00 | 3226 | Kecskemeti TE vs Puskas Akademia | 3.31 | 3.40 | 1.98 |
| 22:30 | 1436 | Lechia Gdansk vs Legia Warszawa | 3.26 | 3.40 | 2.00 |
| 22:30 | 4621 | Stuttgart vs Hertha BSC | 1.86 | 3.66 | 3.71 |
| 22:30 | 4901 | Bayern Munchen vs Werder Bremen | 1.16 | 7.70 | 11.85 |
| 22:30 | 4903 | VfL Bochum vs Monchengladbach | 3.51 | 3.66 | 1.92 |
| 22:30 | 5054 | FCV Dender EH vs Standard Liege | 3.60 | 3.65 | 1.87 |
| 22:45 | 1263 | Coleraine FC vs Crusaders Belfast | 2.82 | 3.51 | 2.17 |
| 22:45 | 1402 | Sheffield Utd vs Rotherham | 1.40 | 4.44 | 7.10 |
| 22:45 | 1519 | QPR vs Huddersfield | 1.72 | 3.53 | 4.67 |
| 22:45 | 2265 | Cremonese vs AC Milan | 5.75 | 4.27 | 1.49 |
| 22:45 | 2291 | Brentford vs Gillingham | 1.14 | 7.37 | 16.94 |
| 22:45 | 2453 | Carrick Rangers vs Portadown FC | 1.50 | 4.26 | 5.03 |
| 22:45 | 2532 | Leicester vs Newport | 1.12 | 7.75 | 17.89 |
| 22:45 | 2808 | Larne vs Dungannon Swifts | 1.22 | 5.65 | 9.75 |
| 22:45 | 2860 | Birmingham vs Swansea | 2.39 | 3.27 | 2.82 |
| 22:45 | 3066 | Cardiff vs Hull City | 1.97 | 3.22 | 3.81 |
| 22:45 | 3280 | Blackpool vs Middlesbrough | 2.92 | 3.37 | 2.27 |
| 22:45 | 3339 | Burnley vs Crawley Town | 1.22 | 5.80 | 12.00 |
| 22:45 | 3343 | Bournemouth vs Everton | 2.70 | 3.30 | 2.50 |
| 22:45 | 4089 | Livingston vs Aberdeen | 2.83 | 3.18 | 2.45 |
| 22:45 | 4479 | Linfield Belfast vs Cliftonville Belfast | 1.99 | 3.40 | 3.30 |
| 22:45 | 4784 | Hibernian vs Ross County | 1.53 | 3.93 | 5.97 |
| 22:45 | 5795 | Glenavon vs Glentoran Belfast | 4.46 | 3.98 | 1.60 |
| 23:00 | 1322 | Watford vs Reading | 1.81 | 3.41 | 4.26 |
| 23:00 | 1777 | Newry City AFC vs Ballymena Utd | 2.49 | 3.47 | 2.44 |
| 23:30 | 3825 | Osasuna vs Barcelona | 5.63 | 4.22 | 1.53 |
| 23:45 | 3623 | Mafra vs Porto | 11.66 | 5.64 | 1.20 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumanne Novemba 8, 2022
Nipashe



UKURASA 29

**Arteta awapigia saluti nyota wake Arsenal**

**TUPO TAYARI...**



Wachezaji wa Yanga mazoezini, kesho watashuka katika Uwanja wa Olympique Hamadi Agrebi jijini Tunis, Tunisia kuivaa Club Africain kwenye mechi ya mchujo ya marudiano kuwania kufuzu hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika. **PICHA: YANGA**

# YANGA MZUKA JUU

## ●●●Nabi aongeza ufundi wa kuivaa Club Africain, wachezaji mastaa watoa darasa kwa...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

KATIKA kuhakikisha wanapambana kuanzia nje ya uwanja hadi ndani kwenye mechi ya marudiano ya mchujo kuwania kushiriki hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika, wachezaji wazoefu wa michuano ya kimataifa ndani ya kikosi cha Yanga, wameungana na benchi lao la ufundi katika kujenga hali ya upambanaji dhidi ya Club Africain ya Tunisia kesho.

Wakati Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi na wasaidizi wake wakiongeza dozi ya mazoezi kwa kuwataka wachezaji kucheza kwa kasi mazoezini ili waweze kumudu mchezo huo, wachezaji wazoefu wa mechi za kimataifa akiwamo Stephane Aziz Ki, wamekuwa wakiwaelekeza wachezaji wenzao namna ya kukabiliana na timu za aina hiyo ya Club Africain.

Yanga inatarajia kuondoka leo mjini Sousse ilipoweka kambi, kuelekea Tunis umbali wa takriban Km. 140, ambako itachezwa mechi yao hiyo ya marudiano dhidi ya Club Africain baada ya mechi ya kwanza Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, timu hizo kutoka suluhu.

Akizungumza kutoka nchini humo jana, Ofisa Habari wa klabu hiyo, Ali Kamwe, alisema siku ambazo wamekaa Sousse aliona mazoezi yaliyokuwa yanatiliwa mkazo zaidi na kocha wao, Nabi ni ya kasi, wachezaji wakitakiwa kucheza kwa kasi kwani anajua wapinzani wao watakuwa na aina hiyo ya mchezo.

"Alichokuwa akisisitiza na kukifundisha ni kasi kwa wachezaji wake kabla ya kuelekea kwenye mchezo siku ya Jumatano (kesho), kocha amekuwa akiwaongezea kasi wachezaji wake kwa sababu awali walionekena kuchoka kutokaa na safari ndefu hadi kufika hapa, lakini pia uchezaji wa timu za Afrika Kaskazini wanapokuwa nyumbani wanakuwa na kasi sana wakiwatumia mawinga wa pembeni," alisema Kamwe.

Alisema hata baadhi ya wachezaji ambao ni wazoefu wa michuano hiyo na kucheza na timu za aina hiyo wakiongozwa na Aziz Ki wamekuwa wakiwaelekeza wachezaji wenzao namna ya kukabiliana na timu za aina hiyo, pamoja na kucheza chini ya presha ya mashabiki waliojazana uwanjani, wakishangilia bila kupumzika.

"Wachezaji wamekuwa wakielekezana wenyewe kwa wenyewe, wale waliopata bahati ya kucheza mechi ambazo zina presha ya mashabiki wamekuwa wanawaambia wenzao ni kitu gani wataenda kukutana nacho uwanjani mbele ya mashabiki hao, lakini nini cha kufanya ili kuepukana na presha yao. Kingine ni kwamba mchezaji wetu Aboubakar Salum 'Sure Boy', ambaye alikuwa majeruhi, ameanza mazoezi na wenzake na ameonyesha kiwango kizuri kwa hiyo yuko fiti ni jukumu tu la mwalimu kama anaweza kumtumia,"

INAENDELEA UK. 31

Nabi

## Simba Queens kumenoga CAF

**Na Somoe Ng'itu, RABAT**

WAKATI kikosi cha Simba Queens kimefika salama jijini hapo (Rabat), kikitokea Marrakech tayari kwa ajili ya mchezo wa hatua ya nusu fainali, nahodha wa timu hiyo, Oppah Clement, amesema sasa kiu yao ni kutwaa ubingwa wa michuano hiyo ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake.

Simba Queens itaikabili Mamelodi Sundowns Queens kutoka Afrika Kusini katika mechi ya hatua ya nusu fainali ya kwanza itakayochezwa kesho kuanzia saa 11:00 jioni hapa Morocco sawa na saa 1:00 usiku kwa Tanzania.

Akizungumza na gazeti hili jana, Oppah, alisema morali ya wachezaji imeongezeka baada ya kutinga hatua ya nusu fainali na sasa kila mmoja anasema hakuna kisichowezekana.

Mshambuliaji huyo alisema wamewaona wapinzani wao katika mechi mbalimbali walizocheza kabla na baada ya kufika Morocco, hivyo anaamini benchi la ufundi litawapa mikakati ya kuwadhibiti na hatimaye kusonga mbele.

Nyota huyo alisema hana wasiwasi na mchezo huo kwa sababu mechi zote walizocheza walikutana na ushindani, hivyo wamejiandaa kupambana ili kupata matokeo chanya.

"Kwanza malengo yetu yalikuwa ni kutinga hatua ya nusu fainali, tumeshaingia, akili yetu sasa imegeukia katika kuuwaza ubingwa, tunaamini tunaweza kuendelea kuweka rekodi nzuri huku tukishiriki kwa mara ya kwanza mashindano haya," alisema mshambuliaji huyo.

Naye Rais wa Heshima wa Simba, Mohammed 'Mo' Dewji, alikipongeza kikosi cha Simba Queens kwa hatua waliyofikia na kusema wameipa klabu na Tanzania heshima kubwa.

"Hongereni sana Simba Queens kwa kutinga hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake, kwa mara ya kwanza, Mmefanya tujivunie, nusu fainali tunakuja," alisema Mo Dewji ambaye ni shabiki mkubwa wa klabu hiyo ya Mtaa wa Msimbazi, Kariakoo Dar es Salaam.

Nusu fainali nyingine ya mashindano hayo itakayochezwa kuanzia saa 4: 00 usiku kwa saa za Tanzania itawakutanisha wenyeji, ASFAR FC dhidi ya Bayelsa Queens kutoka Nigeria, mechi zote zikifanyika kwenye Uwanja wa Prince Heritier Moulay El Hassan.

Timu zilizoyaaga mashindano haya kutoka Kundi A ni Green Buffalo kutoka

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >